# NAHJUL BALAGHA

## JUZUU YA PILI

### MTARJUMI: HARUNA PINGILI

**NENO LA MCHAPISHAJI**

Kitabu kilichoko mkononi mwako ni tarjumi kutoka lugha ya Kiarabu ya kitabu maarufu katika ulimwengu wa Kiislamu, Nahju 'l-Balaghah. Kitabu hiki kitachapishwa katika juzuu mbili, na hii uliyo nayo mkononi ni juzuu ya pili.

Nahju 'l-Balaghah ni mkusanyiko wa khutba, barua na maelekezo ya Imam Ali (a.s). Mengi yamesemwa kuhusu ubora na ufasaha wa maneno yaliyomo katika khutba na harua hizo. Kwa ufupi, Nahju 'l-Balaghah ni kilele cha ufasaha.

Mbali na mawaidha yaliyomo humo, msomaji atafaidika na lugha iliyomo katika khutba na barua hizo, hususan kwa wasomaji wa Kiarabu. Inasemekana kwamba baada ya Qur'ani Tukufu na maneno ya Mtukufu Mtume **(s.a.w.w)**, Nahju 'l-Balaghah ndiyo inayofuatia kwa ufasaha na ubora wa maneno.

Si rahisi kwa msomaji wa Kiswahili kupata ladha ileile aipatayo msomaji wa Kiarabu kutokana na ukweli kwamba lugha ya Kiarabu ni pana mno na msamiati wake ni mkubwa. Pamoja na hayo, mtarjumi wetu amejitahidi sana kuleta mafhumu ya Kiarabu kwenye lugha ya Kiswahili bila kupoteza maana. Kwa vile kitabu hiki ni muhimu sana, tumeona ni bora tukichapishe katika lugha ya Kiswahili ili Waislamu na wasomaji wetu wazungumzao Kiswahili wapate kunufaika na yaliyomo humo. Hivyo, ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakkuwa ni chenye manufaa sana kwao na katika jamii yetu.

Tunamshukuru ndugu yetu, Sheikh Haruna Pingili kwa kukubali jukumu hili kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiri- ki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

## DIBAJI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu. Kwanza yanipasa nimshukuru Mwenyezi Mungu Jalali, asiye kuwa na mithali, kwa neema zake za kila hali na kila mahali, hata nikaweza mimi mja mpungufu, kutimiza kazi hii tukufu ya kuipitia tarjuma hii ya Kiswahili ya Nahju 'l-Balaghah.

Nahju 'l-Balaghah ni jina la diwani mashuhuri yenye khutba, uweza wa kusema, na barua za Imam Alî bin Abu Talib (a.s). Haya yote yamekusanywa na Sharîf Ar-Radhi. Diwani hii yenye khutba takriban 237, baru 79 na mithali 480 ilikamilika mwezi wa Rajab 400 A.H./1009 A.D. Maana ya NAHJ ni njia iliyo wazi, au barabara kuu; na maana ya Balaghah ni ufasaha (wa lugha) au ilimu ya usemaji, n.k. Kwa hivyo Nahju 'l-Balaghah yaani Barabara kuu ya ufasaha.

"Huyu Imam 'Ali ni nani? Ni vigumu mno kuzitaja sifa zake kwa ukamilifu. Yeye alikuwa mtaalamu, shujaa na khatibu kuliko wote. Uchamungu wake, mapenzi yake ya Mwenyezi Mungu, uaminifu wake na ushupavu wake wa kufuata dini ulikuwa wa darja ya juu kuliko mtu yeyote ...... akichukia diplomasia (ujanja), na akipenda haki na insafu. Sera zake ni kama zilivyoamrishwa na Mwenyezi Mungu. Wataalamu wa Kiyahudi na wa Kikristo wakijaaliwa kujua daraja ya ilimu yake huisujudia ilimu hiyo isioweza kufananishwa.

Wafalme wa Ki-Rumi wangependa kuzitundika picha zake katika kasri zao, na maaskari wakubwa wa vita wangependelea kulichonga jina lake kwenye panga zao.

لا فتي الاَّ عَلِيَّ وَ لاَ سَيْفَ اِلاَّ ذُو الْفقار.

"Hayuko kijana shujaa mfano wa 'Ali! wala hakuna upanga mfano wa Dh-ul-Faqar (upanga wa Imam 'Alî (a.s) aliorithi kwa Mtume)."

Allama Mustafa Beck Najeeb wa al-Azhar, Cairo amesema:

خَرَجَ اَلي الدُّنْيَا وَ الثَّهَادَةُ مَكْتُوْبَةً علي جَبْيْنه و خرج منْهَا و الثَّهادَةُ مكْتُوْبَةً علي ذلكَ الجَبْيْن بضَــرْبَه حُسَّـا مٍ لَقدْ كَمَا علمْنَا في الْكَعْبَه وَ ضُــرب كَم عَلِمْنَا فِي الْمَسْــجِد فَأَيَّه بدَايَهٍ وَ نِهايَهٍ اَبْه بالْحَيَاة الّتي بيْنَهُمَا مِنْ تلْك الْبدَايَه وَ تلْكَ النَّهَايَه؟

"Imam 'Alî amekuja duniani na shahada imeandikwa kwenye kipaji chake; na ameondoka duniani na shahada vile vile imeandikwa kwenye hicho kipaji kwa dharba ya upanga. Kama tunavyojua amezaliwa ndani ya Ka'bah, na kama tujuavyo amepigwa dharba (ya upanga) msikitini. Ilioje ajabu? Mwanzo wake na mwisho wake kupata darja ya kifo cha kishahidi."

Sheikh Abbas Mahmud al-Aqqad - mwandishi maarufu wa Ki-masri amesema:

"Mtu yeyote ambaye amebobea katika lugha ya Ki-arabu atakubali tu kwamba Nahju 'l-Balaghah inafuata kwa ubora wake baada ya maneno ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

Maneno ya 'Alî ni yenye maana na fikra nzito. Kwa hivyo Nahju 'l-Balaghah lazima isomwe kwa makini, na irejewe na idondolewe na wanafunzi na walimu. Ninapenda kutilia mkazo kwamba Nahju 'l-Balaghah iingizwe kwenye mukhtasar wa masomo na mafundisho (syllabi) ya vyuo vikuu vyote vya Masri na Beirut kwenye masomo ya kiwango cha juu ya lugha na falsafa."

Sheikh Muhammad 'Abdo - Mufti wa Masri na Profesa wa lugha ya Kiarabu na falsafa amesema:

تَحْتَ كَلاَمِ الْخَالِقِ وَ فَوْقَ كَلا مِ الْمَخْلُوق.

"Mtu yeyote hawezi kukataa kwamba 'Alî alikuwa Imamu wa makhatibu, mwalimu na kiongozi wa waandishi na wanafalsafa. Bila ya shaka khutba zake na maneno yake ni yenye kiwango cha juu kabisa kushinda maneno ya mtu ye yote isipokuwa maneno ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake:"

'Abd-ul-Masîh al-Antaqi - Mhariri wa Kikristo wa gazeti la Ki-masri Al-Ahram amesema:

'Alî alikuwa Imamu kwenye nyanja za vita, Imamu wa siasa, Imamu wa dini, Imamu wa falsafa, Imamu wa maadili, Imamu wa maandiko mbali mbali, na Imamu wa ilmu na hikma."

Profesa Muhammad Kamil, Cairo amesema:

فَاِ دَا لَمْ يَكُنْ عَلِيّ نَبِيًّا فلَقدْ كَانَ خُلُقُهُ نَبَوِ يَّا.

"Ijapokuwa Imam 'Alî alikuwa si nabii, lakini khulqa yake ilikuwa ya kinabii."

Shaykh Nasif al-Yazidi alipokuwa akimwaidhi mwanawe alimwambia: “Kama unataka mamlaka ya juu kabisa dhidi ya wenzako katika masomo, hikma, maandiko, inshaa n.k. basi hifadhi Qur'ani Tukufu na Nahju 'l-Balaghah”.

Amîn Nakhlah anasema: “Mtu yeyote anayetamani kuikata kiu yake (ya kiroho) kwa maneno ya 'Ali (a.s) lazima ausome kila ukurasa wa Nahju 'l-Balaghah kwa uangalifu.

Nahju 'l-Balaghah ni diwani ambayo humfanya kila mtu kuukubali ubingwa wa Imam 'Ali (a.s). Hakuna kitabu kinachoweza kuishinda Nahju 'l-Balaghah isipokuwa Qur'ani Tukufu.

Humo ndani ya Nahju 'l-Balaghah utazikuta lulu za maarifa zilizotungwa kwenye mikufu mizuri, utayakuta maua ya lugha ambayo huifanya akili ya binadamu inukie kwa harufu nzuri ya ushujaa na uungwana; vile vile humo utaikuta mito ya lugha safi ambayo ni mitamu na baridi zaidi kuliko mto wa al-Kauthar.

Imam 'Alî (a.s) anawaidhi juu ya maudhui mbali mbali, k.m. Kuumbwa kwa ardhi na mbingu, tawhîd, taqwa, malaika, zuhd, Qiyamah, kiburi, tamaa, vita vya Jamal, Siffin, Nahrawan, ibada, maarifa, tamaa, imani, insafu, n. k.

Katika mithali yake mashuhuri Imam 'Alî (a.s) anatuwaidhi sisi wanaadamu kutobaguwana kwa makabila.

"Watu kwa makamu ni sawa sawa
Baba ni Adamu na mama Hawa
Ukijia'dhimu kwa kuzaliwa
Maji na kinamu uliumbiwa
Fahamu na jua mwana Adamu"

Maneno haya ya Sayyidna 'Alî yamo katika msingi wa Qur'ani Tukufu. (Sh. 'Alî Muhsin al-Barwani).

Tunatumai wasomaji wetu watastafidi sana na tarjama hii ya Nahju 'l-Balaghah (kwa lugha ya Kiswahili) ambayo imefanywa kwa kifundi na ujuzi

mkubwa. Mwenyezi Mungu atujaalie tawfiq ya Kutenda Kheri na atuepushe na kila shari.

Wa Billahi Tawfîq,

Dr. Ja'far A. Tijani.

# NAHJUL BALAGHA

## JUZUU YA PILI

### MTARJUMI: HARUNA PINGILI

## 56 - NA MIONGONI MWA MANENO YAKE (A.S)

Na miongoni mwa maneno yake (a.s) - Zamakhshari ameieleza hotuba hii katika Rabiul-Abraar, mlango wa Al-qatil wa shaha- da. Na ibn Muzahim katika kitabu Swifiin, uk. 520.

### SIKU YA SIFFIIN ALIPOWAAMURU WATU KUFANYA SULUHU

"Kwa hakika tulikuwa na Mtume wa Mungu **(s.a.w.w)**; tunawaua baba zetu na watoto wetu na ndugu zetu na ammi zetu. Hilo lilikuwa halituzidishii kitu isipokuwa imani na kusalimu amri, na kuendelea ndani ya njia ya sawa na kuvuta subira kwa machungu yake na umakini katika kumpiga vita adui. Alikuwa mtu kutoka upande wetu na mwingine kutoka kwa adui yetu wanashambuliana kama wanavyoshambuliana maksai wawili kwa pembe wakitoana nafsi zao, yupi miongoni mwao atawahi kumnywesha mwenzake kikombe cha umauti, basi mara ilikuwa sisi twafanikiwa dhidi ya adui yetu na mara nyingine anafanikiwa adui yetu dhidi yetu, Mungu alipoona ukweli wetu aliwateremshia adui zetu udhalili na kutelekezwa, na aliteremsha kwetu nusura, kiasi cha Uislamu kuimarika na kumakinika na kukaa mahali pake.

"Namuapa Mungu lau tungekuwa tunayafanya mliyoyafanya, dini haingekuwa na nguzo[1], ya kutuwama wala imani tawi lake halingesitawi. Wallahi mtamkamua damu[2] na mtamfuatilia na majuto[3]."

## 57 - NA MIONGONI MWA MANENO YAKE (A.S)

Na miongoni mwa maneno yake (a.s) - Khutba hii ameieleza Al-Baladhuriy ndani ya Ansabul-Ashraafi) katika tarjuma ya Ali (a.s), na Al'Haakim ndani ya Al'Mustadrak, Jz. 2, uk. 385, na At-Tuusi ndani ya Al-Amaali uk. 214 na 347, na wengine.

---

1. Maneno haya kwa utaratibu ujulikanao kwa: Istiara yaani neno huazimwa na kutumika mahali sio pake, mfano: kuimarika kwa Uislamu ametumia neno:
Mathbuta asili ya maana yake: jiiranu ni sehemu ya mbele ya shingo ya ngamia kutokea sehemu anayochinjwa mpaka kooni, ila hapa limetumika kumaanisha kuimarika kwa Uislamu. Hivyo basi Uislamu umeimarika na kuthibiti kama ngamia anapoitupa shingo yake ardhini tayari kwa kuchinjwa, pia neno: Mutabawau awtami limetumika mfano wa mwili unapochukua nafasi ya kuishi nyumbani kwake, na neno Maqamaliddin umuuda ameifanya dini mfano wa nyumba inayosimama juu ya nguzo. Ameifananisha dini na mti wenye matawi yawezayo kusitawii.

2. Mutamkamua damu, mfano huo huambiwa Alie lifuja jambo: (utakamua damu) na asili yake ni ngamia endapo mkamuwaji atapita kiwango kumkamua kiasi cha kwisha maziwa na kuanza kutoa damu. Hivyo basi kukamua damu ni mfano wa kujikokotea matokeo mabaya wao wenyewe kutokana na matendo yao, kwa hiyo hayo matendo yatafuatiwa na majuto mzunguko wa mambo utakapowasibu nyumbani kwao.

3. Maneno haya aliasema Amirul'Mu'minina (a.s.) kuhusu kisa cha Abdullah ibn Aamir Al-Hadramiy alipokuja Basra kwa upande wa Muawiyah, Amirul-Mu'minina (a.s.) ali-wahimiza swahaba zake kwenda Basra; Hawakumwitika.

## AKIWAPA HABARI KUHUSU MTU ATAKAYEAMRISHA ATUKANWE IMAM (A.S)

"Punde baada yangu atapata ushindi juu yenu mtu mwenye koo pana, tumbo kubwa, ala akionacho, na huomba asichoweza kukipata, basi muuweni, na hamtomuuwa [1] . Lo! Kwa hakika yeye atawaamrisheni mnitukane, na kujiepusha na mimi; ama kuhusu kutukana nitukaneni, kwa kuwa hiyo kwangu ni utakaso na kwenu ni uwokovu; ama kuhusu kujiepusha na mimi; wala msijiepushe na mimi; kwa kuwa mimi nimezaliwa ndani ya fitra na kutangulia katika imani na hijra.[2]"

## 58 - NA MIONGONI MWA USEMI WAKE (A.S)

Na miongoni mwa usemi wake (a.s) - Ibn Qutaybah ameieleza ndani ya Al'Imama was-siasa Jz. 1, uk.124. Na Sibtu Ibnul'Jauziy katika Tadhkiratul'khawasi uk.100.

Aliwasemesha Khawarij

"Tufani iwakumbeni, wala asibakie miongoni mwenu chakubimbi. Hivi baada ya imani yangu kwa Mungu, na jihadi yangu pamwe na Mtume wa Mungu **(s.a.w.w)** nijishuhudie binafsi kuwa ni kafiri!

قَدْ ضَلَلْتُ إِذًا وَمَا أَنَا مِنَ الْمُهْتَدِينَ ﴿٥٦﴾

"Hivyo basi nitakuwa nimepotea wala sitokuwa miongoni mwa walio ongoka." (6:56).

Rejeeni marejeo ya shari, rejeeni mkifuata athari ya nyayo. Angalieni! kwa hakika mtapata udhalili baada yangu wa sura ya jumla, na upanga mkali wenye kukata, na hilo litachukuliwa na wadhalimu hao kwenu kuwa ni sunnah.[3]".

**Maelezo**

Ar-Radhiy (r.a) amesema: Usemi wake (a.s) huelezwa katika njia tatu: Iwe kama tulivyosema: kwa raa, kutokana na kauli yao kwa mtu ambaye anapandikiza mtende, yaani yuautengeneza vizuri. Na yaelezwa kwa na yakusudiwa kwalo yule aelezaye Hadithi, na kuizungumzia na hii ndiyo njia sahihi kwa maoni yangu. Kama kwamba (a.s) amesema: Habakii kati yenu msimuliaji. Na huelezwa kwa tamko kwa nayo hukusudiwa mwenye kuchupa na mwenye kuhiliki pia huambiwa.

---

1. Haipingani kati ya kuamrisha kitu na kutoa habari kwamba hakitatokea. Kama ambavyo Mungu swt. amesema: "Fatamannawul-mauta inkutum swadiqiina. Walaa yatamannawunahu abada......." Myatamani mauti kama ninyi ni wakweli. Wala hawayatamani kamwe. (Al-Jumu'a; 62: 6 na 7).

2. Huenda ukamtukana mtu ukiwa umelazimishwa na huku umeficha upendo wake, kwa hiyo hiyo utaiepuka shari ya aliyekulazimisha, na hakukulazimisha ila umtukane isipokuwa anayelitukuza suala lake na yu ataka kumdhalilisha, na huo ni utakaso kwa mwenye kutukanwa. Ama kujiepusha na mtu ni kujivua mbali na madhehebu yake.

3. Aliwaonya kwa watakayokutana nayo miongoni mwa matokeo mabaya, ya kunyimwa ngawira na kuhusika wao (wanyimaji) wenyewe na faida za mali mbali na wao, na kunyimwa kwao kila aina na haki.

## 59 - NA ALISEMA (A.S)

Alipoazimia Kuwapiga Vita Khawarij, Na Aliambiwa: Kwa Hakika Hawa Watu Wamekwishavuka Daraja La An-Nahrawaan

Hapo alisema: "Maangukio yao ni chini ya nutfa, Wallahi hawaponyoki kumi miongoni mwao,[1] na wala hawatokufa isipokuwa kumi miongoni mwetu." Sharifu Ar-Radii (r.a) amesema: nutfa anakusudia maji ya mto wa Furaat na hili ni jina mbadala zuri mno kwa maji japo maji yawe mengi. Na hilo tuliliashiria hapo nyuma wakati wa kulipita linaloshabihiana nalo.

## 60 - NA AMESEMA (A.S)

Na Alisema (a.s) - Ameieleza al-Mubaridu katika al-Kamil Jz. 2, uk. 120, na al-Baihaqiy katika al- Mahasin wal Masawi uk. 380, katika mlango Mahasinus-Swidiqi, na Mas'ud katika Muruj al-Dhahab, Juz. 2, uk. 416.

Walipouliwa Khawarij Aliambiwa: "Ewe Amirul-Mu'minina, Hawa Jamaa Wameangamia Wote!" Ndipo Aliposema:

"Lahasha wallahi: wao ni nut'fah ndani ya migongo ya wanaume na mifuko ya uzazi ya wanawake, na kila kiongozi akijitokeza[2] kati yao hukatwa mpaka wa mwisho wao wawe wevi vibaka".

## 61 - NA ALISEMA (A.S.)

### KUHUSU KHAWARIJ

"Msiwapige vita Khawarij baada yangu; kwa kuwa sisawa kati ya mwenye kuutafuta ukweli na akakosea na ambaye ameitafuta batili na kuipata (amkusudia Muawiya na sahaba zake).[3]".

## 62 - NA KATIKA MANENO YAKE (A.S)

Na Katika Maneno Yake (a.s) - As-Saduq ameinakili katika Man laa Yahdhuruhu al-Faqih, jalada la kwanza, uk. 329, na Abu Na'im katika al-

1. Habari hizi ni miongoni mwa habari ambazo zinakaribia kuwa zimezagaa; kwa umashuhuri wake na kunakiliwa kwake na watu wote; nayo ni miongoni mwa miujiza yake na habari zake za ufafanuzi wa mambo yaliyoghibu. Kwa kuwa hakuokoka miongoni mwao ila watu tisa na wametawanyika katika nchi, na hawakuuliwa katika as'habi wa Amirul-Mu'minin ila wanane.

2. Yaani kila ajitokezapo raisi kati yao huuliwa, mpaka mwishowe mambo yao yaishie kuwa wevi na vibaka, hawatokuwa wafalme, wala hawatopata nusra ya kufikia kufanya madh'habu, wala hawatolingania itikadi, hali yao ni hali ya watu wa shari maharamia wajinga.

3. Madhumuni yake ni kuwa Khawarij wamepotea kwa mkanganyiko uliowaingia, na walikuwa waitafuta haki, hali wao kwa jumla ni wenye kushikamana na dini, na wenye kuihami itikadi waliyoiamini, japokuwa walikosea katika hilo; na kuhusu Muawiyah hakuwa yu atafuta ukweli, bali alikuwa mwenye batili, alikuwa haihami itikadi aliyojijengea kwa mkanganyiko. Hivyo basi wao waliamini kwamba kujitoa katika utii wa Imam ni miongoni mwa ambayo dini inawajibisha juu yao. Wao - yaani Khawarij - walikuwa wametafuta ukweli unaokubalika kisheria, wakakosea usawa wake humo, lakini wao baada ya Amirul-Mu'minina watatoka wakiwa na dhana yao hii kumwendea aliyepata ushindi wa uamiri bila ya haki, nao ni wafalme walioutaka ukhalifa kwa njia ya batili na wakaudiriki hali wakiwa sio wastahiki. Hivyo basi Khawarij pamoja na ambayo waliyonayo wako katika hali nzuri kuliko wao (wakina Muawiyyah).

Hiliyatu, jalada la kwanza, uk. 77, na at-Tusi katika al-Misbahu, uk. 461, na al-Mufid katika al-Amaal, uk. 87.
Pindi Alipohofishwa Kuuliwa Ghafla (Akasema)
"Kwa hakika mimi nina ngao madhubuti kutoka kwa Mungu, siku yangu itakapokuja itajitoa mbali na mimi na kuniachia; wakati huo mshale hautokosea wala jeraha halitopona."

### 63 - NA MIONGONI MWA SEMI ZAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Semi Zake (a.s) - Ameieleza Zamakhshari katika Rabiul-Abrar, na ameieleza mwanzoni mwake Ibn Kathir katika al-Bidaya wan-Nihaya: Jz. 8, uk. 12.

### AHADHARISHA FITNA ZA DUNIA

"Lo! Kwa kweli dunia hii ni mahali ambapo usalama haupatikani ila mtu akiwa yumo humo,[1]tendo lililofanywa kwa ajili ya dunia tu haliokoi[2].

Watu wamekabiliwa na mtihani wa maafa, walivyovichuma humo kwa ajili yake (ya dunia) watatolewa nje yake (kwa kifo) na kuhesabiwa dhidi yao[3], na walivyovichuma kutoka humo (kwa kutenda mema) si kwa ajili ya dunia - kwa ajili ya ya akhera - watavipata, na kubaki navyo humo; kwa kuwa hiyo – dunia - kwa wenye akili ni kama kivuli mara chajitanuwa na kujieneza punde chajikunja na kupungua." Ameitaja al-Amidi katika kitabu Ghurarul-Hikami, chini ya herufi 'inna.'

### 64 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Khutba Zake (a.s) - Ameieleza ibnul-Jauz katika Tadhkira yake, uk. 145, na ameitaja al-Aamidi katika al- Ghuraru wal-Duraru.

### KUHUSU KUJIANDAA KWA AJILI YA MAUTI:

"Mcheni Mungu enyi waja wa Mungu, zitanguliyeni ajali zenu kwa matendo yenu (mema), na mnunuwe kinachobaki kwa ajili yenu kwa

---

1. Maneno yakadiriwa hivi: Kuwa dunia - mtu hatobakishwa salama na adhabu ya dhambi za dunia (huko akhera) ila humu humu -duniani - kwa kuwa adhabu inayostahili hufutwa kwa kupatikana mojawapo kati ya mawili: Aidha kwa thawabu kwa ajili ya utii, au kwa toba yenye masharti kamili, na hayo mawili yote hayapatikani ila katika nyumba ya taklifu ambayo ndiyo dunia. Kwa hiyo mwenye kutaka kusalimika na maafa yake na aandae sababu za kusalimika, nazo hupatikana humo duniani kwani baada ya mauti haiwezekani kuyadiriki mtu yaliyompita, wala majuto hayatofaa kitu.

2. Hapana njia za uokovu ila kwa matendo mema ambayo kwayo hukusudiwa Mwenyezi Mungu na si vinginevyo, ama ayafanyayo kwa malengo ya dunia sio njia ya uwokovu.

3. Walichokichukua kutoka humo duniani kwa ajili ya hiyo dunia, mfano wa mali anaya-hodhi kwa ajili ya ladha, na anayamiliki kwa ajili ya kutekelaza matamanio, na waliyoyachukua, si kwa ajili ya dunia, mfano wa mali ayatumiayo katika njia ya heri, atapewa aliyenayo huko akhera thawabu zake ambazo ni neema za kudumu.

kinachowatokeni[1], tokeni kwani mmehimizwa[2], na jiandaeni kwa ajili ya umauti kwani hakika umewakurubia, na muwe kaumu ya watu waliopigwa kelele wakaamka[3], na wakajua kuwa dunia kwao sio nyumba ya kubaki na wakaibadili; kwa kuwa Mungu (s.w.t) hakuwaumbeni kwa mchezo bila ya lengo[4], na wala hakuwaacheni bure[5], na hakuna kitu (kinachozuia) kuingia mmoja wenu jannah au moto ila ni mauti[6].

Na kwa kweli ni lengo linalopunguzwa na muda mfupi mno, na kubomolewa na saa, kadiri [7] inayopunguzwa na punde na kuharibiwa na saa yabidi izingatiwe kuwa ni fupi mno.

Na hakika ghaibu inayosukumwa na mabadiliko mawili mapya, yaani usiku na mchana, ni ya haraka mno kurejea. Msafiri anayerudi ama amefaulu au kutofaulu yu astahiki kuandaliwa masurufu bora.

---

1. Yaani: Inunueni akhera ambayo ndiyo yenye kubaki kwa dunia yenye kwisha na kutoweka yaani: Nunueni kinachobaki miongoni mwa neema za kudumu kwa kinachokwisha miongoni mwa ladha za maisha ya dunia na matamanio yake yaishayo.

2. Mmehimizwa kuondoka na mmesumbuliwa kwa hilo; husemwa: Juddar-Rahim, wa qad’judda bi fulani: akisumbuliwa na kuhimizwa kuondoka, au ameharakia anayekuondoeni hali ninyi hamtambui. Na muradi wa hayo hapa, ni ulazima wa kuandaa masurufu ambayo hapana budi kwa msafiri, na masurufu katika msafara wa kuiaga dunia sio kingine ila ni uchamungu.

3. Yaani kuweni watu wenye hadhari pindi mghafiliko ukiwalaza kipindi fulani, kisha wito wa muwaidhi ukiwaita wanazinduka toka usingizi wao na wainuka kutafuta jinsi watakavyo okoka.

4. Abathu: Mchezo au kufanya jambo bila ya lengo (liingialo akilini) Mungu yu mtukufu mno si wakufanya kitu abathan (bure tu), kwa kweli amemuumba mwanadamu, na amemtunukia nguvu za akili ambayo inafanya kila ladha ya kidunia mbele yake iwe si chochote, wala haiweki utashi wake kwenye mipaka yake, japo daraja yake iwe ya juu kiasi gani, kana kwamba imeumbwa ili ikidharau kila inachokutana nacho katika maisha haya, na kutafuta kila lengo la hali ya juu liwezekanalo. Kwa hivyo lengo hili la kimaumbile Mungu (swt) hakulifanya liwe abathan, bali ni dalili ya kimaumbile ya ndani kwa ndani inayoelekeza kilicho nyuma ya maisha haya.

5. Lam yatrukukum sudaa: hakuwaacheni mkiwa mmetelekezwa, (bure) bila mwangalizi awezaye kuwakemea yanayowadhuru na kukuongozeni kwenye yanayowanufaisha. Na waangalizi wetu ni manabii na waandamizi wao (juu yao rehema na amani iwafikie).

6. Yaani hapana kiziwizi kwa yeyote cha kuingia peponi isipoikuwa afikiwe na mauti, endapo atakuwa amefanya maandalizi yake. Wala kiziwizi kati yake na kuingia Jahannam (motoni) isipokuwa kufikiwa na kifo, endapo atakuwa ametenda matendo ya watu wa Jahannam, hivyo basi hapana kitu baada ya maisha haya isipokuwa maisha ya akhera na maisha hayo - mtu atakuwa - ama mwenye kuneemeka au shaqii (mwenye kuwa katika mashaka).

7. lengo hilo ni ajali, na lapunguzwa mpaka muda wa kumalizikia huko, hivyo kiasi cha muda mdogo upitao ni upungufu kwa ule muda kati yetu na muda wa ajali, na saa inabomoa pembe moja kutoka huo muda, na ambalo huwa hivyo bila shaka muda wake ni mfupi.

8.Jiandalieni duniani kutoka duniani: ni maneno fasaha: kwa sababu ambacho anaweza kujikidhi nacho muqalaf nafsi yake akhera kwa kweli anakichuma duniani, nacho ni taqwa, ikhlas na imani.

Hivyo basi jiandalieni masurufu duniani kutoka duniani,8 kwa ambayo mtazihifadhi nafsi zenu kesho, kwa hiyo mja akimcha Mola wake Mlezi atakuwa ameinasihi nafsi yake, na atakuwa ameitanguliza toba yake, na atakuwa ameyashinda matamanio yake, kwa kuwa kifo chake kimefichwa, na matumaini yake yanamhadaa, na Shetani amefanywa kwake wakala, yuampambia maasi ili ayatende, na yuamshawishi kuchelewesha toba kwa kujifanya nitatubu baadae, kifo kitakapomhujumu kitamsahaulisha aliyonayo.

Lo! Hasara iliyoje kwa mwenye kughafilika ambaye umri wake utakuwa hoja dhidi yake, na siku zake zimfikishe kwenye maafa! Tunamuomba Mungu (s.w.t) atujaalie na ninyi tuwe miongoni mwa ambao neema hai- wafanyi wajivune wala lengo haliwafanyi wazembee kumtii Mola Wao, wala baada ya umauti hafikwi na majuto wala huzuni.”.

# NAHJUL BALAGHA

## JUZUU YA PILI

### MTARJUMI: HARUNA PINGILI

## 65 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Khutba Zake (a.s) - Ameitaja hotuba hii as-Saduq katika at-Tawhiid, uk. 19 na 62. Na al-Aamidiy katika Ghurarul-Hikami, uk. 238.

### KATIKA KUMTAKASA MWENYEZI MUNGU (S.W.T)

"Himidi ni za Mwenyezi Mungu ambaye hali (Yake) haikutanguliwa na hali[1]. Kwa hiyo anakuwa wa kwanza kabla hajawa wa mwisho na anakuwa wa dhahiri[2], kabla hajawa baatin[3]; kila chenye kuitwa moja kisichokuwa yeye ni kichache[4], na kila mtukufu asiyekuwa Yeye ni dhalili[5]. Na kila mwenye nguvu asiyekuwa yeye ni dhaifu, na kila mfalme asiyekuwa Yeye ni mmilikiwa, na kila mjuzi asiyekuwa Yeye ni mwanafunzi[6], na kila muweza

---

1. Sifa yoyote ambayo Mungu anayo huwa ni sifa ya dhati Yake (miongoni mwa sifa zijulikanazo kuwa ni sifa athubutia al'kamalia), zinakuwa wajibu kama ilivyo wajibu dhati Yake, hivyo basi kama ilivyo dhati yake (s.w.t) haisogelewi na hali ya kubadilika na kugeuka, hali ni hiyo hiyo kuhusu sifa Zake, ziko thabiti pamoja Naye, hapana sifa yaitangulia sifa nyingine, japo kufahamika kwake zaweza kutambulika kama moja imekuja baada ya nyingine, endapo itaambatanishwa na asiye kuwa Yeye, kwa kuwa Yeye ni wa mwanzo na wa mwisho. Azaliy - yaani isemwapo: wa mwanzo na wa mwisho sio maana yake Mungu (s.w.t) alianza wakati fulani kuwepo bali mwanzo wa kila kiumbe waanzia Kwake na mwisho wake ni Kwake, Yeye (s.w.t) hana mwanzo wala mwisho.

2. Wa kwanza: yaani hajakosa kuwapo, wala chochote hakijawa aslan; na wa mwisho, yaani yeye ni mwenye kubaki hakomi kuwapo, na vitu vyote vitakosekana kabisa.Na yawezekana awe yu akusudia (a.s) kuwa Yeye (s.w.t) haifai awe mahali pa sifa zinazokuja moja baada ya nyingine.

3. Wa dhahiri: kwa maana ya dalili na uthibitisho kumuhusu uko wazi,na baatini: Ni asiyeweza kutambulika kupitia hisia tano za fahamu bali hutambulika kwa akili. Na pia yawezekana kutafsirika adhwahiru kwa maana ya mshindi, na al-baatinu kwa maana ya Al'aalimu mjuzi.

4.(Viitwavyo kimoja ni vichache) Kwa kuwa moja ni idadi ndogo mno, na maana ya Yeye kuwa mmoja yabainisha mbali na hilo, kwa sababu maana ya kuwa Yeye ni mmoja ama kukanusha kuwapo wa pili katika uungu, au kuwapo Kwake ni muhali agawanyike, na kwa mujibu wa tafsiri hizi mbili uungu waepushwa mbali na mafuhumu ya uchache. Na pia yawezekana ikasemwa kuwa aliye mmoja pekee hana mshirika, asiyekuwa na msaidizi hudharauliwa kwa unyonge wake, yu duni kwa kukosa wa kumsaidia. Ama umoja katika upande wa Mungu ni utukufu wa dhati kwa kukosa muungano unaoishiria lazima ya kuchanguka, na kuwa pekee Kwake kwa utukufu na mamlaka na kutoweka kwa kila dhati isipokuwa yenyewe (yaani ya Mungu (s.w.t) endapo itazingatiwa hainasibiani, hivyo basi asiyekuwa Mungu kusifika na upweke ni kumfanya kuwa mdogo, hali ya kuwa ukamilifu katika ulimwengu wake ni kuwa awe wengi, isipokuwa Mungu kwani kumsifu kwa upweke ni kumtakasa na kumuepusha.

5. Na kila mtukufu asiyekuwa Yeye ni dhalili; kwa sababu yu katika mashiko ya qadhaa na qadara.

6. Kwa sababu Yeye (s.w.t) ndiye anayegawa ilimu, hivyo Yeye ni mwalimu wa kwanza.

asiyekuwa Yeye ni mwenye kuweza na kushindwa[1]. Na kila msikiaji asiyekuwa Yeye hasikii sauti iliyo dhaifu mno[2].

Na kubwa zamfanya kiziwi, na za mbali humpita, na kila muonaji asiyekuwa Yeye haoni rangi hafifu na miili nyeti, na kila kilicho dhahiri kisichokuwa Yeye ni baatin, na kila batini kisichokuwa yeye si baatini[3]. Hakuumba alivyoviumba ili kuimarisha mamlaka wala kuhofia matukio magumu ya zama, wala kujisaidia dhidi ya anayelingana naye mwenye kuhujumu, wala mshirika mwenye kujigamba kwa wingi, wala mpinzani mwenye kujiona kuwa yuko zaidi, lakini ni viumbe wenye kumilikiwa, waja walio dhalili. Hawi kwenye vitu: hata isemwe kuwa Yeye yu ndani yake, hajawa mbali navyo kiasi cha kusemwa:

Yumbali navyo[4]. Hakuchoshwa na kuumba alivyovibuni[5],wala kuviratibu alivyoumba, haikumtokea kushindwa na alivyoviumba, wala hakuingiwa na mkanganyiko kuhusiana na aliyoyahukumu na kuyafanyia makadirio[6],12 bali ni hukumu iliyofanywa kwa umakini, na ilimu iliyo madhubuti, na ni jambo lililobidi, mwenye kutumainiwa pamoja na kuwa yu anaadhibu, mwenye kuogopwa japokuwa ni mwenye kuneemesha."

## 66 - NA MIONGONI MWA MANENO YAKE [(A.S)]

Na Miongoni Mwa Maneno Yake [(a.s)] - Al-Bayhaqi ameyaeleza maneno haya katika kitabu al-Mahasin, uk. 45, na Ibn Asakir katika Ta'rikh Damishqi, na Ibn Qutaiba katika Uyunul-Akhbar, 1: 110.

---

1. Kwa kuwa Mungu ni muweza dhati yake, na asiye kuwa Mungu huwa muweza kwa jambo nje ya dhati yake.

2. Uziwi: ni kuharibika kwa ala ya kusikia, na ibara "kila asikiaye asiyekuwa Yeye huwa kiziwi" ni kwa sababu msikiaji ambaye si Mungu husikia kwa njia ya ala ya kimwili, ambayo huwa na nguvu yenye kikomo, na Muumba (s.w.t) yu kinyume na hali hiyo, na hivyo hivyo kuhusu kauli yake "na kila mwenye kuona asiyekuwa yeye huwa kipofu" hivyo basi wanaosikia miongoni mwa wanyama na wanadamu nguvu ya usikivu wao ina mpaka uliowekwa, kwa hiyo sauti zilizo hafifu usikivu wao hauzifikii, kwa hiyo ni viziwi kwenye sauti hizo. Na zilizo kubwa miongoni mwa sauti zitokazo nje ya hali ya kawaida haziwezi kuvumilika, uziwi hutokea kwa kuraruriwa nazo, na zilizo mbali miongoni mwa sauti katika hali ya kwamba mawimbi ya hewa yanayozichukua sauti hizo hayafiki, yote hayo kwa asiyekuwa Yeye swt, ama yeye mtukufu kwake inakuwa sawa sauti ndogo na kubwa, ya karibu na ya mbali; kwa sababu mnasaba wa vitu Kwake ni mmoja, na mfano kama huo husemwa katika kuona na vionavyo.

3. Hapa baatin ina maanisha: Sio yeye kwa mifano iliyotangulia, yaani kila kilicho dhahiri kwa kuwepo kwake kulikotolewa na Mungu (s.w.t) huko ni baatin dhati yake, yaani kuwapo kwake sio kwa yeye mwenyewe binafsi, kwa hiyo yeye kiukweli hayupo, na kila baatin mbali na yeye ni kwa maana hii,wala haiwezekani awe dhahiri mwenyewe kwa dhati yake, bali yeye ni baatin daima.

4. Yaani, hajatengana navyo mtengano wa kimwili hata isemwe yu mbali navyo.

5."Hakuchoshwa na kuumba alivyovibuni" mpaka kauli yake: "alivyoumba" ni kwa sababu Mungu (s.w.t) ni muweza kwa dhati Yake, hivyo basi hachoki wala hashindwi; kwa kuwa yeye sio mwili; wala sio yuaweza kwa uwezo wenye mpaka.

6. Ni kwa sababu Yeye (s.w.t) ni mjuzi dhati yake; ni muhali aingiwe na shub'ha, (yaani utata).

## AWAAMBIA SAHABA ZAKE KATIKA BAADHI YA SIKU ZA SIFFIIN

"Enyi Waislamu! Ifanyeni hofu ya ucha Mungu iwe kuwa ndio nguo yenu ya ndani, na ufanyeni utulivu kuwa joho lenu. Umeni meno, kwani kufanya hivyo hudugisha mno panga kwenye fuvu la kichwa.

Kamilisheni kuvaa ngao, zitikiseni panga ndani ya ala zake kabla ya kuzichomoa, mwangalieni adui kwa kijichopembe cha ghadhabu, pigeni kwa panga zenu pande zote, kushoto kulia, pambaneni kwa panga, juweni kuwa mpo mbele ya macho ya Mungu, na mpo pamoja na mwana wa ammi yake Mtume wa Mungu, jizoesheni kurejea tena na tena, kwenye mapambano, oneni haya kukimbia[1]; hiyo ni aibu kwa vizazi vijavyo[2], na ni moto siku ya hesabu.

Yatoeni maisha yenu (kwa Mungu) kwa hiyari, na yaendeeni mauti mwendo wa rahisi, jihadharini na kundi hili kubwa[3], na hema lililofungwa kwa kamba, pigeni katikati yake, kwa kweli Shetani amejificha pembeni mwake, ameunyosha mkono wake tayari kwa kushambulia, na kuubakisha nyuma mguu kwa kukimbia.

Bakieni thabiti katika kusudi lenu! Mpaka ikudhihirikieni nguzo ya ukweli; "Ninyi ndio washindi, na Mungu yu pamwe na ninyi, wala hatopunguza (thawabu za amali zenu).[4]".

## 67 - NA MIONGONI MWA SEMI ZAKE (A.S)

Na miongoni mwa semi zake (a.s) - Ameieleza An-Nuweiry mwanzo wake katika kitabu Nihayatul-Irbi, Jz. 8, uk. 168.

Wamesema: Na zilipomfika Amirul-Mu'minin habari za Saqiifah[5], baada ya kutawafu Mtume **(s.a.w.w)** alisema Ali (a.s):

"Wamesema nini Ansar?" Wakasema: Wamesema: Sisi tuwe na amiri na ninyi muwe na amiri; akasema (a.s): "Je hamkuhoji dhidi yao kuwa Mtume ameusia atendewe mema aliye mwema miongoni mwao na asame- hewe muovu wao!?"

Wakasema: Katika hili hakuna hoja yoyote dhidi yao? Akasema (a.s): "Lau uimamu ungekuwa katika wao, wasingeusiwa." Kisha akasema (a.s): "Basi nini walisema maquraishi?" Wakasema: Wametoa hoja kuwa wao ni mti wa

---

1. Kwa kuwa kukimbia vitani ni dhambi kubwa.

2. Yaani katika watoto, kwa sababu wao wataaibishwa kwa kukimbia mababa.

3. Kundi hili kubwa: anawakusudia watu wa Sham(Syria).

4. Maneno haya Amirul-Mu'minin (a.s) aliyahutubia siku ambayo jioni ya usiku wa al-Harir katika riwaya nyingi, na katika riwaya ya Nasir bin Muzahim kuwa alihutubia siku ya kwanza ya mapambano katika vita vya Siffin, na hiyo ilikuwa katika mwezi wa Safar, mwaka wa 37 Hijiria.

5. Saqifa Bani Sa'idah masahaba walijikusanya humo baada ya kutawafu Nabii (s.a.w.w), ili kumchagua khalifa wake.

Mtume **(s.a.w.w)**. Akasema (a.s): "Wameutolea hoja mti na wamelipoteza tunda.[1]"

### 68 - NA MIONGONI MWA MANENO YAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Maneno Yake (a.s) - * Tabariy ameieleza khutba hii ndani ya matukio ya mwaka wa 36, na Al'Baladhuuriy ndani ya Ansabul-Ashrafi, uk. 404, chapa ya Al'aalamiy. Alipomteua Muhammad bin Abi Bakr kuwa Gavana wa Misri, alizidiwa na kuuliwa:[2]

"Nilitaka kumtawaza Hashim bin Utba huko Misri[3]; lau ningemtawaza yeye Misri pasingebakia eneo, na wasingepata fursa, bila ya kumlaumu Muhammad bin Abi Bakr, kwa kweli alikuwa mpenzi kwangu na kwangu alikuwa (rabiiba)." * Rabiiba - mtoto wa kamsbo.

### 69 - NA MIONGONI MWA MANENO YAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Maneno Yake (a.s) - Al-Baladhuriy ameieleza hii katika Ansabul-Ashraf, uk. 438 katika tarjuma ya Ali (a.s).

### KUWALAUMU SAHABA ZAKE

"Kwa kadiri gani niwatendee kwa upole kama atendewavyo ndama wa ngamia aliyeraruka nundu yake kwa ndani, na nguo iliyochoka, kila ishonwapo upande mmoja wararuka upande wa pili, na wanapokupitieni askari wa Sham, kila mmoja wenu huufunga mlango wake, na hutokomea utokomeaji wa guruguru shimoni mwake, na fisi ndani ya tundu lake.

Wallahi dhalili ni yule mliyemnusuru! Na mwenye kutupa mshale kwa msaada wenu ni sawa na atupae mshale uliovunjika pande zote mbili. Ninyi mnakuwa wengi kwenye kumbi za nyumba, na mnakuwa wachache chini ya bendera.

Mimi najua kinachoweza kuwarekibisha, na kunyoosha kupindama kwenu, lakini mimi Wallahi sitowarekebisha kwa kujiharibu binafsi. Mungu azidhalilishe nyuso zenu, na aangamize hadhi zenu, hamuujui ukweli kama muijuavyo batili, wala hamuibatilishi batili kama mubatilishavyo ukweli."

---

1. Tunda anawakusudia Ahlil-Bayt Rasuul (s.a.w.w).

2. Muhammad bin Abi Bakr: Mama yake ni Asma bint Umays bin An-Nu'man, alikuwa chini ya Ja'far bin Abi Talib, na katika hij'ra ya kwanza alihama na Ja'far mpaka Uhabeshi. Huko alimzalia Abdullah bin Ja'far Al-Jawadi, baada ya hivyo (Ja'far) aliuawa katika siku ya Mu'uta. Alichukuliwa na Abu Bakr, akamzalia Muhammad, kisha (Abubakar) alikufa na kumwacha Asma akiwa hai, baadae alichukuliwa na Ali bin Abi Talibi ndipo Muhammad alipokuwa mtoto wake wakulea, na alikuwa akimchukulia kama mwanawe. Alinyonya upendo na ufuasi toka zama za utoto, kwa hiyo alikulia kwake, ilikuwa hajulikani baba yake ila Ali (a.s) kiasi kwamba Ali alisema: Muhammad ni mwanangu kutoka mgongo wa Abu Bakar.

3. Hashim bin Utba bin Abi Waqqaas, ami yake ni Sa'ad bin Abi Waqqaas, na baba yake ni Utba bin Abii Waqqaas, ndiye ambaye alivunja jino la Mtume (s.a.w.w) siku ya Uhud, na Hashim ndiyo Al-Mirqalu: Ameitwa Al-Mirqalu kwa kuwa alikuwa anaharakia katika vita, naye ni miongoni mwa Mashi'a wa Ali.

# NAHJUL BALAGHA

## JUZUU YA PILI

### MTARJUMI: HARUNA PINGILI

## 70 - NA AMESEMA [(A.S)]

Na Amesema [(a.s)]- Ibn Sa'ad ameielezea ndani ya at-Tabaqat, Jz. 3, uk. 36, na Al'Qaaliy ndani ya Dhaylul'amali uk. 190, na Al'Isfahani ndani ya Maqatilu Talibiin uk.16, na Ibn Abdi Rabih ndani ya Al-Iqdul al-Farid Jz. 2, uk. 298, na wengine.

### KATIKA MKESHA WA SIKU ALIYOSHAMBULIWA

"Nilipatwa na usingizi nikiwa nimekaa nikamuona Mtume wa Mungu **(s.a.w.w)**, nilimuuliza: 'Ewe Mtume wa Mungu! Kupindama kulikoje na uadui ambao nimekabiliana navyo kutoka kwa umma wako!' Akasema: 'Wapatilize,' Nikasema: 'Mungu anibadilishie walio bora kuliko wao, na anibadilishe na aliye mbaya zaidi kwao kuliko mimi.[1]"

Amesema Ar-Radhiy (r.a): Anakusudia kwa neno kupindama, na kwa neno mzozo, na huu ni ufasaha wa hali ya juu mno wa maneno.

## 71 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE [(A.S)]

Na Miongoni Mwa Khutba Zake [(a.s)] - Al-Mufid ameielezea katika al-Irshad uk. 61, na ibn Da'abiy katika al-Ikhtiswas uk. 155, na Tabrasiy katika al-Ihtijaj Juz.1, uk. 254.

### KATIKA KUWALAUMU WA-IRAQI:

"Ama baada! Enyi watu wa Iraqi, mko kama mwanamke mwenye mimba, ameshika mimba na alipotimiza upevu wa mimba akaporomosha mimba, na mumewe akafariki, kwa hiyo muda wake wa ujane ukawa mrefu, na akarithiwa na wa mbali kabisa[2]. Wallahi sijakujieni kwa hiyari; isipokuwa nilikujieni katika hali ya kusukumwa[3].

---

1. Sharran: Shari hapa haijulishi kwamba ndani yake kuna shari, ni kama kauli yake swt: "Qul adhalika khairun am janatul-khuldi." (Swafat) haijulishi kuwa ndani ya moto kuna heri.

2. Anakusudia kuwa wao walipoona kuwa watu wa Sham wanakaribia kuangamizwa, na kujitokeza alama za kuwashinda, walielemea kwenye (wazo la suluhu) mapatano ya kusimamisha vita, ili kuwaitikia walioomba kufanya tah'kiimu, hivyo basi mfano wao ukawa sawa na mwanamke mwenye mimba, alipotimiza miezi ya mimba yake, akamporomosha mwanawe bila ya kutokea sababu ya kimaumbile, bali kwa sababu tu ya tukio lililojitokeza, kama kipigo na kuanguka, na halifanyi hilo ila ataangamia. Na wala hakutosheka katika kuifanyia mfano hofu yao katika hilo, bali alifikia kusema: 'Na akafa mumewe akiwa katika hali hii, na udhalili wake ulichukua muda mrefu, kwa sababu ya kumkosa kwake wa kumsimamia, mpaka akifa bila ya mtoto, watamrithi wa mbali walio duni katika daraja kinasaba, miongoni mwa ambao nasaba yake haitiliwi manani.'

3. Anaapa kuwa yeye hakuja Iraqi akiwaomba nusra watu wake kwa hiyari kwa kuwaboresha wao juu ya wengine, isipokuwa alisukumwa kwao na msukumo wa dharura, kwani lau si tukio la Jamal (ngamia) asingefarikiana na Madinatul'Munawarah. Na maneno haya pia huelezwa kwa njia nyingine, nayo: Sikuja kwenu kwa hiyari, wala sikuja kwenu kwa shauku na ninyi.

Nimepata habari kuwa ninyi mwasema: 'Ali anasema uwongo, Mungu (swt) akuangamizeni! Nani nimsemee uwongo? Nimuongopee Mungu? Mimi ni wa kwanza kumwamini! Au nimsemee uwongo nabii wake? Mimi ni wa kwanza kumsadiki yeye!
Hapana wallahi, lakini hiyo ni ibara ambayo mmeshindwa kuitambua maana yake[1], hamkuwa wenye kustahiki nayo, Waylumah, ninakupimieni vipimo vya kiilimu na hikma, upimaji usio na thamani[2],4 lau angekuwa na chombo apime humo." "Na bila shaka mtajuwa habari zake baada ya muda," (38:88).

## 72 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Khutba Zake (a.s) - Ameieleza ibn Qutayba katika Gharibul-Hadith, na Thaqafi katika al-Gharatu, na al- Qadhy al-Qadhwaiy katika as-Sahifatul-Alawiyah, uk. 3.

### ALIWAELIMISHA WATU NAMNA YA KUMSALIA MTUME WA MUNGU

"Ewe Mola Wangu! mkunjuaji wa yakunjuliwayo na mhifadhi wa yahifadhiwayo, na muumba wa nyoyo katika maumbile yake ya asili, zenye taabu na mashaka na zenye maisha ya furaha, zijaalie sala zako za ziada na baraka zako zenye kuendelea juu ya Muhammad, mja wako na mjumbe wako, mhitimishaji wa yaliotangulia katika unabii[3], na mfunguzi wa yaliojifunga[4] na mtangazaji wa haki kwa haki na mzuiaji wa mfuriko wa batili[5] na mvunjaji wa ukali wa upotovu[6] kama alivyobebeshwa akasimama kwa nguvu, akitekeleza amri Yako, mwenye kuharakia katika ridhaa Zako, si goigoi kwenda vitani, wala si dhaifu katika azimio, mwenye kufahamu wahyi Wako, mhifadhi wa wahyi Wako, mhifadhi wa amri Zako na mwenye kuzitekeleza,

---

1. Lahaja: Ni kiungo cha mwili cha kutamkia, husemwa: ana lahaja fasaha. Na inawezekana anakusudia hapa lahaja ya Rasuli (s.a.w.w), na inawezekana anaikusudia lahaja yake yeye mwenyewe; anasema kwamba hiyo ni lahaja ambayo mko mbali na man- ufaa yake, yaani aina ya maneno ambayo ninyi mko mbali na maana yake, hivyo hamyafahamu, kwa ajili hiyo ndio mnayakadhibisha.

2. Neno: husemwa kuonesha kustaajabishwa na kutukuza; huandikwa lime- unganishwa na asili yake: na mradi wao ni kuadhimisha, hivyo basi lasemwa mahali pa kusifu japokuwa asili ya madhumuni yake ni kinyume chake. Na mifano kama hiyo ni maarufu katika lugha yao (watu wa Basra) kwani wao humwambia mtu wanayemheshimu na kumtukuza: na Hasan Al'Basriy alisema hali yu amtaja Ali (a.s) akimueleza kuwa yeye yuko na haki katika mambo yake yote: lau ningepata chombo nipime humo, yaani lau ningezipata nyoyo zenye kupokea na akili tambuzi.

3. Yaani unabii uliotangulia.

4. Mfunguaji wa yaliyojifunga: Milango ya nyoyo ilikuwa imefungwa kwa matendo ya upotovu zikiwa mbali na mwongozo, naye (s.a.w.w) akazifungua kwa aya za unabii, na akatangaza ukweli na kuudhihirisha kwa haki na uthibitisho.

5. Alitangaza haki kwa haki na kuidhibiti batili na kuushinda upotovu kama ambavyo amezibeba kazi hizo tukufu kwa kubeba uzito wa risala. Mwenye kuzituliza batili zilizo jitokeza.

6. Mvunjaji wa ukali wa upotovu na nguvu zake, hivyo yafanyika kwa kuangaza dalili na kudhihiri kwa hoja.

mpaka kupatikana haki, na akaiangaza njia kwa ababaikaye, na nyoyo zikaongozwa baada ya kuingia fitna na dhambi. Na alitekeleza dalili wazi za njia, na hukumu zenye nuru.

Hivyo yeye ni muaminifu Kwako mwenye kuaminiwa, na mhifadhi wa ilimu Yako iliyo mahsusi, na shahidi Wako Siku ya Hukumu[1].

Yeye ni mtumishi Wako wa kweli, na Mtume wako kwa viumbe. Oh, Ewe Mola Wangu! Mpanulie nafasi katika kivuli chako[2], na umlipe kheri ya ziada katika fadhila Zako. Umnyanyulie daraja jengo lake[3], na ikirimu daraja yake Kwako[4], mtimizie nuru yake, mlipe akutakalo ushahidi unaokubalika, na usemi unaoridhiwa, muadilifu wa mantiki, na hutba pambanuzi.

Oh Ewe Mola wangu! Kusanya kati yetu na yeye tuwe katika maisha baridi na neema tulivu ya kudumu[5], na kutosheka na yatakiwayo, na ladha ya utashi, maisha ya raha, utulivu wa akili, na tunu za heshima.[6]".

## 73 - NA MIONGONI MWA MANENO YAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Maneno Yake (a.s) - Ibn Sa'ad ameieleza sehemu ya maneno haya katika Tabaqat, Jz. 1, na al-Baladhuliy kati- ka al-Ansab, uk. 361.

### ALIMWAMBIA MARWAN BIN AL-HAKAM HUKO BASRA

"Walisema: Marwan bin Al-Hakamu alitekwa siku ya Jamal na aliwasihi Hasan na Husain wamuombee kwa Amirul-Mu'minina (a.s). Nao walisema naye kuhusu suala lake, naye (Amirul'Mu'minina) alimwacha huru.

---

1. Shahidi Wako kwa watu kama alivyosema (s.w.t): "Basi itakuwaje pindi tukiwaletea kutoka kila umma shahidi, na tukakutetea wewe kuwa shahidi wa hawa" ( 4:41).

2. Kivuli chako: Yawezekana ikawa majazi, kama wasemavo: "kivuli cha fulani kimenienea", yaani hisani yake, hapo kivuli kimetumika majazi ikikusudiwa hisani. Na yawezekana ikakusudiwa maana yake halisi, ikikusudiwa kivuli kilichotajwa na Mungu (s.w.t), aliposema: "Na kivuli kilichotanda, na maji yanayomiminika" (56:30-31).

3. Yaani ifanye daraja yake katika ulimwengu wa thawabu kuwa ni ya juu zaidi, au iwe akusudia jengo lake, lile alilojenga (s.a.w.w) kwa amri ya Mola Wake miongoni mwa sheria ya kiadilifu na mwongozo ulio bora ambao wanaobabaika warejea humo, na humo wana kimbilia wanaokandamizwa, na imam yu amuomba Mungu aliinue jengo la sharia zake juu ya shera zote, na ainue hali ya uwongozi wake juu kuliko uongozi wa yeyote mwingine.

4. Kuipa heshima daraja: ni kuikamilishia nuru: Yaani kuipa nguvu dini ili iwaenee wakazi wa ardhini, na ipate ushindi juu ya dini zote kama Mungu alivyomuahidi. Na kuikamilisha daraja akhera, imetangulia katika usemi wake.

5. Waarabu husema: "Aishun baaridun" - Maisha baridi: yaani yasiyo na vita wala mzozo, kwa sababu baridi na utulivu vinalazimiana ulizimiano wa joto na harakati. Na wakararu ni'ima: Kutuama kwa neema kwa namna ambayo inadumu wala haiishi.

6. Tunu: Ni anachokirimiwa mtu miongoni mwa wema na upole, na alikuwa (s.a.w.w.) ni miongoni mwa wenye raha sana katika watu kiakili, na mwenye kujiambatanisha mno na utulivu, na alikuwa wa daraja la juu sana kiroho, hivyo basi Imam alikuwa anamuomba Mungu amsogeze karibu naye katika sifa hizi zote za heshima. Anaomba amuwafikishe kuwa pamwe na Nabii (s.a.w.w.) katika ayapendayo na ayaelemeayo.

Walimwambia (wasemaji ni Hasan na Huseni): Akuba'i ewe Amirul-Mu'minina.Akasema (a.s):

"Kwani hakunifanyia bai'a baada ya kuuliwa Uthman? Sina haja ya bai'a yake! Kwa kuwa huo ni mkono wa kiyahudi[1], lau anifanyie bai'a kwa mkono wake angenisaliti kwa tako lake[2]. Ila tu yeye Marwan atakuwa na uamiri wa muda mfupi kama vile mbwa anavyoramba pua yake[3]. Na yeye ni baba wa maraisi wanne wa kaumu[4].

Umma utapata siku nyekundu kutoka kwake na kwa wanawe.[5]".

## 74 - NA KATIKA USEMI WAKE (A.S)

### WALIPOAZIMIA KUMFANYIA BAI'A UTHMAN

"Kwa kweli mnajua kuwa mimi ni mwenye haki nao (ukhalifa) zaidi kuliko mwingine yeyote asiye kuwa mimi; na wallahi nitamwachia (Uthman) maadamu kumwachia mambo ya waislamu yatakuwa katika amani na dhulma haitokuwa isipokuwa kwangu tu[6], nikitaraji ujira wa hilo na fadhila zake, na kujiweka mbali na mnachoshindania na kujiweka kando na kuyafikia mapambo yake ambayo mnagombania."

## 75 - NA MIONGONI MWA SEMI ZAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Semi Zake (a.s) - Ibn al-Athir ameieleza katika an-Nihayah katika mada ya Qirzu.

### ALIPOPATA HABARI KUWA BANI UMAYYAH WANAMTUHUMU KUSHIRIKI DAMU YA UTHMAN

---

1. Mkono wa kiyahudi yaani: wakisaliti wenye vitimbi, na uyahudi hunasibishwa na vitimbi na udanganyifu.

2. Tako ni kitu mtu huwa na pupa ya kukisitiri, na amelitumia hapo likiwa jina mbadala la vitimbi vya chini kwa chini, na amelichagua kwa ajili ya kumdunisha mwanavitimbi.

3. Uamiri: Ni utawala, na usemi wake: 'kama mbwa anavyoramba pua yake' anakusudia muda wa utawala wake utakuwa mfupi, na ndivyo ulivyokuwa muda wa ukhalifa wa Marwani, kwa kuwa alitawala miezi tisa. Na riwaya husika ya Amirul-Mu'minin kuhusu Marwan: "atabeba bendera ya upotovu baada ya panja zake mbili kuwa na mvi". Kwa kuwa yeye alishika uongozi wa ukhalifa akiwa na miaka 56 katika riwaya ya wastani.

4. Al-Akbush: ni wingi wa Kabshu, nayo katika kaumu ya watu ni raisi wao. Na wamefasiri al-Akbushu kuwa ni Abdul-Malik bin Marwan huyu, nao ni al-Walid, Sulayman, Yazid na Hisham. Na wamesema: Hawakuutawalia ukhalifa ndugu wanne isipokuwa hawa. Na inajuzu iwe wamekusudiwa wana wa Marwan mwenyewe, nao ni Abdul-Malik, Abdul-Aziz, Bashar na Muhammad, na walikuwa kundi shujaa: Ama Abdul-Malik alitawalia ukhalifa, na Muhammad alitawala Jaziira, na Abdul-Aziz Misri, na Bashar Iraqi. Na tafsiri hii ni bora; kwa sababu al-Walid na ndugu zake ni watoto wa mwanawe, na hao ni watoto wa mgongo wake.

5. Siku nyekundu: Ni siku ya shida, waarabu husema mwaka wa ukame mwaka mwekundu.

6. Anaapa Mungu kuwa atakabidhi suala la ukhalifa kwa Uthmani, madamu kuukabidhi hakuwadhuru waislamu, na kutawahifadhi na mateso, akitaka thawabu yake (swt) kwa hilo. na kufanya zuhudi kuacha Uamiri ambao wameshindania japo katika hilo anadhulumiwa yeye hasa.

“Je Bani Umayyah kunijua kwao hakujawazuia kuniaibisha? Je kutangulia kwangu (kuukubali uislamu) hakujawaweka mbali wajinga na kunituhumu? Kwa kweli aliyowaonya Mungu amewaonya kwa ufasaha zaidi kuliko ulimi wangu, mimi ni mtoa hoja dhidi ya watokao nje ya dini, na ni hasimu wa wavunjao ahadi na wenye shaka[1], na kwenye Kitabu cha Mungu.

Kwa Kitabu cha Mungu hupimwa yasiyo wazi[2]. Kulingana na yaliyo mioyoni waja watalipwa.” Anaikusudia kauli yake (s.w.t) “Hadhani khasmani ikh’taswamu fii Rabbihim” (22:19).

# NAHJUL BALAGHA

## JUZUU YA PILI

### MTARJUMI: HARUNA PINGILI

## 76 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Khutba Zake (a.s) - Ameyaeleza hayo al-Haraniy katika at-Tuhaf, uk. 150, na ibn Shakir katika Uyunul- Hikami wal mawa’idh, na Zamakhshari katika Rabiul-Abrar Jz. 1, uk. 231, na al-Hisriy katika Zuhurul-Adabi, Jz. 1, uk. 42.

### KUHUSU ZUHUDI

“Mungu amrehemu mtu aliyeisikia hukumu akaihifadhi na kuielewa, na aitwapo kwenye mwongozo akausogelea[3], na amfuata kiongozi (kwa kushika mkanda wake wa kiunoni) na akaokoka, akajihadhari na Mola wake Mlezi, na kuhofia dhambi zake, akatanguliza ikhlas na kutenda mema, akachuma na kupata hazina, na akajiepusha na yaliyohadharishwa. Na akalenga lengo, na kufanikiwa kupata kitu mbadala, akaukabili utashi wake, na kuyakadhibisha matumaini yake (bandia), na akaifanya subira kuwa ndio njia yake ya uwokovu, na taqwa kuwa ndio masurufu ya kifo chake. Akapita njia ya haki, kwa mwenendo wa kiadilifu, na akijiambatanisha na njia ya hali ya juu ya ukweli, na kuutumia vyema wakati wake, na kuuharakia mwisho (wake), na akaenda na akiba ya matendo mema.”.

## 77- NA MIONGONI MWA SEMI ZAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Semi Zake (a.s) - Al’Isfahaniy ameielzea usemi huu ndani ya ‘Al-Aghaaniy’ Juz. 11, uk. 29, na Al-Azhariy ndani ya ‘Tah’dhiibi-lughah’ Juz. 15, uk. 27.

---

1. Anakusudia Siku ya Kiyama, imeelezwa kutokana naye (a.s) usemi: “Anaa awwalu man yaj’thu lilhukuumati bayna yaday llahi taala” - Mimi ni wa kwanza miongoni mwa watakaopiga magoti mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

2. Aikusudia kauli yake (s.w.t): “Hawa wagomvi wawili waliogombana kwa ajili ya Mola wao Mlezi” (22:19), hivyo basi mambo yanayotatanisha hupimwa na Qur’ani, linaloafikiana nayo ndio haki kisharia, na litakalokwenda kinyume nayo ndio batili linakatazwa kisharia. Na yeye, Karrama-llahu waj’hahu amekwenda kwa mujibu wa hukumu ya Kitabu cha Mungu (swt) katika matendo yake, hana haki mwenye kukifumbia macho amnyooshee kidole cha kebehi hali yeye (a.s) akiwa yu ajiambatanisha na hukumu ya Kitabu.

3. Hukumu hapa: Ni hekima, Mungu (s.w.t) amesema: “Nasi tulimpa hekima angali mtoto;” (19:12).

### KUWAHUSU BANI UMAYYAH

"Kwa kweli Bani Umayyah wananiruhusu kiasi kidogo cha mirathi ya Muhammad **(s.a.w.w)**. Wallahi endapo nitabaki nitawapuliza mpulizo wa muuza nyama apulizapo mnofu wa nyama ulioenea mchanga!"

**Maelezo**

Ar-Radhiy (r.a) amesema: Na yaelezwa kwa tamko nayo iko katika hali ya kugeuza, kwa sababu ukweli ni kama ilivyokuwa katika riwaya ya kwanza, sio kwa kuwa hilo halina maana, kwa hiyo hii yakusudiwa riwaya iliyogeuzwa.

Na kauli yake (a.s) (Layufawiqunaniy) yaani wananipa kutoka mali ya (Muhammad) kitu kidogo sawa na mkamo mmoja wa maziwa ya ngamia. Na wid-hamu at-taribatu: ni udongo, ni wingi wa neno wadhamatu, nacho ni kipande cha tumbo au cha ini kilichoanguka na kutapakaa vumbi hupulizwa.

## 78 - NA MIONGONI MWA SEMI ZAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Semi Zake (a.s) - Al-Jaahidhwu ameueleza mwisho wa du'a hii katika al-Miatu al-Mukhtaratu.

### ALIKUWA AKIOMBA KWA DUA HII:

"Ewe Mungu wangu! Nisamehe ambayo wewe wayajua zaidi kuliko mimi, endapo nitarudia nirejelee kwa msamaha. Ewe Mungu Wangu! Nisamehe kwa niliyoyaahidi nafsini mwangu, na wala hukuuona utekelezaji wake kwangu[1].

Ewe Mungu Wangu! nisamehe niliyojikurubisha nayo kwako kwa ulimi wangu, halafu moyo wangu ukawa kinyume nayo[2]. Ewe Mungu Wangu! nisamehe na mikonyezo, na maneno ya ovyo, na usahaulifu wa moyo na mtelezo wa ulimi."

## 79 - NA MIONGONI MWA MANENO YAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Maneno Yake (a.s) - Ibrahim ibn Hasan ibn Dizili ameieleza katika kitabu Swiffiin, na Saduq katika kitabu Uyunul-Akhbar ar-Ridha, Jz. uk. 138.

Aliwaambia baadhi ya sahaba zake alipokuwa ameazimia kufanya msafara kukabiliana na Khawarij. Na (mmoja wa sahaba zake) alimwambia: "Ewe Amirul-Mu'minina ukifanya safari katika wakati huu nahofia hautofanikiwa mradi wako kwa mujibu wa ilimu ya nyota." Akasema (a.s):

"Wadhani kuwa wewe unaelekeza saa ambazo mwenye kufanya safari katika saa hizo ataepushwa na jambo baya, na unahofisha saa ambazo mwenye

---

1. Nisamehe kwa niliyoahidi: Ukiazimia tendo la kheri, ni kama kwamba umechukua ahadi binafsi kuwa utatekeleza amri ya Mungu, na endapo haukupata tawfiiqi ya kutekeleza, ni kama Mungu hajaona utekelezaji wa ulilomuahidi, kwa hali hiyo unakuwa umemkhalifu, na mwenye kukhalifu ahadi ni muovu. Kwa hivyo yeye anaomba msamaha wa uovu wa aina hii. (Na hiyo ni daraja ya juu ya uchamungu, sio ya watu wa kawaida).

2. Kujikurubisha kwa ulimi hali moyo uko kinyume: Kama vile mtu aseme kwa mfano: Al'hamdu lillahi alaa kulli haali, na aghlabu yuakasirika katika baadhi ya hali. Au aseme: Iyyaka na'abudu wa Iyyaka nasta'iinu - Wewe tu tunakuabudu na Wewe tu tunakuomba msaada - hali akiwa yu amuabudia na kumwomba msaada mwingine na anawatukuza walio duni kuliko Yeye (s.w.t).

kusafiri humo atakumbwa na jambo la madhara? Hivyo basi mwenye kukusadiki kwa hilo atakuwa ameikadhibisha Qur'ani, na atakuwa amejitosheleza hatohitaji kuomba msaada kwa Mungu ili kuyapata yapendwayo na kujikinga na makruhu; kwa kauli yako hii wamtaka atakeye itendea kazi amri yako akumiminie shukrani wewe sio Mola wake, kwa kuwa wewe - kwa dhana zako - ndiye uliye muongoza saa ambazo kwazo amepata manufaa, na ataepukana na madhana."

Kisha Aliwaelekea Watu (a.s) Akasema:

"Enyi watu! Jihadharini na kujifunza elimu ya falaki isipokuwa kiasi cha kupata mwongozo, bara au baharini[1], kwa kuwa hiyo (falaki) inaitia kwenye ukuhani, na mwanafalaki ni sawa na kuhani, na kuhani ni kama mchawi[2], na mchawi ni sawa na kafiri na kafiri (marejeo yake) ni motoni. Safirini kwa jina la Mungu."

## 80 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

Baada Ya Vita Vya Jamal (Ngamia) Katika Kuwalaumu Wanawake

"Enyi watu, kwa hakika wanawake ni wapungufu wa imani[3], wapungufu wa hisa, wapungufu wa akili. Ama kuhusu upungufu wao wa imani ni kule kubaki kwao bila sala na saumu siku zao za hedhi. Ama upungufu wao wa akili ni kule kuwa ushahidi wa wanawake wawili ni sawa na ushahidi wa mwanaume mmoja. Ama upungufu wao wa hisa ni kule kuwa mirathi zao ziko nusu ya mirathi za wanaume. "Hivyo basi zicheleeni shari za wanawake na jihadharini na walio wa kheri miongoni mwao, wala msiwape tamaa katika jema ili wasiwe na tama katika jambo la munkari.[4]"

---

1. Utashi wa kujifunza elimu ya anga na mienendo ya sayari kwa ajili ya kupata mwon-gozo haujakatazwa ila tu yu akataza ile ijulikanayo kwa jina la (falaki) nayo ni elimu iliyojengeka kwa misingi ya itikadi ya kuwa sayari zina ruhaniya, na yakuwa roho hizo za angani zina mamlaka ya kiroho juu ya vitu vya asili (vya kimaada), hivyo mwenye kuwa na mawasiliano na roho zake kwa aina fulani ya utayarifu kwa kusaidiwa na riyadha, humdhihirikia yaliyofichika miongoni mwa siri za wakati uliyopo na wa baadaye.

2. Al-Kaahinu: Kuhani ni mtu ambaye anadai kufichua ghaibu, na maneno ya Amirul-Mu'minin (a.s.) ni hoja yenye nguvu dhidi ya mawazo ya wanaoamini ramli na hesabu na kutazamia nyota na mfano wake, na ni dalili ya wazi ya kutosihi kwake na kuwa kwake kinyume na misingi ya sheria na ya kiakili.

3. Mwenyezi Mungu amewaumba wanawake na kuwabebesha uzito wa kuzaa na kulea watoto mpaka miaka maalum, inakaribia kutokwisha mpaka wanajiandaa kubeba mimba na kuzaa hivyo hivyo, wanakaribia kutokuwa kando na uzazi na kulea watoto, kana kwamba wao wamefanyiwa mahususi kuratibu mambo ya nyumbani na kubaki huko. Nayo ni duru yenye kikomo ambayo waume zao wanawasimamia, hivyo amewaumbia akili kwa kadiri wahitajiavyo kwa hili, na ikaja sheria inayoafikiana na hali ya kimaumbile wakawa wao katika hukumu za kisheria hawalingani na za wanaume, si katika ibada wala shahada wala mirathi.

4. Hakusudii aache (mtu) jema ilimradi tu ni kwamba wao (wanawake) wametoa amri. Kwa sababu kuacha kutenda jema ni kinyume na Sunnah njema hasa endapo itakuwa jema hilo ni miongoni mwa wajibu, bali yu ataka tendo la wema lisiwe limefanyika kwa ajili ya kuwatii wao tu, kwani ufanyapo jema fanya kwa sababu ni jema, usilifanye kwa kutekeleza amri ya mwanamke. Kwa kuwa Imam alikwishasema kauli ambayo imethibiti ndani ya dahari ndefu, na hapana anayeachwa nje kwa hayo aliyoyasema ila kwa baadhi miongoni mwao

Sibti ibn Jauzi ameieleza katika at-Tadhkira uk. 85, na ameieleza baadhi yake Abu Talib al-Makki katika Fautul- Qulub, Jz. 1, uk. 282.

## 81- NA MIONGONI MWA MANENO YAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Maneno Yake (a.s) - Saduq ameieleza katika Ma'anil-Akhbar, uk. 251, na katika al-Khisal, Jz. 1, uk. 11, na al- Barkiy katika al-Mahasin, uk. 234.

### KUHUSU ZUHUDI (KUTOTILIA MANANI RAHA YA DUNIA)

"Enyi watu! Zuhudi ni kupunguza matumaini[1],na kushukuru neema[2], na kuogopa kujiingiza kwenye haramu[3], na endapo hilo likiwa mbali kwenu basi haramu isiishinde subira zenu[4],wala msisahau shukrani kwenye neema, Mungu amemaliza udhuru kwenu[5],5 kwa hoja zilizo wazi, na vitabu vilivyo na udhuru wa wazi.".

## 82 - NA MIONGONI MWA SEMI ZAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Semi Zake (a.s) Sharifu ar-Radhiy amesema: 'Nasema: Mzingatiaji akizingatia kauli yake (a.s): "Atakayeizingatia itampa mwanga" chini yake atakuta maana ya ajabu, na lengo la mbali, lisilofikiwa upeo wake wala hakifikiwi kina chake hasa hasa ikilinganishwa na kauli yake:

---

waliotunukiwa hali ya kimaumbile iliyo ya juu kuliko ya kawaida ya utambuzi, au yakaribiana, au malezi yao yana mamlaka ya hali ya juu, kinyume na silka iliyowekwa katika wao na ikamgeuza mbali na yalikomuelekeza maumbile.

1. Kupunguza matumaini: Kuchelea mauti na kujiandaa nayo kwa matendo, na wala mradi wake sio kuungojea umauti bila ya kazi.

2. Kushukuru neema: Ni kutambua kuwa yatoka kwa Mungu na kuitumia kulingana na sharia.

3. Sheikh Muhammad Abduh amethibitisha katika matni kuwa kuogopa maana yake ni kujizuia na jambo lisilo wazi ukweli wake, ili kuchelea kuingia ndani ya matendo ya haramu. Yaani endapo la haramu likijitokeza itakuwa ni katika zuhudi kujizuia na linalofanana nalo sembuse la haramu.

4. Hilo likiwa mbali kwenu basi ni mambo mawili katika matatu ambayo hapana budi na mawili hayo; mambo hayo ni: woga na kushukuru neema, ameyafanya kuwa na nguvu zaidi na ni muhimu sana kuliko kufupisha matumaini, na endapo ikiwawia vigumu kufupisha matumaini yenu na kuwa katika ukamilifu wa zuhudi itakiwayo kwenu, basi haramu isi-ishinde subira yenu, yaani hizi nguzo mbili nyingine zisikupiteni, nazo ni: Kushukuru neema, na kujiepusha na haramu; kwa sababu kusahau shukrani kwavuta kujidai, na kutenda ya haramu kunaharibu nidhamu ya maisha haya na ya marejeo. Na kujidai na ufisadi vyaleta malipizi duniani, na maisha ya mashaka na majuto akhera.

5. Mungu amemaliza udhuru kwenu yaani ametimiliza, anakusudia kuwa yeye ameweka wazi kwenu kwa hoja zenye mwanga zinazowajibisha kujiuepusha, na zinazowajibisha kutenda, endapo mtafanya kinyume adhabu itakuwa wajibu juu yenu, hivyo Yeye katika kuwaadhibu anao udhuru. Na yaani amefanya insafu, na hamza hapa wanasema yamaanisha kuondoa, yaani usemapo yaani nimempa fulani udhuru yamaanisha nimeondoa udhuru wake sikumwachia nafasi ya kutoa udhuru endapo atahalifu niliyomnasihi. Na pia husemwa yaani nimejisimamishia binafsi kwake udhuru uliowazi kuhusu adhabu nitoayo kwake kwa kuwa nimemhadharisha na nimempa nasaha.Na inafaa ibara iwe katika kitabu kwa maana hii pia, bali yenyewe ndio iliyo karibu na tamko Ilaykum. Na maneno yanakuwa majazi na kutimia kwa hoja upande wake ni kukam lika kwa udhuru kwetu.

“Atakayeikodolea macho itampofusha” kwani yeye atakuta tofauti wazi yenye mwanga na ajabu kubwa kati ya “Atakayeizingatia” na “Atakayeikodolea macho”. Salawatul-llahi wasalamuhu alayhi.’

### KUHUSU DUNIA NA WATU WAKE

“Nieleze nini kuhusu dunia hii ambayo mwanzo wake ni taabu, na mwisho wake ni kuharibika. Ya halali yake yatakuwa na hesabu, na ya haramu yake yatakuwa na adhabu. Awaye tajiri humo (duniani) hukabiliwa na fitna. Na maskini humo yu ahuzunika. Mwenye kuipenda sana huikosa[1],na mwenye kuitupilia mbali humwelekea[2].

Atakayeizingatia itampa mwanga, na atakayeikodolea macho itampofusha.[3]”.

# NAHJUL BALAGHA

## JUZUU YA PILI

### MTARJUMI: HARUNA PINGILI

## 83 - MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE [(A.S)]

Miongoni Mwa Khutba Zake [(a.s)] - Ibn Shu’uba ameieleza katika ‘Tuhaful’uquli’ uk. 146; Na Al-Qaadhi Al-Qudhaiy katika mlango wa tatu wa kitabu ‘Dasturu maalimil’Hukm’ uk. 59; Na Abu Na’im katika ‘Al’hilya’ Juz. 1, uk. 77; Na Al-Amidiy katika ‘Ghurarul’hukam.’

### NAYO NI MIONGONI MWA KHUTBA ZA AJABU, NA HUITWA ‘AL-GHARRAAU’:

1. Sa’aha: Yaani juhudi imemuwia sawa, yaani imemwendea sawa katika utashi wake. Na al-Qasdu: ameitilia umuhimu katika kuitafuta. Na kauli yake; ‘huikosa’: yaani kila akipata kitu hufunguka milango ya matumaini katika kitu hicho, inakaribia kwamba hakidhi haja ila nyingine humwita kwenye haja elfu moja.

2. Humkubali, yu akusudia mwenye kuzipima ladha ziishazo kwa mpito kwa kipimo chake cha ukweli na akajua kuwa kuzifikia huwa kwa taabu, na kuzikosa kwaishia kuzijutia, na kustarehe nazo hakukosi mchanganyiko wa machungu, maisha haya yatamuia vyema na kumweka katika raha, kwa kuwa yeye hajutii limkosalo humo, wala hakabiliwi na dharura ya lililopo, wala hataabiki na machungu ya kungoja lijalo.

3. Ameizingatia: Yaani mwenye kuifanya kioo cha kusafisha moyo wake na kuona athari ya matendo matukufu na kumjia kivuli cha matukufu yaliyobaki, yaliyotendwa na mikono ya wakamilifu, na kumfichulia matokeo mabaya ya wajinga miongoni mwa watu wa raha, dunia inakuwa kwake funzo, na matukio yake ni uelewa. Ama mwenye kuikodolea, na akashughulika nayo huyu anakuwa mpovu katika kila kheri humo, na analiwazika na vitakavyotoweka badala ya vitakavyobaki, ubaya ulioje wa aliyojichagulia kwa ajili ya nafsi yake.

“Ninamhimidi Allah (s.w.t) ambaye amekuwa na daraja ya juu kwa nguvu Zake[1], na amekurubia kwa fadhila Zake[2], Mtoaji wa kila faida na fadhila, na muondoaji wa kila kubwa na dhiki. Ninamhimidi kwa ajili ya huruma na ukarimu Wake, na uwingi wa neema Zake. Na ninamwamini kwa kuwa ni wa mwanzo Aliye dhahiri[3], na ninamuomba mwongozo kwa kuwa yu karibu mwongozaji.

Na ninamuomba msaada kwa kuwa ni mshindi mwenye nguvu. Na ninamtegemea kwa kuwa ni mtoshelezaji, mnusuru. Na ninashuhudia kuwa Muhammad **(s.a.w.w)** ni mja Wake na Mtume Wake, amemtuma ili kutekeleza amri yake, na kumaliza udhuru wake[4], na kutoa maonyo yake[5].

“Nakuusieni! Enyi waja wa Mungu kumcha Mungu ambaye amekufanyiyeni mifano[6], na amekuwekeeni wakati maalumu wa maisha, na amekuvikeni riyasha (yaani vazi)[7],na ameyafaharisha maisha yenu[8] na kuyaboresha, na amekuzungukeni kwa hesabu[9],na amekuandalieni malipo, na amekutunukieni neema nyingi na takrima kwa wasaa. Amekuonyeni kwa hoja za wazi bainifu. Amekufanyeni kwa idadi, na amekuainishieni muda, ndani ya nyumba ya balaa na mtihani, na kwenye nyumba ya mazingatio ninyi ni wenye kufanyiwa mtihani humo, nanyi mtahesabiwa matendo yenu.”

---

1. Nguvu: Amekuwa na daraja ya juu kwa nguvu zake: Yaani ametukuka na kupaa kuliko kila kisichokuwa Yeye; kwa nguvu zake zilizo na mamlaka ya juu ya kuumba kuliko kila nguvu.

2. Fadhila: Amekurubia kwa fadhila Zake: yaani Yeye pamoja na kuwa juu Kwake kwa utukufu, amesogea na kuwa karibu na viumbe Wake kwa fadhila Zake, yaani kwa upaji na ihsani Zake.

3. Maana inakuwa: Namsadiki Mungu kwa kuwa yeye ni wa mwanzo kabla ya chochote katika kuwepo, kwa hivyo Yeye yu dhahiri dhati Yake na mdhihirishaji wa vingine, na mwenye kuwa hivyo kumsadiki kunakuwa hakuna shaka. Na aliye karibu na mwongozaji yapendeza aombwe hidaya, na muweza mshindi anafaa kuombwa msaada, kwa kuwa ndiye mwenye uwezo wa kusaidia. Na mtoshelezaji mnusuru ndiye wa kutegemewa.

4. Kumaliza udhuru wake: Ni kufikisha kwake. Na udhuru hapa: Ni kinaya yamaanisha hoja ya kiakili na ya kunakili au kunukuu ukitaka, zilizowekwa kwa kutumwa kwake Nabii (s.a.w.w). Kwa kuwa mwenye kuhalifu sharia ya Mungu atastahili adhabu, na mwenye kuitekeleza anastahiki thawabu nyingi.

5. Maonyo: Yaani utoaji habari wa ki-ungu wenye kuonya adhabu kwa kutenda maovu.

6. Mifano ameileta katika maneno ili kuziweka wazi hoja na kuziimarisha ndani ya fahamu.

7. Na sababu ya vazi kuwa neema: Kwa kuwa ni stara ya utupu, na ni hifadhi ya baridi na joto.

8. Ameyafaharisha maisha, yaani ameyafanya kuwa ya hali ya juu yenye wasaa na kustawi.

9. Amekuzungukeni kwa hesabu: yaani amejaalia hesabu za matendo yenu na kuyajua kama tendo la kuzungushia ukuta kiasi kwamba hamtotoka nje ya ukuta huo wala kuuvuka wala mtu yeyote kuachwa nje yake.

## KUTAHADHARISHWA NA DUNIA

"Kwa kweli dunia kinywaji chake kimetibuka, chanzo chake kina udongo na tope. Mandhari yake yanavutia, na yanaangamiza.

Ni yenye kudanganya na kutoweka, na ni mwanga utowekao haraka na kivuli kipitacho, na ni nguzo iliyoelemea upande, mpaka anayeichukia aanzapo kuifurahia, na mwenye kuichukia aanzapo kuwa na matumaini, punde yainua miguu yake na kuirudisha chini na kumnasa mwanadamu kwa kamba yake, na kumuuwa pale pale kwa mishale yake, na kumfunga mtu[1], shingoni kamba ya kifo ikimuongoza kwenye malalo yaliobana (yaani kaburi), na marejeo ya upweke, na kuainisha mahali[2] - na thawabu za Aamali[3].

Na hivyo hivyo waliokuja nyuma baada ya waliotangulia, kifo hakikomi kuziondoa nafsi, wala waliobakia hawakomi kutenda dhambi. Watafuatia mfano wao- (mfano wa waliotangulia katika matendo).

Wanapita kwa makundi mpaka upeo wa mwisho, na mwisho wa mambo, mpaka mambo yatakapokatika, dahari zitakapopita, na kukaribia kufufuka, Mungu atawatoa nje kutoka makaburini, na viota vya ndege, na maficho ya wanyama wakali, na katikati ya maangamizi.

Wataharakia kwenye amri Yake, wakienda haraka kuelekea maeneo yalioandaliwa kwa marejeo yao ya mwisho makundi kwa makundi, wakiwa kimya, hali wamesimama safu kwa safu, wakiwa katika kuonwa na Mungu wakiwa mahali mwitaji aweza kuwaita wamsikie.

Wakiwa na vazi la unyonge, wakifunikwa na unyenyekevu na udhalili, hila imekwisha, matumaini yamekatika, nyoyo zikiwa hazina furaha[4], sauti zikiwa zimedhoofu, hafifu, na jasho limekuwa kama hatamu[5], hofu imekuwa kubwa, na masikio yatakabiliwa na radi, kwa kelele ya sauti ya mfanya daawa, akiwaita kwenda kwenye upitishwaji wa maamuzi, na kupata malipo mbadala adhabu na kupata thawabu.[6]".

---

1. Yaani imemtega na kumnasa kwenye mtego wa kamba zake yule mwenye kughurika nayo (dunia).

2. Kuainisha mahali: yaani mahali ambapo mtu mukalafu - mwenye majukumu - atakapo fikia baada ya kifo, hapana budi kwa kila mtu mukalafu kuijuwa baada ya kifo hali yake itakavyo kuwa, peponi au motoni, na ataona mahali pake kati ya neema (za peponi) na (mateso ya) Jahannam.

3. Thawabu za aamali: Anakusudia malipo kwa sura ya jumla yanayoienea furaha na mashaka.

4. Nyoyo zimeporomoka: yaani hazina furaha wala matumaini ya kuwa na mafanikio, zikiwa kimya kwa kukabiliwa na mfadhaiko.

5. Jasho limekuwa hatamu limekithiri kiasi cha kujaa midomoni kwa wingi wake na kuzuia uwezo wa kusema na kuwa kama hatamu.

6. Mbadala: yaani ubadilishanaji wa malipo ya kheri kwa kheri na shari kwa shari.

## KUWATANABAHISHA VIUMBE

"Waja wenye kuumbwa kwa uwezo, na wamemilikiwa kwa kahari[1], na mamlaka, na watakufa kwa kuhudhuriwa na Malaika wachukuaji roho[2], na watawekwa kaburini, na hatimaye kuwa mifupa iliyochakaa, na watafufuliwa (kila mtu) pweke[3], na watalipwa malipo, na watafanyiwa hisabu kila mtu na yake[4] walipewa muda wa kujiepusha[5], na waliongozwa njia ya wazi[6], na waliruhusiwa kuishi na muda wa kutafuta maridhawa, na wameondolewa giza la shaka, na wameachwa kwenye medani ya mashindano ya farasi[7], na kuachwa wafikiri na kutafuta yahitajiwayo kwa mazingatio, kuwa na uvumilivu wa mtafutaji, anayejaribu kukipata kilichompotea, katika muda wa harakati za kazi kabla ya ajali."

## UBORA WA KUKUMBUSHA

"Mifano muwafaka ilioje na mawaidha yaponyayo! endapo yangeafikiana na nyoyo safi, na masikio sikivu, na rai zenye azma na akili thabiti!

"Mcheni Mungu uchaji wa mwenye kusikiliza na akanyenyekea, na atendapo ovu yu-atambua, na akiogopa hutenda yaliyo sawa, akiwa na hadhari huharakia kwenye mema, akiwa na yakini hufanya mema, akipewa mazingatio mara kadhaa huzingatia, akitahadharishwa hujihadhari, akikaripiwa hukaripika, aitwapo na wito wa mlinganiaji (kwa Mungu) hurejea kwake.

Arejeapo hutubu, na akifuata hufanya vizuri, akionyeshwa njia ya sawa huiona na yu aharakia akitafuta, na kuokoka mbio! na yuafaidika na mali, na kuwa na tabia njema, na kuyajenga marejeo, na akabeba masurufu mgongoni

---

1. Iq'tisaran: wamilikiwa kwa ushindi: yaani wao kama vile walivyoumbwa kwa uwezo Wake Mungu (s.w.t) na kwa nguvu Zake, pia wao ni wamilikiwa kwa mamlaka ya uwezo Wake, hawana hiyari katika hilo, na muda wao ujapo roho zao zitachukuliwa na kupelekwa Kwake (s.w.t) na wanaohudhuria miongoni mwa watowao roho na nguvu yenye mamlaka juu ya uishaji wa viumbe.

2. Asili ya kuhudhuria: ni kuhudhuria Malaika ili kuchukua roho. Na Waarabu walikuwa wakisema: Maziwa yemehudhuriwa, yaani yameharibika, wakimaanisha kwamba majini yamehudhuria na kuharibu yale maziwa, husemwa 'al-Labanu muhtadhwaru faghatwi ina'aka': Maziwa yamehudhuriwa, hivyo funika chombo chako.

3. Watafufuliwa pweke: Yaani, kila mtu ataulizwa mwenyewe binafsi, haitozingatiwa jamii anayoungana nayo, kutokana na kauli Yake s.w.t: "Walaqad ji'itumuna furada." Hakika mmenijia kila mmoja pweke. (An-A'am: 94).

4. Watafayiwa hesabu kila mtu na yake: Yaani kila mmoja atahesabiwa A'amali zake mbali na mwingine kutokana na kauli yake swt: "Na mbebaji hatabeba mzigo wa mwingine" 35:18): "Na enyi wakosefu! Jitengeni leo" (36:59).

5. Walipewa muda: Yaani walingojewa ili watafute njia ya kutoka, yaani walingojewa warejee kwenye utii na watubu kwa ikhlasi, kwa sababu kufanya toba kwa ikhlasi ndio epuko la kutoka tanzi la maasi.

6. Njia ya wazi: Ni njia ambayo sheria takatifu imeonyesha.

7. Wameachwa: Yaani wameachwa uwanjani wanashindania heri. Na muda ambao uliowekwa. Na katika riwaya nyingine, ni mahali ambapo ni pa heri, yaani mahala ambapo wanashindana wachamungu kumridhisha Allah s.w.t.

kwa ajili ya siku ya kuondoka kwake, na akaelekea njia aikusudiayo na hali ya haja yake, na mahali pa mahitaji yake, na kutanguliza mbele yake kwa ajili ya nyumba ya kubaki kwake.

Hivyo basi mcheni Mungu, enyi waja wa Mungu kwa upande wa lengo alilokuumbieni [1], na mjihadhari upeo wa kujihadhari na ambayo amekuhadharisheni nafsi yake [2], na kuweni wastahiki wa ambayo amekuandalieni[3], kwa kutekeleza ya wajibu[4], na kujihadhari na marejeo yake yanayotisha."

Na Sehemu Hii Ya Khutba Kuwakumbusha Watu Neema Za Mungu

"Amekujaalieni masikio ili muweze kufahamu na kuyahifadhi aliyoyakusudia, na macho ili muweze kutandua tandabui ya giza giza, na viungo vya mwili vyenye kuwemo ndanimwe viungo vingine, na vyenye kulingana na umbo la mahali khusika katika muundo wa sura zake, na muda wa umri wao, na miili yenye kutekeleza manufaa yake, na nyoyo ambazo zimeshughulika kutafuta chakula chake, ndani ya neema zake zilizo funi- ka, na yawajibishayo upaji wake, na vizuizi vya afya yake[5].

"Amekukadirieni umri aliousitiri mbali na (uelewa wenu) amekubakishieni mabaki ya athari za waliopita kabla yenu, ili iwe mwongozo kwenu, watu hao walistarehe na hisa zao kubwa, kwa nafasi bila ya kizuizi[6].

Kifo kiliwachukua bila kufikia matumaini yao, (kifo) kiliwakata na kuwa'ngoa mbali nayo - matumaini - hawakujiandaa wakati miili iko salama, wala hawakuzingatia mwanzoni mwa umri wa ujana. Je wenye ngozi laini ya ujana wanangoja mpaka kupinda migongo kwa uzee!

Na ambao wana siha njema wanangoja kufikiwa na hali mbaya ya siha! Na walio na muda wa kubaki wanangoja mpaka uishe, pamoja na ukaribu wa

---

1. Upande wa lengo alilokuumbieni: Yaani kusudieni upande ule ambao Mungu amekuumbeni kwa ajili yake huo, nao ni: Ibada, kwa sababu yeye swt amesema: "Sikuwaumba majini na watu ila waniabudie Mimi." (adh-Dhaariyatu: 96) Yaani mcheni Mungu mkielekea upande ambao amekuumbeni kwa ajili yake, miongoni mwa matendo yenye kukunufaisheni yenye kubaki athari yake kwa watakaokuwa baada yenu.

2. Ametuhadharisha nafsi yake (s.w.t) tusijihusishe na yanayomghadhibisha kwa kuhalifu amri zake na makatazo yake.

3. Kauli yake Amirul-Mu'minin (a.s): "Kuweni wastahiki wa ambayo amekuandalieni: Yaani, mjijaalie binafsi wastahiki wa thawabu Yake ambayo amekuandalieni endapo mtatii."

4. Ukisema: Yatanajazul-haajata: Anaiharakia haja, anaifanikisha na anataka haraka yake, na An-Najizu: Al-Aajilu - ni mwenye haraka. Watanajuzu minal'mukallafina na kuharakia kwa Mukhallafin bisidqi miiadihi Sub'hanahu; kwa kusadikisha wajibu Wake (s.w.t) Wa huwa muwadhabatuhum ala fi'ilil-wajibi, nako ni kudumu kwao juu ya tendo la wajiu, watajanubul-Qabiihi, na kujiepusha na maovu. Na uharakiaji huu wa matendo (mtu) huwa yuastahiki aliyowaandalia Mungu watu wema.

5. Vizuizi vya afya: Yaani, afya inazuia madhara kwa ajili yenu.

6. Na kadirio la maneno ni: Ameacha kwa ajili yenu mafunzo kutoka karne za watu waliopita, miongoni mwayo kustarehe kwao na hisa zao za dunia kisha kumalizika kwao, na miongoni mwayo ni wasaa wa kusongeka kwao na urefu wa muda walioachiwa, kisha mwisho wao ulikuwa ni kuangamia.

kutoweka, na mbabaiko wa kutoweka, na kufikiwa na huzuni moyoni, na kusongwa na mate, na hofu ya mgonjwa na uchungu wa huzuni, na mbinyo wa mate.
Muda utafika wa kuomba nusra ya wajukuu na ndugu wa karibu, wapenzi na wenzi. Je! Ndugu wa karibu wamezuia, au vilio vimeleta nafuu!
Ameachwa mahali pa wafu amefungika, na kwenye malalo yaliyombana akiwa mpweke, wadudu wameirarua ngozi yake, na matukio yameuchakaza upya wake, na dhoruba itakuwa imefuta athari zake, na tukio litakuwa limefuta dalili zake, na miili itakuwa imehiliki baada ya kujaa kwake, na mifupa itakuwa imeoza baada ya nguvu zake, na nyoyo zitakuwa zimefungika kwa uzito wa mizigo (dhambi) yao, zitakuwa na yakini na habari zake zilizojificha, hazitotakiwa baada ya hapo kuzidisha Aamali zake njema[1] wala hazitoombwa kutubia kwa ajili ya ubaya wa kuteleza kwake![2].
Je! Hamko wana wa kaumu hii, na mababa zao, ndugu na jamaa zao wa karibu? Mnafuata mifano yao na kuiga njia zao[3] na mwaenda njia zao, nyoyo ziko bado ngumu, zimeghafilika mbali na mwongozo wake, zaenda njia isiyokusudiwa! Kama kwamba mkusudiwa ni mwingine, kama kwamba mwongozo upo katika kukusanya dunia yake."

## HADHARI YA KITISHO CHA AS-SIIRAAT

"Na juweni kuwa mtapaswa kuvuka juu ya as-Siiraat nyayo zitateleza kiasi cha kumtupa mtu chini, na vitisho vya utelezi wake na mfululizo wa vitisho vyake.
Basi mcheni Mungu enyi waja wa Mungu uchaji wa mwenye akili, ambaye fikra zimeushughulisha moyo wake, na hofu imeutaabisha mwili wake, na sala ya tahadjudi imemfanya akeshe, na matumaini yamembakisha na kiu nusu ya mchana wa siku yake, (yaani anafunga mchana wake) na zuhudu imezuia matamanio yake, na dhikr ya Mungu imeufanya ulimi wake kuwa mwepesi, na ametanguliza hofu kwa ajili ya amani yake[4] akajiepusha njia zilizo kombo kwa kufuata iliyo sawa, kwa ajili ya iliyo sawa, yu afuata njia iliyonyooka zaidi ili kuifikia njia ihitajiwayo; wala geuzo la ghururi halikugeuza fikra yake, wala mkanganyiko wa mambo haukumfanya asijue ukweli.

---

1. Zitakuwa na yakini na habari zake zilizofichika: yaani zitakuwa zimefichukiwa na yaliyokuwa yamejificha miongoni mwa habari zake, na yaliyoandaliwa kwa ajili yake akhera, kwa kuwa mtu baada ya kifo chake hujua hali yake itavyokuwa kama ni peponi au motoni!.

2. Hawatokalifishwa baada ya hapo amali nzuri ya ziada, kwa sababu hapana amali baada ya umauti, wala haiombwi toba ya maovu; kwa sababu taklifu imetoweka.

3. Al-Qidda: Husemewa kwa ajili ya kikundi cha watu wakiwa wako katika utashi wa aina moja, na kutokana na neno hilo, kauli Yake Mwenyezi Mungu swt: Wa kunna taraiqa qidada (al-Jinnu: 11). Na maana: mwafuata athari zao na mnashabihiana nao katika maten- do yao.

4. Ametanguliza hofu kwa ajili ya amani yake: yaani ametanguliza hofu hapa duniani ili apate amani akhera, au ametanguliza hofu wakati ambao hofu yafaa wakati ule, kwa kuwa siku ikiwadia hofu haitomsaidia kitu mwenye hofu.

Akiwa katika hali ya furaha kwa bishara ya kufaulu neema ya maisha mema, katika neema kubwa ya usingizi wake, na siku yake yenye amani mno.
Akiwa amevuka kivuko cha hii haraka (dunia) mwenye kuhimidiwa[1], na akiwa ametanguliza masurufu ya baadaye akiwa na furaha, na ameharakia kutoka kwenye woga[2] na akakaza mwendo katika muda wa uhai[3] na akapenda kipaswacho, na kukiepuka kinachobidi, katika siku yake akaichunga kesho yake, na akaangalia yanayokuja mbele miongoni mwa a'amali, yaani akaangalia atakachokitanguliza miongoni mwa aamali.
Yatosha pepo kuwa ni malipo mema na mafanikio, na moto ni adhabu tosha na mateso, Mungu (s.w.t) ni mlipizaji tosha na mnusuru! Na Kitabu (Qur'ani)[4] ni hoja tosha na hasimu.

"Nakuusieni kumcha Mungu ambaye hakuacha udhuru kwa aliyoyaonya, na ametoa udhuru kwa onyo lake wazi[5], amekutahadharisheni na adui aingiae vifuani kwa kificho[6], na kupulizia masikioni kwa siri, kwa njia hiyo, amepotosha na kufanya uharibifu.
Atoa ahadi ya uwongo na kuyapamba maovu, na kudharau madhambi makubwa yaangamizayo, mpaka anapomporomosha kutoka daraja ya mwongozo mwenzi wake[7], naye atastahiki rehani yake, atakuwa yuakanusha aliyokuwa akiyapamba, na kuyakuza aliyokuwa akiyadharau, na kuyatahadharisha aliyokuwa akiyafanya yako salama."

## MIONGONI MWAYO MAELEZO YA KUUMBWA MWANADAMU

"Au mwangalie mwanadamu ambaye Mungu amemuumba ndani ya giza la mfuko wa uzazi na mifuniko ya sitara, ikibubujikiwa na manii, kisha likafanyika pande la damu lisilo na sura, baada ya hapo mimba, halafu kitoto kichanga kinyonyacho, kisha mtoto, baada ya hapo kijana, kisha amemtunukia moyo wenye kumbukumbu, ulimi wa kunenea, na macho

1. Kivuko cha haraka: dunia na imeitwa kivuko cha haraka kwa sababu ni njia ambayo huvuka (mtu) kuiendea akhera, nayo ni ya baadae.

2. Ameharakia kutoka kwenye woga: yaani ameharakia kutenda mema akiogopa asije kuyakuta yakutisha.

3. Amekaza mwendo katika muhula wa uhai.

4. Kitabu: ni Qur'ani. Na hoja na hasimu: yaani ni chenye kunaisha, kwa ambaye atak- wenda kinyume nacho atajikokotea maangamizi ya nafsi yake. Na inaweza ikakusudiwa kwamba kitabu ni yale yaliyoandikwa miongoni mwa a'amali za mtu atakapokabidhiwa Siku ya Hesabu.

5. Ametoa udhuru kwa onyo lake. Au kwa maana ya: Ameondoa udhuru wa mtoa udhu- ru kwa onyo lake la hali ya matendo itakavyokuwa, na hoja upande wake imetimia dhidi ya wapotovu kwa yale aliyoyaweka wazi miongoni mwa njia za kheri na za ubora.

6. Adui aliyetajwa: Ni Shetani, na kuingia kifuani ni tamthili ya uingiaji wa wasiwasi wake ndani ya nafsi, kwa hivyo yeye anayoyapamba yanakwenda mwendo wa pumzi, na anakwenda na anayokuja nayo kwa mwenendo wa marafiki kana kwamba ni mwandani anakupa siri na anakunong'oneza katika sikio lako ambayo unayadhania ni kheri kwako.

7. Mwenzi hapa ni mwanadamu ambaye amekuwa mwenzi wa Shetani, Mungu (s.w.t) amesema: "ni rafiki muovu mno!" (43:38).

yakuonea, ili aweze kufahamu na kuzingatia, apate kuacha kutenda maovu akijiziwia (kwa nguvu za mazingatio) afikiapo utu uzima, na kufikia kimo chake cha kawaida, na umbo lake kufikia kimo chake.

Akanusha kwa kiburi, aingiwa na ghururi na kubabaika bila kujali. Aijaza ndoo kubwa ya matamanio yake, afanya juhudi kukamilisha utashi wa dunia yake, katika matamanio yake, akienda na yanayomdhihirikia katika utashi wake. Kisha hakuogopa uovu wowote, wala kutishika wala kuwa na wasiwasi. Alikufa ndani ya maovu yake hali yukijana aliyeghurika. Aliishi akiwa makosani kwa muda mfupi. Hakufaidika na thawabu mbadala. Wala hakutekeleza wajibu wowote. Maradhi mabaya yalimkabili akiwa bado na ukaidi wake katika njia ya furaha yake kubwa, na alipitisha usiku akiwa kama amelewa[1].

Alikesha akiwa katika shida ya majonzi na machungu, kufikiwa na uchungu na magonjwa, kati ya ndugu na ndugu wa damu, na baba mwenye huruma, na mama anayelia akisema: ole wangu mwenye huzuni, dada apigaye kifua akiwa amefadhaika; na mtu yu katika sakarati ya mauti anataabika na shida ya kukatisha tamaa, na mvuto wa kuchukiza, na msukumo wa sakarati ya mauti.

Kisha yuatiwa ndani ya sanda akiwa mublisa[2] mwenye kukata tamaa ya rehema ya Mungu avutwa kwa urahisi[3], kisha kutiwa ndani ya jeneza akiwa mwenye machovu ya kutupwa, na aliyekondeshwa na ugonjwa.

Akibebwa na wasaidizi vijana, na ndugu wasaidizi wambeba wakimpeleka kwenye nyumba yake ya upweke na na watu huacha kumzuru[4], na mahali pa upweke, mpaka wanaporudi waliokuwa wakimsindikiza na akarejea wenye huzuni, atakalishwa shimoni mwake akisemeshwa[5] kwa faragha maswali ya kuduwaza, na mtihani wa kujikwaa.

Na balaa kubwa mno huko ni kuingia maji ya moto na kuteseka na Jahannam, na kutokota kwa moto, na ukali wa sauti ya moto, hakuna muda wa mapumziko, wala wa raha, wala nguvu ya kuzuia wala kifo cha kutuliza, wala

---

1. Na hapa makusudio yake (a.s.) ni: Maradhi yaliyomuangamiza, na hiyo ilitokea baada ya kukabiliwa na huzuni za kifo: nazo ni uzukaji wa maradhi ya kuangamiza yasababishayo kifo.

2. Mublisu: Ambaye amekata tamaa ya kupata rehema ya Mungu, ukisema ablasa: yaani ni amekata tamaa. Na humo limechukuliwa neno Ibilisi. Na Iblis pia: ni kule kuingiwa na huzuni baada ya kukata tamaa kwa kila hali.

3. Kuvutwa kwa urahisi hapa kunaishiria kuishiwa na uwezo kiasi cha kushindwa kukataa kitu.

4. Nyumba yake ya upweke: ni kaburi lake. Na pia kukatika kwa ziara yake: kwa sababu kutembelewa kutakatika, hatofanyiwa ziyara.

5. Atakalishwa shimoni mwake akisemeshwa: Hili ni tamko la wazi kuhusu adhabu ya kaburini.

usingizi wa kuliwaza, atakuwa kati ya aina mbalimbali za maiti[1], na adhabu za kila wakati na saa zote! Hakika tunajilinda na Mungu.

Enyi waja wa Mungu! Wako wapi ambao walipewa umri mrefu na kuneemeshwa! Walijulishwa na wakafahamu, na walipewa muda na wakaupoteza bure[2], walikuwa salama na wakasahau, walipewa muda mrefu wa maisha, waliumbwa kwa sura nzuri, walitahadharishwa machungu, waliahidiwa makubwa! Jihadharini na dhambi zinazoangamiza, na aibu zikasirishazo.

Enyi wenye macho na masikio na afya na mali! Je kuna upenyo! Au epuko, au kimbilio, au marejeo (yaani kurejea hapa duniani) au hapana? "Basi mpaka lini mwaibadilisha haki kwa batili?" (6:95) "Vipi mwaondolewa mbali na ibada ya Mwenyezi Mungu." (40:62)

Au mwaghurika na nini! Hali ikiwa mmoja wenu hisa yake ya ardhi yenye urefu na upana ni kadiri ya urefu wake, mwenye kugusishwa shavu lake na mchanga (yaani maiti azikwapo ni sunna shavu lake ligusishwe mchanga kwa kuiondoa sanda aliyovikwa eneo la shavu lake).

Enyi waja wa Mungu! ni hivi sasa hali kamba haijakaza shingoni[3], na roho zimeachwa katika wakati wa kutaka mwongozo, hali miili iko na raha, na ukumbi wa kujikusanya[4], na muda wa maisha upo na mwanzo wa muda wa utashi[5],49 kuna nafasi ya kufanya toba, na nafasi ya wakati wa haja kabla ya shida, dhiki, hofu, na kubanwa, na kabla ya kuja mauti yanayongojewa na kabla ya shiko la Mwenye nguvu Muweza (s.w.t).".

1. Akusudia machungu makubwa, na kila aina ya mateso miongoni mwa mateso ya adhabu, ni kama mauti kwa shida yake.

2. Walipewa muda wakahadaika na kuacha kutenda mema, na hiyo baada ya kuwa walijulishwa na kufahamu, na ilikuwa kwa muktadha wa kufahamu wasingedanganyika na muda na kuipoteza fursa!

3. Yaani fanyeni mema hivi sasa mkiwa huru, mnao uwezo, kamba haijakazwa shingoni mwenu, na roho zenu hazijakamatwa.

4. Ukumbi wa kujikusanya: Yaani, ninyi mpo katika uwanda ambao inakuwieni rahisi humo kushirikiana katika mema ninyi kwa ninyi.

5. Ni mwanzo wa wakati wa azma ya kufanya jambo na kuchagua, lau kama mngepen- da kuanza tena utashi na azma ya kufanya mema mngeweza.

# NAHJUL BALAGHA

## JUZUU YA PILI

### MTARJUMI: HARUNA PINGILI

## 84 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

### KATIKA KUMUELEZEA AMRU IBNUL-A’AS

“Namshangaa ibn An-Nabighah! eti asema akiwa kati ya watu wa Syria (Sham) kuwa mimi ni mtu wa mzaha, na kuwa mimi ni mtu wa mchezo mwingi, najishughulisha na mieleka na kupigana na watu. Amesema batili na ametamka akiwa na dhambi.

Angalieni, (maneno ya uovu mno ni uwongo) naye yuasema na yuadanganya, anaahidi na yuaenda kinyume, anaomba kwa kung’ang’ania[1] na akiombwa yuafanya ubakhili, anavunja ahadi, na anaukata udugu. Awapo vitani yeye ni mkemeaji na muamrishaji!.

Hapo ni ikiwa panga hazijachukua nafasi yake, na zikichukua nafasi yake, ujanja wake mkubwa ni kuwaonyesha maadui zake utupu wake. Ama mimi wallahi kukumbuka mauti kwanizuia kufanya mzaha, na kwa kweli yeye kimzuiacho kusema kweli ni kuisahau akhera, kwa hakika yeye hakumpa bai’a Muawiya mpaka alipompa sharti ya kupewa kitu.[2]”.

## 85 - MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

Miongoni Mwa Khutba Zake (a.s) - al-Wasitiy ameitaja katika Uyunul-Hikami wal Mawa’idhy, na Ibn Sibt Jauziy katika Tadhkiratul-Khawa’is uk. 131.

### KATIKA KUMWADHIMISHA MWENYEZI MUNGU NA KUMTUKUZA

“Na ninashuhudia kuwa hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah swt. peke Yake, hana mshirika, ni wa milele (bila mwanzo) alikuwa yupo wakati hapakuwa na kitu kingine, na ataendelea kuwepo baada ya kutoweka kwa kila kitu, Yeye hana kikomo. Dhana haiambui kumpata na sifa, wala nyoyo haziwezi kumuelewa kwa aina, wala hapatwi na ufanywaji wa sehemu sehemu wala kufanywa kwa mfano kwamba hii ni baadhi ya sehemu ya Mungu. Hazungukwi na uoni wa macho na wa nyoyo.[3]”.

### NA SEHEMU YAKE NYINGINE (YA KHUTBA) KUIELEZEA PEPO

---

1. Anaomba na yuafanya ilhafu, kuomba kwa ilhafu ni kung’ang’a- nia kuomba. Mungu (s.w.t) amesema: “hawang’ang’anii watu wakiwaomba” (2:273).

2. Na makusudi ya chochote kitu hapa alichokuwa akitaka apewe ni kumfanya awe gavana wa Misri.

3. Katika mlango huu, pamoja na ufupi wake, kuna mas’ala manane miongoni mwa mas’ala za Tawhiid: Ya kwanza: Ni kuwa hakuna wa pili yake (s.w.t) katika Uungu. Pili: Yeye ni wa milele yote tangu na tangu hana mwanzo wala mwisho. Tatu: Yeye ni Abadiyu: yaani dhati yake haina mwisho. Nne: kumkanushia sifa. Tano: kumkanushia jinsi. Sita: kuwa Yeye (s.w.t) hagawanyiki, kwa kuwa Yeye sio mwili wala sio kiumbe ambacho si mwili kama vile uzito, na wepesi. Saba: Kuwa Yeye haonwi wala haipiti katika akili ya mtu kuwa yuko hivi. Nane: Dhati yake haijulikani.

"Tabaka zinazo zidiana, na daraja zinazo tafautiana, neema zake hazikati- ki, atakayedumu humo hatozeeka, wala mkazi wake hatokuwa fakiri.".

## 86 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Khutba Zake (a.s) - Ad-Dainuriy ameitaja katika al-Akhbar at-Twiwalu uk. 145; na ibn Shu'ba katika Tuhaful- Uqul uk. 100, na al-Barqi katika al-Mahasimu uk. 233.

### KUHUSU WAADHI WA KUJIANDAA KWA AJILI YA ULIMWENGU MWINGINE NA KUFUATA AMRI ZA MUNGU

"Amezijua siri, na habari ndani ya dhamiri, yuakizunguka kila kitu, na mwenye kukishinda kila kitu, na mwenye nguvu juu ya kila kitu. Basi mtendaji miongoni mwenu na atende ndani ya muda wa (uhai) wake kabla ya kukabiliwa na ajali yake. Na atende wakati wa wasaa kabla ya kushughulishwa kwake, na wakati wa nafasi yake kabla hajashikwa koo[1].

Ajiandae kwa ajili ya nafsi yake na safari yake, na aandae masurufu kutoka kwenye nyumba ya kituo chake (cha muda) kwa ajili ya nyumba ya kudumu kwake.

Mkumbukeni Mungu swt. enyi watu, kwa aliyokutakeni ndani ya Kitabu chake kuyazingatia, na haki Zake alizozihifadhi humo, kwa kuwa Mungu (s.w.t) hajakuumbeni bure, na wala hajawaacheni bila ya faida, wala hajawaacha katika ujinga wala upofu. Amepandisha daraja ya athari zenu, na amejua amali zenu, na ameamua ajali zenu.

Na amekuteremshieni Kitabu kinachobainisha kila kitu, na amemrefushia umri nabii Wake kwa zama ndefu, kiasi cha kumkamilishia yeye na ninyi ujumbe - aliouteremsha Kitabuni mwake - ambao ni dini Yake ambayo ameiridhia nafsini Mwake; na amebainisha kwenu - kupitia ulimi wake - matendo mema na mabaya, makatazo Yake na amri Zake, na ameweka mbele yenu hoja Yake na kuondoa udhuru kwenu, amekukemeeni na kuwaonya na adhabu kali. Hivyo basi zidirikini siku zenu zilizobaki, na zifanyeni nafsi zenu zivumilie humo. Kwa kuwa ni chache katika siku nyingi ambazo mnakuwa katika mghafala, na kutotilia manani mawaidha, msiuachie muda, utawawekeni katika njia ya madhalimu, na msijipendekeze, kwa kuwa kujipendekeza kutawasukumeni kwenye maasi.

Enyi waja wa Mungu! Kwa kweli mnasihi mzuri mno wa nafsi yake katika watu ni yule mtii mno wa Mola Wake[2]; Na kwa kweli mwenye kuighushi mno nafsi yake ni muasi sana wa Mola Wake[3]; na mwenye kupunjwa ni yule

---

1. Kushikwa koo: Ni kinaya - yaani kule kubanwa wakati wa kuifariki dunia.

2. Kwa kuwa yeye ameihifadhi isiadhibiwe, na kuiwajibishia thawabu, na huo ndio upeo wa nasaha.

3. Mwenye kuighushi mno nafsi yake kati ya watu ni yule muasi mno kwa Mola Wake kwa kuwa yeye ameitumbukiza katika maangamizi ya daima, na huo ni upeo uwezekanao wa kuighushi na kuidhuru nafsi.

ambaye ameipunja nafsi yake, na mwenye kutamani mfano wa hali ileile[1] ni yule ambaye dini yake iko salama, na mwenye furaha ni mweye kuwaidhika na mtu mwingine, na dhalili ni mwenye kuhadaika na utashi wa nafsi yake na kughurika kwake. Jueni kwamba kuwepo kwa kiasi kidogo cha riya'a[2] - ni ushirikina, na kukaa na watu wanaofuata matamanio ya nafsi zao - hawaa - yaliyoko nje ya maadili ya kisharia - kunasahaulisha imani, na ni mahudhurio ya Shetani.

Jiepusheni na uwongo, kwa kuwa ukando na imani. Mkweli yu ukingoni mwa wokovu na heshima, na muongo yuko katika kilele cha kuanguka na kudharauliwa. Msihusudiane, kwa kuwa husuda huila imani kama moto ulavyo kuni.

Msibughudhiane, kwa kuwa huko ni kwenye kufuta imani[3]; na jueni kwa mba kuwa na matumaini mno - kunaisahaulisha akili na kumbukumbu[4]. Basi yakidhibisheni matumaini kwa kuwa ni ghururi, na mwenye nayo ameghurika."

## 87 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Khutba Zake (a.s) - Zamakhshari ameieleza katika Rabiul-Abrar mlango wa al-izzu
wa sharaf.

### KUHUSU AMPENDAYE MUNGU MTUKUFU

"Enyi waja wa Mungu! Kwa kweli miongoni mwa waja wapendwao mno na Mungu ni mja ambaye Mungu amemsaidia kupambana na nafsi yake, akawa yuaifanya huzuni ni shi'aru yake - vazi la ndani[5], na amevaa joho la hofu, kwa hiyo taa ya mwongozo ikaangaza moyoni mwake, na aka andaa takrima kwa ajili ya siku yake atakayofikia, kwa hivyo akasogeza kwa ajili yake kilicho

1. Mwenye kutamani mfano wa hali ile ile hapa ni tafsiri ya: naye ni mtu aionaye neema kwa mwenzake naye akatamani apate neema kama ile bila ya kumtakia kinyume yule aliyetunukiwa neema hiyo.Waila itakuwa ni mwenye husuda.

2. Riya'a ni kufanya tendo la kheri ili wakuone watu kwa ajili ya sifa hali moyo wako ulikuwa haupendi kufanya, (pia yawezekana moyo ulikuwa wapenda lakini mbele ya watu ukahamasika zaidi na ukaongeza mikogo katika tendo la kheri kutaka sifa).

3. Kwenye kuifuta kila kheri na baraka. Na kwenye kung'oa ambayo huwajia kaumu kama kinyozi wa nyele.

4. Matumaini ambayo husahaulisha akili na kumkumbuka Mungu na amri zake, na makatazo yake, ni kule kutuwama nafsi pale ilipofikia, haitazamii mabadiliko ya hali ya mambo, wala haina azma katika kazi.

5. Huzuni ameifanya Shi'aru: Na shi'aru ni vazi la ndani. Kwa hiyo huzuni ameifanya kama vazi la ndani, na huzuni hapa ni uelewa wa kushindwa kutekeleza wajibu ipasavyo, nalo ni jambo la kiroho, athari yake haidhihiri kwa umbali ambao Mungu anaghadhibika, na kuharakia kutenda yanayomridhisha, na hiyo ni athari ya nje.

mbali, na akapoza makali ya shida[1], ameangalia akatambua, akakumbuka na akakithirisha[2].

Alipoza kiu kwa maji baridi aliyorahisishiwa maendeo yake, akanywa na kutosheka. Akapita njia iliyosawa, akiwa amevua vazi la matamanio, na kujiepusha na mahangaiko ya moyo, isipokuwa hangaiko moja pekee amebaki nalo[3], kwa hiyo akawa ametoka na kuwa mbali na sifa za upofu, na mbali na kushirikiana na watu wa matamanio, hivyo akawa miongoni mwa funguo za milango ya uongofu, na vifungio vya milango ya kuangamia.

Ameiona njia yake na akaipita njia hiyo, na akaijua miongozo yake, akaivuka bahari yenye maji mengi iangamizayo, na akashikamana na kishiko kwa umadhubuti, na miongoni mwa kamba iliyo ngumu mno, kwa hiyo yeye kwenye yakini yu kama mwanga wa jua, ameisimamisha nafsi yake kwa ajili ya Mungu (s.w.t) katika mambo ya hali ya juu kabisa; kwa kulikabili kila limfikalo, na kuchukua kila hatua ihitajiwayo kwa hilo, na kulirudisha kila tawi kwenye shina lake[4].

Ni taa ya giza jingi, mfichuaji wa upofu, ni ufunguo wa yaliyofumbika, mzuiaji wa shida, mwongozaji wa jangwani, akisema yuafahamisha, akinyamaza husalimika.

Amekuwa na ikhlasi kwa Mungu naye akamfanya makh'susi kwa ajili Yake, hivyo yeye ni chimbuko la dini Yake, na vigingi vya ardhi Yake. Amejiambatanisha binafsi na uadilifu, na ukawa uadilifu wake wa kwanza kujiondolea utashi wa kibinafsi.

Anaielezea haki na anaitendea kazi, haachi lengo la kheri ila atalikusudia, wala padhaniwapo kheri ila atapaendea. Amekishika Kitabu hatamu zake[5] nacho ndio kiongozi wake na Imamu wake. Anashuka pale ambapo kinapoifikisha mizigo yake[6], na anateremka mahali pake pakufikia."

---

1. Kujisogezea karibu kilicho mbali: yaani umauti udhaniwao uko mbali akausogeza karibu, kwa kutenda mema kwa ajili yake siku utakapomshukia, kwa hiyo akalegeza shida ya uvumilivu wa kuziacha ladha za mpito na kuwa makini kujipatia ubora wa juu kabisa, na hiyo ndiyo shida.

2. Amemkumbuka Mungu akakithirisha matendo mema ili kumridhisha.

3. Hangaiko moja, nalo ni la kubaki ndani ya mipaka ya kisharia.

4. Kwa kuwa ambaye kwake la muhimu ni kubakia ndani ya mipaka ya Mungu, katika amri zake na makatazo yake, uoni wake hupenya mpaka kuufikia ukweli wa siri za Mungu katika hayo na anakuwa katika daraja ya ir'fani kiasi kwamba halimfikii jambo ila atalitoa kama lilivyo, wala halimtokei tawi ila atalirudisha kwenye shina lake.

5. Kitabu ni Qur'ani, kushika hatamu zake ni tamthili, anamaanisha kuzitekeleza kwake hukumu zake, yeye anakuwa kama farasi na Kitabu kinamsukuma mahali kinapopenda.

6. Mizigo hapa yakusudiwa: amri na katazo yanayobebwa na Kitabu.

## SIFA ZA MTU FAASIQI

"Na mwingine amejiita mwanachuo hali akiwa si mwanachuo[1], amedondoa dhana za kijahili kutoka kwa majaahili, na upotovu kutoka wapotovu, na amewategea watu mtego uliotengenezwa kwa kamba ya udanganyifu, na maneno ya uwongo; anakichukuwa Kitabu-Qur'an - kwa maoni yake; na ukweli ameupindisha kulingana na utashi wake binafsi.

Anawafanya watu wajione wako salama watendapo makosa ya jinai, na hulichukua kosa kubwa kama ni kitu chepesi, anasema: 'Nasita kwenye mambo yasiyo wazi,' na humo yuajiingiza; na anasema: 'najiepusha mbali na bid'a,' na punde amejiingiza humo. Hivyo basi sura yake ni ya mtu, na moyo ni moyo wa mnyama, hajui mlango wa uongofu ili aufuate, wala mlango wa upotofu ili aufunge akiwa mbali nao, na huo ni umauti wa walio hai. "Basi mpaka lini mwaibadilisha haki kwa batili?" (6:95) "Vipi mwaondolewa mbali na ibada ya Mwenyezi Mungu." (40:62).

Na alama zipo[2], Na aya ziko wazi, na minara imesimamishwa[3],mnapotezewa wapi! na vipi mnakuwa vipovu na kati yenu kuna itrah ya Nabii wenu![4] Nao ndio hatamu za ukweli[5], na ni alama ya dini, na ndimi za ukweli! Hivyo wawekeni daraja nzuri mno ya Qur'an[6], na muwaendee mwendo wa ngamia walio na kiu[7]. "Enyi watu! Chukueni kutoka kwa Khatamun-Nabiyina - hitimisho la Manabii **(s.a.w.w)**: (Kwa hakika hufa afaye katika sisi na wala si

---

1. Huyu ni mja mwingine (mmoja katika aina nyingine ya watu) sio mja yule aliyemuelezea sifa zake zile za mwanzo, sifa za huyu zatofautiana na zake.

2. Alama hapa: ni miujiza.

3. Na minara hapa: Ile iliyosimamishwa ikiwa ni alama ya kheri na shari.

4. Itrah ya Mtume ni kizazi chake, na si kweli isemwe kuwa ni ukoo wake japo wawe wa mbali. Na Mtukufu Mtume (s.a.w.w) aliwabainisha Itrah wake ni akina nani, pale alipowafunika shuka, na akasema: 'inniy tariku fii kum athaqalayni' akasema: 'Itratiy ah'lu baytiy' na katika kikao kingine alibainisha Ahlul-Bayt wake ni nani alipowafunika shuka na akasema ilipoteremka: "innama yuriidu llahu liyudh'hiba ankumur-rijsa ah'lal'bayti." (33:33): Allahuma haulai ah'lubaytiy fadh'hib rijsa anhum, na kwa Itrah Amirul-Mu'minin alikuwa anajikusudia mwenyewe binafsi na watoto wake wawili; na asili yake kwa ukweli ni yeye mwenyewe, kwa kuwa watoto wake wamfuata yeye.

5. Ameufanya ukweli kana kwamba wazunguka pamoja na wao wanakozungukia, kama ilivyo kwa ngamia, hutii na huielekea hatamu yake inakozungukia. Na Mtume (s.a.w.w) alitoa habari ya ukweli wa kadhia hii kwa kauli yake: "na izungushe haki pamwe na yeye azungukiako".

6. Mwendo wa ngamia wenye kiu: Yaani kuweni na hima kuchukua elimu na dini kuto- ka kwao, mfano wa hima ya ngamia wenye kiu sana wayaendeapo maji. Njooni kwenye bahari ya elimu yao haraka kama waharakiavyo ngamia wenye kiu maji.

7.Wawekeni daraja nzuri mno ya Qur'ani chini yake kuna siri kubwa, na hivyo ni kuwa yeye amewaamuru mukalafeena waipitishe Itrah katika kuitukuza, kuiadhimu na kuongoka na mwongozo wao, na utii wa amri yao kwa mwendo wa Qur'ani, anasema: iwekeni Itrah ya Nabii mioyoni mwenu mahala pa Qur'ani kwa kuiadhimu, kuitukuza na kuiheshimu, na kwa kweli moyo ni mahali pazuri pa materemkio ya Qur'ani.

mfu[1], na huoza aliyeoza katika sisi wala hakuoza) hivyo basi msiseme msiyoyatambua, kwa hakika ukweli mwingi upo katika myakanushayo[2].

Kubalini udhuru wa msiye na hoja dhidi yake - naye ndimi - je sikuifanyia kazi kwenu thiq'lu kubwa![3] Na ninaiacha kwenu thiq'lu ndogo? Na nikasimika katika nyinyi bendera ya imani, na nimekusimasheni kwenye mipaka ya halali na haramu, na nikakuvisheni afya kutokana na uadilifu wangu, na nimekukukunjulieni mema kwa kauli yangu na vitendo vyangu, na nimekuonyesheni tabia njema za hali ya juu kutoka kwangu mimi mwenyewe binafsi. Hivyo msitumie rai katika ambayo hakifikiwi kina chake na macho, wala fikra haziingii.[4]"

Na Sehemu Ya Khutba Hii Kuwahusu Bani Umayyah:

"Mpaka atadhania mwenye kudhani kuwa dunia imefungwa aqal, kwa Bani Umayyah, yawapa kheri zake[5], na kuwaongoza kwenye chemchemi safi za manyweo yake, na wala ummah huu hautaondolewa mjeledi wala upanga wake, na atakuwa ameongopa adhaniaye hivyo. Bali hilo ni tone la maisha ya ladha[6] (watalila kwa muda kisha watalitema lote).".

## 88 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Khutba Zake (a.s) - al-Kailaniy ameieleza katika ar-Raudhwa uk.62, na Sheikh al-Mufiidu katika ar-Rishadu uk.173, na Ibn Athir amezitafsiri (hadith) ghariib katika an-Nihaya mada ya Azalu.

1. Mwendo wa ngamia wenye kiu: Yaani kuweni na hima kuchukua elimu na dini kuto- ka kwao, mfano wa hima ya ngamia wenye kiu sana wayaendeapo maji. Njooni kwenye bahari ya elimu yao haraka kama waharakiavyo ngamia wenye kiu maji.

2. Ichukueni kadhia hii kutoka kwake, nayo ni: Mtu hufa kutoka miongoni mwa Ahlul'Bayti naye kiukweli si mfu, kwa sababu ya kubakia roho yake yamwetuka nuru kati- ka ulimwengu wa dhahiri.

3. Mjinga huufunika ukweli na kuukanusha, na kwa hakika kweli nyingi ziko kwenye kina cha ndani zaidi.

4. Thiq'lu hapa ni kitu chochote cha thamani kubwa, na limekuja neno hili katika hadi- ithi kutoka kwa Nabii (s.a.w.w) alisema: Nimekuachieni vya thamani viwili, Kitabu cha Mungu na Itrah yangu, yaani vyenye thamani viwili. Na Amirul-Mu'minina ameitendea kazi thiq'lu kubwa nayo ni Qur'ani na ataiacha thiq'lu ndogo nayo ni watoto wake wawili. Yasemwa: kuwa Itrah yake ni mwongozo kwa watu.

5. Yawapa kheri zake: Yaani ameijaalia dunia kama ngamia aliyefungwa kwa ajili yao, ni kwa wao tu, ametiishwa kwa ajili yao, kana kwamba wao wamemfunga kwa aqal anawap- atia kheri yake, yaani anawapatia maziwa yake.

6. Funda la maisha ya ladha: funda ni kiasi cha ujazo wa maji mdomoni kwa mara moja, mtu huyasukutuwa na haraka anayatema, huo ni mfano, na hapa imetafsiriwa kwa maana ya tone la asali limekuwa midomoni mwao kama linavyokuwa mdomoni mwa nyuki, wataionja kwa muda kisha wataitema. Kwa hiyo ni mfano wa maisha ya raha waliyopewa Bani Umayyah, ni mfano wa tone la asali limekuwa midomoni mwao kama linavyo kuwa kinywani mwa nyuki, wanalionja (utamu wake) muda, kisha wanalitema.

## KATIKA KUELEZEA MAKOSA WALIYONAYO WATU

“Amma ba’ad. Kwa kweli Mungu hakupata kumuangamiza dhalimu wa zama fulani katu isipokuwa baada ya kumpa fursa na raha, wala hakuuganga mfupa wa yeyote katika wana umma isipokuwa baada ya dhiki na shida, na hakuwakabili kwa misiba na shida juu yao hata kwa kiasi kidogo kuliko ambacho kitawafikeni au tayari kimewafikeni, kinatosha kuwa somo. Wala sio kila mwenye moyo ni mwerevu, wala sio kila sikio ni sikivu, wala sio kila aangaliaye ni mwenye kuona.

Ajabu ilioje! Nitakuwaje nisistaajabishwe na makosa ya vikundi hivi kwa tafauti za hoja zao katika dini yao! Hawafuati athari ya Nabii (wao) wala hawaongoki na matendo ya waswii, wala hawaamini ghaibu, wala hawajiepushi na jambo la aibu, wanatenda katika mambo yanayoshakiwa, na wanakwenda na matamanio.

Kwa wao jema ni lile wanalolipenda wao, na ovu kwao ni walikataalo[1], kimbilio lao katika matatizo ni kwao wenyewe binafsi, mategemeo yao katika mambo yanayoshakiwa ni rai zao. Kama kwamba kila mmoja ni imamu wa nafsi yake[2], amejiamulia ayadhaniayo kuwa ndiyo tegemeo, na ni sababu thabiti.”.

---

1. Yaani waliona zuri walipendalo, na kuliona baya waonalo binafsi kuwa baya, bila ya kurejea kwenye dalili iliyo bayana, au kwenye sharia iliyo wazi, kila mmoja wao anajiamini kwa mawazo ya binafsi, kana kwamba ameshika kishiko madhubuti, kwa ule ujinga na kasoro walizonazo.

2. Kana kwamba kila mmoja kati yao ni Imamu mwenyewe binafsi, yaani kuwa wao hawachukui shauri kwa mwanachuoni, wala hawamuulizi mjuzi, bali kimbilio lao pindi yatokeapo mambo yenye mushkili ni kwao wenyewe binafsi na rai za kibinafsi. Na hii ni sifa ya anayejigamba kuwa ameelimika na kuwa yu mbora.

# NAHJUL BALAGHA

## JUZUU YA PILI

### MTARJUMI: HARUNA PINGILI

## 89 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Khutba Zake (a.s) - al-Qummiy ameisema katika Tafsiir yake uk. 3, na al-Kailaniy katka Usuli, uk. 69.

### AZIELEZEA HALI ZA WATU WALIVYOKUWA KABLA YA BI'ITHA:

"Amemtuma wakati wa mwanya baada ya mitume[1], na usingizi mrefu kati ya umma, na kukithiri kwa fitna, na kuenea kwa mambo, na kulipuka kwa vita, na dunia imetoweka nuru, ghururi imejitokeza; wakati jini lake limekuwa manjano, na kukatishwa tamaa na matunda yake[2].

Na kutoweka maji yake, minara ya uongofu imefutika, na zimejitokeza alama za kuangamiza, na zimefinya nyuso zao[3], mwenye kukunja uso mbele ya mwombaji wake, tunda lake ni fitna, na chakula chake ni mzoga[4], na nguo yake ya ndani ni woga, na nguo yake ya juu ni upanga[5],hivyo zingatieni enyi waja wa Mungu, na (ikumbukeni ile)[6]ambayo baba zenu na ndugu zenu wako rehani[7], kulingana nayo watahesabiwa. Kwa umri wangu, muda wenu haujapishana sana na wao, wala haijapita kati yenu na wao miaka wala ummah, wala ninyi hii leo na siku mlizokuwa migongoni mwao sio mbali.

Wallahi Nabii hakuwasemesha kitu ila hii leo na mimi ni mwenye kuwasemesha nacho, na ambalo mmelisikia leo haliko tafauti na walilo sikia

---

1. Ni muda wa kukatika kwa risala na wah'yi, na ilikuwa kati ya Muhammad (s.a.w.w) na wakati wa zama za Masihi (a.s) ni muda mrefu. Waliowengi miongoni mwa watu wanasema ni miaka mia sita.

2. Neno hilo na la baada yake ni methali ya kugeuka kwa dunia na kuwa i karibu na kutoweka, na watu kukatishwa tamaa na starehe yake zama za jahilia.

3. Ufinyaji wa nyuso: Yaani mtu alipokeapo jambo asilolipenda sura yake huwa imekunjamana.

4. Yaani haina natija isipokuwa fitna, chakula chake ni mzoga: yaani chakula cha zama za jahiliya ni mzoga kwa sababu ya kudharurika sana, au ni kwa istiara, yaani chakula chake ni kibaya mno. Na kuna riwaya yasema: "chakula chao ni hofu".

5. Ameifanya hofu na upanga kuwa ni shiaru na ditharu, yaani nguo ya ndani na ya nje, kwa hiyo shiaru ni ile inayoambatana na mwili na dithari huja juu yake, kwa hiyo ameifanya hofu kuwa nguo yake ya ndani kwa sababu ni ya karibu mno na mwili, na kuifanya nguo ile ya juu inaifuata ya ndani, hivyo basi hofu iko ndani na upanga upo nje waziwazi. Na haya ni maneno safi mno.

6. Yaani ikumbukeni dunia, au amana aliobebeshwa mwanadamu na akaibeba, au ni ishara ya matendo maovu, na itikadi batili na matokeo mabaya.

7. Wako rehani yaani wamewekwa mahabusi kwa matokeo yake duniani kama vile udhalili na unyonge.

jana. Macho hayakuwa wazi kwao, na mioyo iliyokuwa kwa ajili yao wakati ule, ni sawa na ile mliyo nayo hivi sasa.

Wallahi hamkuwa mmeambiwa chochote baada yao ambacho hawakuwa wanakijuwa, na hamkupewa chochote ambacho wao walinyimwa, na kwa kweli balaa imewashukieni[1], inayumba hatamu yake, kamba yake iliyolegea. Isi kughurini hali waliyo nayo watu walioghurika, kwani hicho ni kivuli kilichopanuka mpaka muda uliopangwa[2].

## 90 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Khutba Zake (a.s) - al-Wasiti ameisema katika Uyunul-Hikami, na al-Aamidi katika Ghuraru-Hikami uk. 185, na Ibn al-Athir katika an-Nihaya, Jalada la 2, uk. 345.

### KUHUSU BAADHI YA SIFA ZA VIUMBE

"Shukrani ni zake Mungu (s.w.t) aliye maarufu bila ya kuonwa, na ambaye ni muumba bila ya kufikiri[3],na ambaye hakukosa kuwapo yu thabiti daima[4]; pindi hapakuwa na mbingu zenye njia kuu za sayari (zodiac), wala pazia zenye vifungo vikubwa vya fahari[5], wala usiku wenye giza, wala bahari tulivu, wala jabali lenye njia, wala njia yenye kupinda pinda, wala ardhi yenye tandiko, wala viumbe wenye nguvu na kutenda kwa makusudi na utashi, Yeye ndiye mwenye kubuni uumbaji na mwenye kubaki baada yao, Mungu wa uumbaji na mtoaji wa riziki.

Jua na Mwezi vinatembea kwa uthabiti katika ridhaa Yake. Vinakifanya kikuukuu kila kipya, na kila kilicho mbali vinakisogeza karibu.

"Amezigawa riziki zao, na amedhibiti kwa idadi athari zao[6], na amali zao, idadi ya pumzi zao, na ishara za kukonyeza kwao, na ambayo yafichwa na

---

1. Yaani mtihani mkubwa, alikusudia fitna ya Muawiyah na Bani Umayyah.

2. Kwa kweli hicho ni kivuli kilichopanuka, mpaka muda uliowekwa: Ameyafanya walio kuwa nayo walio ghurika mfano wa kivuli kwa kuwa yametulia katika muono wa jicho hali yakiwa katika hali ya haraka katika ukweli wake, yaendelea kupungua, kwa hivyo yashabihiyana na dunia.

3. Yaani Yeye (s.w.t) hutambulika bila ya macho kujiangika kwenye dhati yake na hayawezi, kwani asema (s.w.t): "Hafikiwi na uoni wa macho wala wa fikra" na yu aumba bila ya kuchemsha bongo au kuwa na ramani ya kumwongoza.

4.Thabiti daima: Linatokana na al-Qa'imu al-Qayumu: Aliye thabiti ambaye hatoweki, na limetafsiriwa kutokana na maana ya kauli yao: 'Fulanun Qa'imun bi amri kadhaa,' yaani fulani ni mwenye kulitawalia na kulishika lisiyumbe.

5. Anakusudia kwa neno pazia zenye nguzo, ni pazia za nuru zilizowekwa kati ya Ar'shi Yake tukufu na malaika wake; na yawezekana akawa yuakusudia hujubu mbingu zenyewe; kwa sababu zimekuwa hijabu dhidi ya Shetani wasijue waliyonayo malaika.
Yawezekana ikakusudiwa athari zao, athari za kukanyaga kwao ardhini, au harakati zao na matendo yao.

6. Yawezekana ikakusudiwa athari zao, athari za kukanyaga kwao ardhini, au harakati zao na matendo yao.

vifua vyao miongoni mwa dhamiri[1],Anajua makazi yao ya muda, na mahali pa makazi yao ya kudumu, hali wakiwa katika matumbo ya uzazi na migongoni[2],mpaka wafikiapo mwisho wao.

"Yeye ndiye ambaye adhabu Yake itakuja kuwa kali kwa maadui zake japokuwa huruma Zake ni zakutosha. Na rehema Zake zimewaenea wapenzi wake japokuwa adhabu Yake ni kali. Humdhibiti anayekusudia kumshinda Yeye.

Muangamizaji wa anayempinga, na humdhalilisha amuendae kinyume, mshindi wa amwendeaye kwa uadui. Humtosheleza amtegemeaye, na mwenye kumuomba humpa, na mwenye kumkopesha anamlipa[3], Na mwenye kumshukuru humlipa.

Enyi waja wa Mungu! Jipimeni wenyewe kabla hamjapimwa, na jihesabuni kabla hamjahesabiwa, na pumuweni kabla ya koo halijasonga. Ongokeni kabla ya kusukumwa kwa nguvu[4].

Na jueni kuwa asiyesaidiwa na nafsi yake kiasi cha kuwaidhika nayo na kuwa mwenye kujikemea, hatowaidhika kutoka kwa mwingine, si mkemeaji wala si muwaidhi.[5]".

## 91 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Khutba Zake (a.s) - Ibn Abd-Rabi ameitaja katika al-Iqdul-Farid, jalada la pili, uk. 406, na al-Saduq katika at-Tawhiid, uk. 34.

## IJULIKANAYO KUWA NI KHUTBA YA AL'ASH'BAAHU, NAYO NI MIONGONI MWA KHUTBA TUKUFU MNO:

Al'ash'baahu: Al'ash'khaasu ni watu, na waliokusudiwa hapa ni malaika, kwa sababu khutba ndanimwe muna utajo wa malaika.

Mas'adah bin Sadaqah ameeleza akinukuu kutoka kwa as-Sadiq Ja'far bin Muhammad (a.s), kuwa yeye alisema: Amirul'mu'minina (a.s) aliitoa khutba hii juu ya mimbari ya (mji wa) Kufa hivyo ni kwa sababu mtu mmoja alimjia na akamwambia: 'Ewe Amirul-Mu'minin! Tusifie Mola wetu iwe kama twamuona bayana ili tuzidi upendo na kumtambua.'

---

1. Ni ufafanuzi wa yafichwayo na vifua, na hiyo ni yenye kufichika mno kuliko ishara ya konyezo za jicho.

2. Anajua makazi yao, makazi hapa ni tafsiri ya neno 'Mustaru': yakusudiwa katika tumbo za uzazi. Na 'Mustaudau': Yaani katika migongo. Na yawezekana ikasemwa: Alikusudia 'Mustaruhum wa maawahum,' - juu ya mgongo wa ardhi, na 'Mustaudauhum' yaani ndani ya tumbo la ardhi baada ya umauti, na 'Al-Arham wa dhuhuur' matumbo na migongo: yaani ndanimwe.

3. Amejaalia kutanguliza matendo mema kupo katika daraja sawa na kukopesha, na thawabu ni sawa na kulipa deni, ili kudhihirisha kuwa malipo ya matendo mema yamethibiti; Amesema Mungu (s.w.t) "Ni nani atakayemkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema, ili amzidishie mzidisho mwingi?" (2:245).

4. Yaani ongokeni kuyaelekea mnayotakiwa kuyafanya mkihimizwa kwa upole kabla hamjasukumwa kwa nguvu na ukali.

5. Yaani ambaye Mungu hakumsaidia kuonyeka na kujirudi yeye mwenyewe, uzinduzi wa mtu mwingine hautomnufaisha kitu.

Hapo alighad- hibika (a.s) na akanadi: ‘Asalaatu jaamia,’ Hivyo watu walijumuika kwake kiasi cha kuwa msikiti ulijaa watu, hapo basi (a.s) alipanda mimbari akiwa ameghadhibika, rangi imembadilika, alimuhimidi Mungu na kumsifu na alimsalia Nabii sala llahu alayhi wa Aalihi, kisha akasema:

“Alhamdu-lillahi - utukufu ni wake Mungu ambaye kuzuia na ubahili hakumzidishii utajiri, wala kutoa na ukarimu hakumfanyi kuwa fakiri, kwa kuwa kila mtoaji asiye kuwa yeye ni mwenye kupungukiwa, na kila mzuia- ji ni mlaumiwa mbali na yeye[1].

Na yeye ni mtoaji sana wa faida za neema, na rejea za ziada na mgawanyo. Wamtegemeao ni viumbe, amechukua dhamana ya riziki zao, na amekadiria vyakula vyao, na amefanya njia kwa wapendao kuziendea, na kwa watakao yaliyo kwake, wala si mkarimu sana kwa aliloombwa kulinganisha na asiloombwa[2]. Ni wa Mwanzo ambaye hapakuwa na wa kabla hata iwe kabla yake kulikuwa na kitu, na ni wa Mwisho ambaye hana wa mwisho baada yake hata iwe kuna kitu baada yake, ni Mwenye kuizuia mboni ya jicho isiambue kitu Kwake au kumdiriki, Kwake hazibadililki zama kiasi cha kumfanya Yeye abadilike hali, au awe mahali ili iwe jaizu Kwake kugura.

“Lau angetoa ambavyo madini ya milima imevipumua[3], Na zimemchekelea chaza za bahari mfano wa dhahabu, fedha, na madini ya fedha ya aina makhsusi, na dhahabu iliyo halisi, na mtawanyiko wa lulu na mavuno ya marijani. Hilo lisingeathiri kitu katika ukarimu wake, wala usingekwisha wingi wa aliyonayo, na Kwake kungekuwa hazina ya wanyama ambayo isiyomalizwa na mahitaji ya viumbe, kwa kuwa Yeye ni Mpaji ambaye hamalizwi na ombi la waombaji, wala kunga’ng’ania kwa waombaji hakumfanyi awe bakhili.

“Basi ewe muulizaji, zile ambazo Qur’ani imekujulisha katika sifa Zake msifu nazo na faidika na mwanga wa mwongozo wake, na elimu ambayo Shetani amekutwisha nayo ambayo haiko Kitabuni wajibu wake juu yako, wala ndani ya Sunna ya Nabii **(s.a.w.w)** wala athari ya Maimamu waongofu, iwakilishe elimu yake kwa Mungu (s.w.t), kwa kuwa huo ni mwisho wa haki ya Mungu kwako.

Na tambua kuwa waliojikita katika elimu ndio ambao Mungu amewatosheleza kwa kutoivamia milango iliyofungiwa ya yasiyojulikana. Kukiri jumla ya wasioyajua ni tafsiri ya ghaibu iliyofichikana, Mungu

---

1. Hivyo ni kwa sababu Mungu (s.w.t) humzuia ambaye hikma na mas’laha vyaelekeza anyimwe mwenye kunyimwa, si kama wazuiavyo wanadamu.

2. Yaani ukarimu wa muumba sio kama ule uliopo katika njia ya wanadamu, ambao wanatikiswa na ombi, bali ukarimu wake ni wa jumla katika hali zote.

3. Ambavyo madini ya milima imevipumua ni istiara, yaani ilivyotoa inakuwa kana kwamba mnyama apumuapo hutoka kifuani mwake na mapafu yake hewa. Imam hapo ame- tumia balagha ya hali ya juu kwa kuuita utokaji wa madini nje ya johari zake kuwa ni tana- fusan - kupumua, kwani aghlabu huwa hivyo – bali karibu mara zote - kutokana na mtik- isiko wa maada zinazowaka ndani ya ardhi na kutoka nje, nazo zikiwa katika hali ya kufanya mvuke zinashabihiana na - tanafusi - kutoa pumzi, kama alipotumia badi’iu katika kuita ufungukaji wa chaza na kukitoa kilicho ndanimwe kuwa ni kucheka.

akawasifu kutambua kwao kushindwa kuyapata wasiyo yazunguka elimu yake.
Amekuita kuacha kuzama katika wasiyokalifishwa kutafuta kumjua alivyo kuwa ni kuimarika, hivyo basi tosheka na hayo, usiupime utukufu wa Mwenyezi Mungu (s.w.t) kwa kipimo cha akili yako utakuwa miongoni mwa wenye kuhiliki.
"Naye ni Muweza ambaye endapo fikra zimekwenda ili ziudiriki mwisho wa uwezo wake, na fikra zilizoepushwa na hatari ya wasiwasi zikajaribu kutaka kuiona hakika ya dhati Yake, na nyoyo kuwa na shauku ya kutam- bua hakika ya sifa Zake, na maingilio ya akili kuwa mazito, kwa kuwa sifa hazimfikishi ili kuipata hakika ya dhati Yake, anazirudisha nyuma. Na zitarudi hali zimeshindwa, hali zikitambua kuwa uhakika wa ilimu yake hauwezi kufahamika kwa njia iliyopotoka, wala hauingii akilini mwa wanafikra fikra yeyote, katika kukadiria ukubwa wa utukufu Wake."

## KUUMBA ULIMWENGU

"Ambaye amebuni viumbe bila ya mfano aliofananisha[1], wala hakuchukua kipimo na kulinganisha kutoka kwa muumba muabudiwa aliyekuwa kabla yake, na akatuonesha milki ya uwezo Wake, na ajabu zili- zotamkwa na athari ya hekima Yake. Na kwa viumbe wote kutambua kuwa ni wahitaji (hawana) ila awashike kwa nguvu Zake. Jambo ambalo limetufanya tumjue ni kuthibiti hoja ya dhahiri kwetu (dhidi yetu) na dalili ya kumtambua, japo viwe viumbe visivyosema.
Hivyo basi hoja yake ni kwa mazingatio yatamkayo, na dalili yake kwa muumba ipo wazi[2].
"Hivyo basi nashuhudia kuwa mwenye kukushabihisha na mtengano wa viungo vya miili ya viumbe Wako, na kushikana ncha za mifupa yao iliyositiriwa ili kuizingatia hekima Yako, dhamira yake haijawa na maari- fa ya kukutambua Wewe, na wala moyo wake haujagusa yakini kuwa hauna kifani, kana kwamba hakusikia kujitakasa kwa wafuasi mbali na wenye kufuatwa watakapokuja kusema: 'Wallahi! Kwa yakini tulikuwa katika upotovu ulio bayana. Tulipokuwa tunakufanyeni ni sawa na Mola Mlezi wa walimwengu wote!' (26:96-97)*
"Wamedanganya wanaokulinganisha, walipokushabihisha na sanamu zao, na wakakupamba na mapambo ya viumbe kwa dhana zao, na wakakufanya (uko) sehemu sehemu ufanywaji sehemu wa vitu vyenye miili kwa fikra zao, na wakakulinganisha na viumbwa vyenye kutofautiana nguvu kwa uwezo wa

1. Kauli yake Ib'tada'al'khalqa: Amewabuni viumbe bila kuwepo na kitu, na kauli yake: "Ala ghayri mithaalin imtathalahu" (bila ya mfano alioiga) yawezekana awe amekusudia kwa neno: Imtathalahu mathalahu, na maana inakuwa Yeye (s.w.t) hakujiwekea mfano kabla hajaanza uumbaji (kama vile ramani) wa ulimwengu; kisha iwe amefuata katika uumbaji ule mfano, na yawezekana awe amekusudia kwa neno: Imtathalahu kuwa amefuata nyayo na kuiga, na maana inakuwa: Yeye (s.w.t) hakufanyiwa mfano na mtendaji mwingine kabla yake naye akamuiga na kufuata nyayo na kufanya kama alivyofanya.

2. Na amejaalia haja ya wazi wazi kwa viumbe ili kuweka kuwepo kwao kwa kiwashika- cho miongoni mwa nguvu Zake kama mfano wa mtamkaji wa utambuzi huo wa kumtam- bua Yeye, yaani ametujulisha kumtambua Yeye kwa sababu kuwepo kwa hoja kumetulaz- imisha hivyo.

fikra ya akili zao. Na ninashuhudia kuwa mwenye kukufanya uko sawa na kitu chochote katika viumbe wako anakuwa amekufanyia mfano, na mwenye kukufanyia mfano ni kafiri wa yaliyoteremka miongoni mwa aya Zako za wazi na kuelekezwa na ushuhuda wa hoja Zako zilizo bayana, (pia nashuhudia) kuwa Wewe ni Mungu haujafungwa kwenye mabano ya akili ili uwe kwenye mwelekeo wa kifikra mwenye kugeuka geuka[1], wala katika fikra yake mwenye namna, wala si katika mawazo yake mwenye mipaka, mwenye kukubali kubadilika.

## BAADHI YA SEHEMU YA KHUTBA HII HII

Kuhusu ukamilifu mkubwa wa uumbaji Wake (s.w.t): "Miongoni mwayo: Amekadiria alivyoviumba na kuimarisha makadirio Yake, na amepanga na akaufanya mpango mzuri, na akaelekeza mwelekeo wake, wala haukuvuka mpaka wa ngazi yake, wala kuzembea kwa kutokufikia lengo lake, wala haikuona vigumu kutii utashi wake.

Na itakuwaje hali ikiwa mambo yametokea kulingana na utashi wake! Mbunifu wa sam- puli za vitu bila ya kuvuta fikra, wala kudhamiria kwa msukumo wa silka[2], wala hakufaidika na uzoefu wa matukio ya zama, wala hakusaidiwa na mshirika kubuni mambo ya ajabu, umbo lake likatimia, na kutekeleza utii wake, na kuitikia wito wake, na viumbe vikaitika wito wa muumba, kulingana na wajibu wa maumbile yake bila ya ujahili akavinyosha vitu vilivyopinda, na aliainisha mipaka yake na kwa uwezo wake ameunganisha kati ya vinavyopingana, na aliziunganisha (kamba za nafsi) na kuifarikisha jinsi tofauti katika mipaka na makadirio, silka na namna, ubunifu wa viumbe akaimarisha umbo lao, na ameviumba alivyopenda na kuvibuni."

Na Miongoni Mwayo Kuihusu Sifa Ya Mbingu

"Na amefanya mwanya (s.w.t) kati ya miili - yaani sayari za angani - moja na nyingine miongoni mwa sayari za angani na kuiweka katika nidhamu bila ya kuuangika moja na nyingine na bila ya kuifunga na ala ihisiwayo. Na amesawazisha miatuko ya mianya yake[3], na akafuma kati ya kila sayari na miili mienzake inayowiana nayo na kufanana miongoni mwa miili mingine katika tabaka la juu na chini kwa vifungo vinavyozishika (vifungo vya

---

1. Yaani Haujawa na ukomo ukiwa ndani ya mipaka kiasi cha kuzungukwa na akili kwa hali hiyo akili iko katika aina makhsusi.

2. Silka: Yaani Yeye (s.w.t) hana silka kama walivyo viumbe zenye hisia kwa mujibu wa hiyo (silka), viumbe husukumwa kutenda, bali Yeye (s.w.t) ni mtendaji kwa muktadha wa dhati Yake sio kwa msukumo wa tukio la nje.

3. Yaani ikiwa kwenye sayari moja kuna mwatuko anausawazisha (s.w.t) na kuuweka sawa na hivyo inakuwa kama ilivyokuwa mwanzo wa kuumbwa kwa ardhi na kuiengua kutoka miili ya mbinguni na kuwa na mwanya kati ya miili ya juu na hiyo (ardhi), kiwacho na mwanya katika hiyo anasawazisha (s.w.t). "Awa lam yara lladhiina kafaru annas samawati wal'ardha kaanataa rat'qan fafataqnaahuma" 'Je hawatambui waliokufuru (waabudia sanamu) wao hutofautisha kati ya kuumba na kuratibu, wananasibisha uumbaji kwa Mungu (s.w.t) na uratibu wa mambo kwa miungu - sanamu' (Al'anbiyau: 30) Kuwa mbingu na ardhi zilikuwa zimeungana mwanzo wa kuumbwa kwao naye swt. akazitenga, na hiyo ni katika tad'biiri (kuratibu, kuongoza), basi vipi yawezekana uumbaji uwe kwa mmoja na uratibu wa mambo uwe kwa wengine?!.

maanawiy, sio vya kimwili) vya mwinuko na vya bonde na akaziba mianya ya miatuko yake na amefuma (s.w.t) kati ya kila mbingu na miili yake na inayofanana nayo.
Na amerahisisha kuikurubia miinuko yake kwa (malaika) wateremkao na amri yake, na kwa wapandao wakiwa na amali za viumbe Wake. Mgumu upandaji wake.
Aliziita hali zikiwa bado mvuke ulio bayana[1], mara moja viungo vyake viliungana na aliifungua milango yake hali ilikuwa imefungwa, na aliweka walinzi wa angani[2] yaani vijinga vipenyavyo kwenye njia zake, na akazishika zisiyumbe katika mapito ya upepo kwa mkono (uwezo) wake.
Na akaiamuru isimame kusalimu amri Yake, na amejaalia jua kuwa ni alama yenye kuangaza kwa ajili ya mchana wake, na mwezi ni alama yenye kufutwa katika baadhi ya usiku[3]. Na akazipitisha sayari mbili (jua na mwezi) kwenye mzunguko wake na akakadiria khatua za mienendo yao kwenye mapito yao, ili (kwa viwili hivi) aweze kubaini kati ya usiku na mchana na ipate kujulikana idadi ya miaka na hisabu kwa makadirio yao (jua na mwezi), kisha akaangika katika anga lake falaki (njia za sayari) na akaiambatanisha humo mapambo yake, miongoni mwa nyota zake (zajulikana kwa jina la "Duriyu") nazo ni nyota zin'gaazo sana, na taa za nyota zake (hizi ni nyota ndogo ndogo), na aliwatupia waibao usikizi vijinga vyenye mwanga upenyao, na akazipitisha kwenye njia alizoziweka sawa kwa ajili ya iliyothibiti (miongoni mwa nyota zilizo thabiti mahali pamoja) na kwa ajili ya zenye kwenda kwa ziendazo (yaani tano zenye nuru, kwa kuwa daima ni zenye kwenda) kuporomoka kwao na kupanda kwao, na zile za ndege mbaya na ndege njema.[4]".

## MIONGONI MWAYO KUHUSU SIFA YA MALAIKA

Kisha (s.w.t) aliumba viumbe ili awafanye kuwa wakazi wa mbingu zake, na kuzifanya mbingu ziwe na wenyeji tabaka za juu za milki yake, viumbe wapya, nao ni miongoni mwa malaika wake, na aliwajaza maeneo ya wazi

---

1. Usemi wake: Naadaaha - aliziita, ni kurejea kwenye kubainisha baadhi ya jinsi ilivyokuwa kabla ya nidhamu. Anasema: Mbingu zilikuwa moshi unaoyumba, za shabihi- ana na moshi kwa mandhari yake, na kushabiahiana na mvuke kwa hali yake ya maada, hapo ndipo siri ya uumbaji ikajitokeza.

2. Walinzi: Ni kaumu ya wanaoangalia kama walinzi, na kuwa walinzi ni katika vimon- do mwanzo wa kuumba viumbe, ni kama alivyosema Imam (a.s) ni dalili ya ambalo lime- thibitishwa na elimu kuwa vimondo ni vyenye kupiga baadhi ya sayari.

3. Mwanga wake hufutika baadhi ya nyakati za usiku baadhi ya nyakati au usiku mzima siku nyingine.

4. Kwa kweli nyota zina athari, kupanda na kuteremka, katika mambo kwa sura ya jumla, kama kusababisha joto au baridi, au kujulisha maradhi au ukame kwa sura ya jumla, au mvua ya kudumu, na mfano wa mambo kama hayo miongoni mwa mambo ambayo hayahusiani na suala la mtu fulani peke yake. Na ambalo alilikanusha kwa aliyemshauri asiende vitani katika siku makhsusi, kwa ajili ya nyota kuwa na athari katika mambo au matukio ya watu mmoja mmoja au tukio la mtu binafsi, mfano wa safari kukaa mahali fulani, vita, amani, na mfano wake.

katika mabonde yake, na aliwajaza sehemu tupu za anga Zake, na kati ya mwanya miongoni mwa hiyo mianya kuna kelele za sauti za (malaika) wafanyao tasbiihi wakiwa ndani ya maboma matakatifu[1], na pazia za utukufu, na nyuma ya hayo kuna mtikisiko ambao masikio huziba, na tabaka za nuru zinakiwisha macho yasifike na kubaki yamezuilika kwenye mpaka wake, yaani zinapoishia nguvu zao, amewaumba wakiwa katika sura zilizo tofauti, na uwezo ulio tofauti, wenye mbawa wanautakasa utukufu wa enzi Yake, hawajidaii uungu binafsi, wala hawajigambi kuwa wanaumba kitu pamoja na Yeye miongoni mwa aliyojitenga nayo "Bali hao (wanaowaita wana) ni watumwa walitukuzwa. Hawamtangulii kwa neno, nao hufanya kwa amri Zake." 21:26-27.

"Mungu amewajaalia kuna ambao ni waaminifu kwa ajili ya wahyi Wake, na kuwatuma kwa manabii Wake wakiwa wabeba amri Zake na makatazo Yake. Amewahifadhi dhidi ya kuwa na shaka ya utata, hivyo basi hapana yeyote miongoni mwao anayepotoka kando na njia ya maridhawa Yake.

Amewapa jinsi ya kufaidika na msaada na kuzifunika nyoyo zao adabu na unyenyekevu na amani, na amewafungulia milango laini ya kumtukuza, na amewasimamishia minara ya wazi ikiwa ni alama za tauhiidi Yake, uzito wa dhambi haukuwatopea, wala kupokezana kwa usiku na mchana hakujawamaliza au kuwageuza.

Wala shaka hazijashambulia kwa mishale uimara wa imani zao, dhana hazija songamana kwenye misingi ya yakini yao, wala chuki haijawasha moto kati yao, wala mbabaiko haujawapokonya walichoambatana nacho miongoni mwa maarifa Yake kwa dhamira zao, na kilichotulia miongoni mwa utukufu Wake na haiba ya utukufu Wake ndani ya nyoyo zao, wala wasiwasi haukuwa na tamaa kwao ya kuwatandazia kutu yake kwenye fikra zao.

Miongoni mwao kuna ambao wako katika uumbaji wa mawingu mazito ya maji, na walio kwenye milima mirefu, na walio katika maficho ya giza linaloduwaza. Na miongoni mwao kuna ambao nyayo zao zimetoboa ardhi ya chini nazo zikiwa kama bendera nyeupe zilizopenya kwenye penyo za hewa na chini yake kuna upepo uliotulia yaifunga kwenye mipaka inakoishia.

Shughuli za ibada Yake zimewatenga, hakika ya imani imekuwa wasila kati yao na maarifa Yake, yakini na Yeye imewakata na kuwafikisha kuwa na shauku Naye, upendo wao kwa Aliyonayo haukuvuka na kuwafikisha kwa aliyenayo mwingine. Hakika wameonja utamu wa kumtambua Yeye, na wamekunywa kwa gilasi ipozayo kiu kwa mahaba Yake, na imekita kwenye kiini cha mioyo yao kamba ya kumkhofia.

"Wamepindisha unyofu wa migongo yao kwa sababu ya urefu wa utii. Kwa kweli urefu wa matumaini Kwake haukumaliza mada ya unyenyekevu wao, wala ukubwa wa ukaribu haujawafungua tanzi za unyenyekevu wao, wala hawakutawaliwa na fahari, kiasi cha kuwafanya wakithirishe waliyoyatanguliza miongoni mwa mema, wala unyenyekevu wao kwenye utukufu wa Allah hauwaruhusu kuthamini mema yao, hawajapitiwa na utepetevu muda wote wa kudumu kwao, raghba yao haikupungua hata

1. Boma hapa ni boma la kuwahifadhi wanyama, nalo hapa limetumika kwa majaazi (istiara) yakimaanishwa makazi matakatifu ya roho zilizo tohara.

wahalifu kumtarajia Mola wao, wala ncha za ndimi zao hazikukauka kwa urefu wa faragha[1], wala hawakukaliwa na la kuwashughulisha mbali na Mungu hata walazimike kunong'ona ili kuzipunguza sauti zao za juu kwa dua, wala mabega yao hayakutofautiana katika safu za utii, wala hawakuzipindisha shingo zao kwa raha ili kuzembea amri Yake, wala upuuzi wa mghafala haushambulii azma ya juhudi yao, wala hadaa za matamanio hazishambulii hima zao.

"Wamemfanya Mwenye Arshi kuwa ni akiba ya siku ya haja yao, na wamemkusudia Yeye kwa wayatakayo na matarajio pindi waja walipojitenga mbali na Yeye na kuwaelekea viumbe kwa wayatakayo, hawaufikii mwisho wa upeo wa ibada yake, kila wazidishapo utii wake huzidi msukumo wa kumuabudu miongoni mwa upendo na hofu.

Sababu za hofu hazijakatika mbali na wao, hata wadhoofu katika juhudi zao, wala hawakutekwa na tamaa hata watosheke na juhudi ndogo mbali na juhudi zao kubwa, hawakuuzingatia ukubwa wa amali zao zilizotangulia, lau wangezikuza hizo, matumaini yao yangefuta hali ya woga wao.

Wala hawajatofautiana katika Mola wao kwa kughilibiwa na shetani. Uovu wa kutengana kati yao haukuwatawanya. Wala chuki ya kuhusudiana haikuwatawala, wala shaka haikuwatawanya, wala hima tofauti hazikuwagawa, hivyo wao ni mateka wa imani, hauwaachii watoke nje ya tanzi lake, sio upotovu wala ukiukaji, wala udhaifu, wala utepetevu. Hakuna sehemu hata ndogo katika tabaka za mbinguni ila kuna malaika; ama yu katika sijida au yu kwenye juhudi mwenye haraka. Muda wote wa utii kwa Mola wao wanazidi elimu kumhusu Mola wao, na enzi na utukufu wa Mola wao Mlezi unazidi kuwa mkubwa nyoyoni mwao."

## SEHEMU YA KHUTBA KUHUSU SIFA YA ARDHI NA KUKUNJULIWA KWAKE JUU YA MAJI

"Ameingiza ardhi (s.w.t) kwenye harakati za mawimbi yaliyochafuka, na kilindi cha bahari iliyojaa, mawimbi yake yanapigana pigana yenyewe kwa yenyewe, na zinatoa povu mfano wa ngamia dume, upandaji wa maji yenye kupigana kwa sababu ya uzito wa mzigo wake ukarudi chini, na ukatulia mhemko wa kupigana kwake, pindi ardhi iliposhindilia kifua chake[2],ikanyenyekea ilipojigaragaza, ikawa baada ya kelele za mawimbi yake imetulia, yenye kushindwa na kuwa dhalili chini ya mateka ya unyonge, mateka mnyenyekevu.

Na ardhi ilitulia ikiwa imekunjuka katika mawimbi yake makubwa, na ikayarudisha mwinuko wake, na (ardhi) ilivunja nguvu ya maji baada ya kupanda kwake, na kuinua pua yake na kukithiri kuvuka kwake mpaka, na ikayazuia maji hali yakiwa yamesongamana, yakatulia baada ya msukumo wake, ikajiambatanisha na ardhi baada ya kuvuma kwake.

Na yalipotulia kuchafuka kwake pembeni mwake, na kuibeba milima mirefu mikubwa pembezoni mwake, ikatumbua chemchemi za milima,

---

1. Yaani ncha za ndimi zao hazikukauka kiasi cha kuwa hawawezi kuendelea kumdhukuru (s.w.t).

2. Kifua hapa ni istiara - anakusudia kile ambacho maji yamekipata kutoka ardhini.

akayatawanya kwenye ardhi tambarare na mifereji, na alisawazisha harakati zake kwa majabali marefu miongoni mwa mawe magumu ikatulia kuyumba kwa kutumbukia majabali kwenye vipande vya sehemu zake, na kujipenyeza kwa maji na kuenea katika makorongo na tundu za pua, na kupanda kwake juu ya milima alipoitandaza ardhi yake na kupitisha amri yake, alimteua Adamu [(a.s)] akiwa mteule katika viumbe Wake, na alimfanya wa kwanza katika umbo lake, na alimfanya kuwa mkazi wa pepo Yake, na alijaalia wasaa wa mlo wake, na alimuonya kabla katika aliyomkataza, na kumjulisha kuwa kuyaelekea aliyoyakataza ni kujiingiza katika kumuasi, na ni hatari kwa daraja yake.

"Alijiingiza kwenye aliyomkataza - kulingana na ujuzi Wake (s.w.t) - alimteremsha baada ya toba, ili aikae ardhi Yake na kizazi chake, na kwake yeye iwe ni hoja kwa waja Wake. Hakuwaacha tupu wanadamu baada ya kumfisha yeye Adam. Ni katika yatiliayo nguvu juu yao hoja ya kuwa Yeye ni Mola Mlezi, na iwe kiungo kati yao na kumtambua Yeye, na kuchukua ahadi kwa ushahidi kupitia ndimi za walio wema miongoni mwa manabii wake, na wabeba amana ya risala Yake, karne na karne. Mpaka kutimia hoja yake kwa Nabii wetu Muhammad **(s.a.w.w)**, na suala kufikia udhuru wake kwa Muumba[1].

"Amekadiria riziki, ameikithirisha na kuipunguza. Na ameigawa kwa dhiki na wasaa, akaiweka katika makadirio, ili kuwajaribu waitakao kwa wepesi wake na ugumu wake, kwa hilo anatahini shukrani na subira kwa tajiri na masikini.

Kisha ameambatanisha utajiri na shida ya ufakiri, na salama ameiambatanisha na misiba na maafa yake, na fursa ya furaha yake imeambatanishwa na taabu za huzuni yake. Na ameumba muda wa umri wa kuishi, ameurefusha na kuufupisha, na ameutanguliza na kuucheleweshа, na ameuunganishia umauti na kamba zake, na kuufanya wenye kuvuta kamba zake, na wenye kukata kamba yake imara.

"Ni mjuzi wa siri za dhamiri za wenye kudhamiria, na siri za wenye kuficha, na mawazo ya moyoni, na vifungo vya azma yenye uyakini, na yanayo ibwa na muangazo wa kope za macho, na yaliyomo ndani ya siri za nyoyo, na yaliyo kwenye kina, na yaliyosikiwa kwa kuibwa na tundu za masikio, na maeneo ya sisimizi ya kupitishia muda wa kiangazi, na makazi ya wadudu wakati wa masika.

Na kurejea kwa mimba ni miongoni mwa yahuzunishayo, na sauti hafifu ya nyayo, na mahali tunda linapokuwa, katika kifuniko cha ua, na maficho ya wanyama kwenye mapango ya milima, na mabonde yake, na maficho ya mbu kwenye mashina ya miti na magome yake, na maoteo ya majani kwenye

1. Yaani hoja imetimia baada ya kumtuma Muhammad (s.a.w.w) kwa viumbe wote na jambo kufikia mwisho wake, hapajabakia baada yake Mtume mwingine anayetazamiwa; hivyo inakuwa udhuru na onyo kwa Mungu vimekamilika. Udhuru wake ni: Ule ubainisho wake kwa mukalafiina, miongoni mwa kuwaonya na adhabu Zake endapo wakiasi, na maonyo Yake: Ni kule kuwaonya Kwake kuhusu matukio.

matawi, na materemkio ya amshaji - tone la manii[1] kwenye mtiririko migongoni mwanzoni mwa kutungika kwake na kujiambatanisha kwake.

"Na kutiririka kwa matone ya mvua kutoka kwenye mkusanyiko wake, na yabebwayo na upepo pembezoni mwake, na yanayofutwa na mvua kwa mafuriko yake, na kuelea kwa wadudu wa ardhini na ni kitulizo cha mchanga, na ni makazi ya wadudu wenye mbawa kwenye vilele vya majabali, na kuimba kwa wenye kutamka katika giza la viota, na vilivyokusanywa na chaza na kutotolewa na mawimbi ya bahari[2], na vilivyofunikwa na giza la usiku au kuchomozewa na jua la mchana na viliyotokomezwa na tabaka za giza na daraja za nuru, na athari za kila hatua na hisia za kila harakati, na rejea ya kila neno[3] na - mtikisiko wa kila mdomo, na makazi ya kila mtu, na uzito wa kila chembe, na hima ya kila nafsi, na yaliyomo ardhini miongoni mwa matunda ya mti, au jani lililodondoka, au makao ya manii[4], au mahali panapokusanyika damu na mudh'ghah au mwanzo wa kuumba na kizazi[5] hakupata mashaka katika hilo, wala hakukabiliwa na upinzani katika kuhifadhi alichokibuni miongoni mwa viumbe Wake, wala hakupatwa katika kutekeleza na mambo na kuwaratibu viumbe uchovu wala ulegevu, bali elimu yake iliwaratibu, na aliwajua idadi, na kuwaeneza uadilifu wake, na kuwaingiza katika fadhila zake japokuwa ni wachache wanaostahiki.

"Ewe Allah! Wewe ni mwenye sifa nzuri, na ukamilifu usio na idadi. Ukitumainiwa ni mtumainiwa bora, na ukitarajiwa ni mtarajiwa bora. Ewe Allah! Umenikunjulia nguvu hasa kiasi cha kuwa simsifu nayo mwingine asiyekuwa Wewe, na simtukuzi mwingine yeyote asiye kuwa Wewe, si elekezi wasifu kwa chimbuko la kutofaulu na mahali pa shaka shaka[6],umeuepusha ulimi wangu mbali na sifa za wanadamu na kuwasifu waruzukiwa, wa lioumbwa.

---

1. Amshaaju: Ni maji ya mwanamume yaliyochanganyika na maji ya mwanamke na damu yake, ni wingi wa neno Mashiij katika Kiarabu, limeitwa amshaaji kutoka na neno mashaja yanapochanganyika, kwa sababu mashiij ni mchanganyiko wa viini mbalimbali, kila kimoja kinafaa kutengeneza kiungo miongoni mwa viungo vya mwili.

2. Kama ambari na mfano wake.

3. Kirejeacho miongoni mwa maneno nafsini mwako na kurudia rudia fikirani mwako.

4. Makao ya manii: kituliacho katika maji mahali, na nut'fa ni maji yenyewe, na yawezekana awe amekusudia manii, na hili latiliwa nguvu na alilotaja baada yake miongoni mwa mudh'ghah - bonge la damu.

5. Kizazi yaani Sulala. Na Sulala: katika asili yake ni kilichotolewa kwenye kitu, na nut'- fa imeitwa Sulalatul-insaan, kwa sababu mtu anatolewa humo, na hivyo hivyo mtoto.

6. Anakusudia kwa neno: 'Ma'dinul-Khaiba' - chimbuko la kutofaulu: ni wanadamu; kwa kuwa mwenye kuwasifu na kuwatumainia aghalabu hafaulu, na amewafanya kuwa ni mahali pa shaka, kwa kuwa wao hawaaminiki kwa hali yeyote ile.

Ewe Allah! kila mwenye kusifu ana haki ya ujira na fidia kwa anayemsifu, kwa hakika, nimekugeukia na macho yangu, nimekutarajia kuwa ni dalili ya kwenye akiba ya rehema na hazina ya msamaha[1].

"Ewe Mungu Wangu! hapa ni mahali aliposimama ambaye amekupwekesha kwa tauhiidi ambayo ni haki Yako, na wala hajamuona anayestahiki shukrani hizi na wasifu asiyekuwa Wewe. Mimi ni mhitaji Kwako, kwa kiwango ambacho hakiondoi umasikini wake isipokuwa fadhila Zako, wala cha kuepusha ufakiri wake isipokuwa ihisani yako na upaji wako, hivyo basi tupe sisi ridhaa Zako mahali hapa, na tutosheleze tusinyooshe mikono kwa asiyekuwa Wewe; (kwa hakika wewe umuweza wa kila kitu).".

1. Anataraji amjulishe matendo (mema) ambayo yatamridhisha. Ameyafanya matendo mema mfano wa hazina ya rehema.

# NAHJUL BALAGHA

## JUZUU YA PILI

### MTARJUMI: HARUNA PINGILI

## 92 - MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE [(A.S)]

Miongoni Mwa Khutba Zake [(a.s)] - Tabariy na Ibnul'Athiir wameisema katika matukio ya mwaka, 35 kukiwa na tofauti ndogo mno.

### WATU WALIPOTAKA KUMPA BAI'A BAADA YA KUULIWA UTHMANI

Na maneno haya sahibu zetu wanayachukulia katika hali yake ya dhahiri; Kwa hiyo wanasema: Kuwa yeye [(a.s)] hakuusiwa na Mtume **(s.a.w.w)** awe Imam, japo kuwa awe ni mbora kwa jambo hili kuliko watu wengine, na ni mwenye haki zaidi kwa daraja aliyonayo. Kwa sababu lau angekuwa ameusiwa Uimamu na Mtume **(s.a.w.w)**, isingejuzu aseme: "Dauniy waltamisuu ghayriy" - Niacheni na mwombeni mtu mwingine; na aseme: "Wa la'Ali asmaukum waatwaukum liman walaytumuhu amrakum" au aseme: "wa anaa lakum waziran khayrun minniy lakum amiran."

"Niacheni na mtafuteni mtu mwingine, kwa kuwa sisi twatazamia jambo lenye sura nyingi na rangi nyingi, nyoyo haziwezi kuvumilia wala akili haziwezi kulibeba.

Kwa kweli msitari wa upeo wa macho umefunikwa na mawingu, na njia iliyonyooka haijulikani tena[1]. Na jueni kuwa endapo mimi nitawaitikieni nitawabebesheni niyajuayo na sitosikiliza kauli ya msemaji yeyote, wala lawama ya mwenye kulaumu.

Na mkiniacha mimi nitakuwa kama mmoja yeyote miongoni mwenu. Na huenda nitakuwa mwenye kumsikiliza na kumtii mno mtakayemtawaza hili suala lenu, na mimi kuwa waziri kwenu ni bora kuliko kuwa Amiir."

**Maelezo**

Na Imamia wanauchukua usemi huu kwa maana nyingine, wao wanasema: Ambao walitaka kumpa kiapo cha utii (bai'a) ni wale waliokula kiapo cha utii kwa makhalifa waliokuwa hapo kabla; na Uthman aliwanyima walio wengi haki yao ya fungu lililokuwa wakipewa.

Kwa kuwa Bani Umayyah walikomba mali katika siku za Uthman; alipouliwa wakamwambia Ali [(a.s)]: "Tutakubai (kula kiapo cha utii kwako) kwa sharti

---

1. Njia iliyonyooka haijulikani, kwa sababu alama zake zimebadilika, kwa hiyo ikawa haijulikani tena, na maana inakuwa: Shub'ha imezitawala akili na nyoyo, na watu walio wengi wamekuwa hawaijui ilipo njia ya kweli! Na hiyo ni kwa sababu tamaa imewaingia watu wengi katika utawala wa Uthman kutokana na kuboreshwa katika upewaji wa ruzuku, kwa hiyo haiwi rahisi kwao kuwekwa sawa na wengine, hivyo basi lau wangetendewa uadilifu wangemponyoka na kutaka vurugu ya fitna; kwa tamaa ya kupata utashi wao. Na hao aghalabu ndio maraisi katika kaumu.

Endapo Imam [(a.s)] atawapitishia kama walivyokuwa katika kuboreshwa atakuwa ameleta dhulma, na kuihalifu sharia, na walipizao kisasi kwa Uthman walikuwa wanataka insaafu, vinginevyo watachochea fitnah, hivyo basi wapi aelekee ili kuifikia haki akiwa salama bila ya fitna! Na yalitokea baada ya bai'a yake aliyokuwa akiyabashri kabla yake.

kwamba uende na sisi mwendo wa Abu Bakr na Umar; Kwa kuwa wao hawa wawili walikuwa hawahodhi mali kwa ajili yao binafsi wala kwa ajili ya ah'li zao, kwa ajili hiyo walimuomba Ali (a.s) wamfanyiye bai'a ili awagawiye mgao kutoka baytul'mali kama ule wa Abubakar na Umar; Hapo ndipo akawakatalia na akawataka wamchague mtu mwingine ambaye atakwenda mwendo wa hawa wawili.

## 93 - MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

Miongoni Mwa Khutba Zake (a.s) - Abu Na'im amesema katika Hilyatul-Auliyai, jalada la kwanza, uk. 68, na Ibn Wa'dhwih katika Ta'arikh yake, jalada la tatu, 182.

### NDANI YA KHUTBA HII AMIRUL-MU'MININ ANABAINISHA UBORA WAKE NA ELIMU YAKE. NA ANABAINISHA FITNA YA BANI UMAYYAH

"Baada ya kumhimidi Mungu na kumtukuza! Enyi watu! kwa hakika mimi nimetoboa jicho la fitna[1], na hangethubutu mwingine yeyote asiyekuwa mimi baada ya kutanda giza lake[2]. Shari yake na maudhi yake yamekuwa makali.

"Hivyo basi niulizeni kabla hamjanikosa, namuapa ambaye nafsi yangu iko mkononi Mwake kwamba hamtoniuliza kitu tokea hivi sasa na siku saa itakapofika, wala kuhusu kikundi kitakachowaongoza watu mia moja na kuwapoteza mia nitakupeni habari nani mlinganiaji wake na kiongozi wake na mhamasishaji wake na mashukio ya ngamia wake, na kituo cha msafara wake, na ambao watauwawa miongoni mwa watu wake, na ambao watakufa kwa kifo cha kawaida.

"Na mtakaponikosa na mtapofikwa na shida ya vita na mambo magumu waulizaji wengi wangenyamaza na kuinamisha vichwa chini, na kuogopa wengi miongoni mwa watakaoshika nafasi za kuulizwa, na hivyo itakuwa viishapo vita vyenu, ikiwa na magumu kwenu, dunia itakuwa imebana kwenu, siku za balaa mtaziona ndefu, mpaka Mungu atakapowapa ushindi baadhi ya watu wema waliobaki miongoni mwenu.

"Kwa kweli fitna inapoingia utata hujitokeza[3].

---

1. Faqa'atuha: Nimeyachana (macho) na kuyang'oa. Hayo ni maneno ya mfano akiwa anamaanisha kuishinda fitna, hivyo ameijaalia fitna kama kiwa chenye macho makali watu wanayachelea, yeye alithubutu, akayapasua macho yake ikatulia baada ya kucharuka kwake, na hii ni miongoni mwa istiara, na hiyo ilikuwa baada ya kuumaliza mgogoro wa An-Nah'rawani na kuwashinda kwake Khawarij.

2."Al'ghayhabu": Giza, na "maujuha", ni kutanda na kuenea kwake, hivyo basi maana inakuwa baada ya kutanda na kuenea upotovu, kwa hiyo amedokeza badali ya upotovu akatumia neno "Al-ghayhabu''na badali ya kutanda na kuenea ametumia neno "at-Tamauju."

3. Shabbahat: Utata huingia, yaani haki haitambuliki kwa kuchanganyika na wingi wa batili.

Ikigeuza mgongo hutambulika[1]; haitambuliki inapokuja, na hutambulika inapotoweka[2]. Na yazunguka mzunguko wa upepo, unaisibu nchi na kuikosa nchi.

"Jihadharini, kwa hakika fitna ninayoihofia sana mimi kwa ajili yenu ni fitna ya Bani Umayyah. Kwa kuwa hiyo ni fitna pofu yenye giza: Jambo lake limeenea[3]Na balaa lake limekuwa kwa sura makh'susi. Na wakapatwa na balaa humo wenye kuitambua haki[4]. Balaa litamuepuka asiyejua.

Namuapa Mungu kwamba mtawakuta Bani Umayyah ni watu waovu kwenu baada yangu kama ngamia jike mzee mwenye tabia mbaya, yuang'ata kwa mdomo wake na apiga kwa mkono wake na kupiga teke kwa miguu yake ya nyuma na yu azuia kukamuliwa maziwa yake.

"Watabakia juu yenu mpaka hawatomuacha miongoni mwenu isipokuwa yule wa manufaa kwao, au asiye na madhara kwao. Balaa lao litaendelea juu yenu mpaka kiasi cha kuwa kuomba nusura kwa mmoja wenu dhidi yao ni kama kuomba nusura kwa mtumwa dhidi ya bwana wake[5]- na kwa mfuasi dhidi ya amfuataye, fitna yao mbaya na ya kuogofya itakujieni na sehemu ya jahiliya, hakuna humo alama za muongozo, wala dalili ionekanayo. Sisi ni Ahlul-Bayt (wana wa nyumba ya Mtume) twaepukana na hayo, wala si wanusuru wa hayo.

Kisha Mungu atakuondoleeni kama iondolewavyo ngozi kutoka kwa wenye kuambatana nayo kwa madhila, na kuwasukuma kwa mabavu, na kuwanywesha kikombe kichungu, hatowapa ila upanga, na wala hatowavika isipokuwa hofu.

Hapo Makuraishi watataka hata kwa gharama ya dunia yote na yaliyomo humo ili wanione mimi japo kwa mara moja tu lau kwa kadiri ya muda ule wa kuchinjwa ngamia ili niwakubalie lile ambalo hivi sasa nawaomba sehemu tu lakini hawako tayari kunipa.[6]".

---

1. Hujulikana ikigeuza mgongo yaani ikienda, kwa sababu zajulikana baada ya kupita kwake na hufichuka ukweli wake kwa hiyo huwa funzo.

2. Mfano wake ni fitna ya vita vya Jamal, na fitna ya Al-Khawarij - wenye kujiengua - watu wengi kuyahusu matukio hayo mawili mwanzoni walisita, na hali ya mambo ilitata kwao, mpaka vita vilipokwisha ikawabainikia kwa kumtambua mpotovu mbali na muongofu.

3. Kuenea kwa jambo hili kwa kuwa ni uongozi wa sura ya jumla, na balaa lake limekuwa kwa sura makh'susi kwa Ahlul'bayti, kwa sababu ni kuporwa kwa haki yao.

4. Kwa mwenye kuitambua haki humo balaa la kisasi humshukia kutoka kwa Bani Umayyah.

5. Yaani kunusurika kwa watu wanyonge si kunusurika; kwa kuwa mtumwa hanusuriki dhidi ya bwana wake kamwe.

6. Huku ni kutoa habari za kudhihiri kwa "Musawudatu" na kumalizika kwa ufalme wa Bani Umayyah: yaani Bani Abbasi 'kaulimbiu' yao ilikuwa ni: Assawadu. Na habari aliyoielezea (a.s.) kuhusu wao ilitokea, imekuwa kweli kauli yake: "tawad Quraishi:…" - wanatamani Maquraishi - wamenakili wana historia wote kuwa Marwan bin Muhammad siku ya Zaabbu alipomuona Abdullah bin Ali bin Abdillahi bin Abbas mbele yake katika safu ya Khurasani alisema: "Ningependa Ali bin Abi Talib angekuwa chini ya bendera hii badala ya huyu kijana.".

Kisha alisema (a.s): “Niulizeni kabla hamjanikosa.” Bwana mwenye Kitabu cha Al-Isti’ab naye ni Abu Umar Muhammad bin Abdil-Bari ameeleza akinakili kutoka kwa jamaa wasimuliaji na wanahadiithi, wamesema:
‘Hakupata kusema yeyote miongoni mwa masahaba (r.a): ‘niulizeni’ isipokuwa Ali bin Abi Talib. Na Sheikh Abu Ja’far Al-Iskafi ameeleza ndani ya Kitabu Naq’dhul-Uth’maniyah’’ akinakili kutoka kwa Ali bin Al- Jahdi kutoka kwa Ibin Shubrimah, Amesema: ‘Hawezi yeyote miongoni mwa watu kusema juu ya mimbari ‘niulizeni’ isipokuwa Ali Bin Abi Talib (a.s).

## 94 - NA MIONGONI MWA KHUTBA YAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Khutba Yake (a.s) - Ibn Abd-Rabi ameieleza katika al-Iqdul-Farid, jalada la 4, uk. 74, na al-Saduq katika Tawhid, uk.20.

### KUHUSU SIFA ZA MANABII

“Ametukuka Mwenyezi Mungu [1] ambaye umbali wa mtazamo na fikra haumfikii, wala dhana ya utambuzi haimpati. Wa mwanzo ambaye hakuna upeo iwe anaishia huko wala hana mwisho iwe yuamalizikia hapo.
Na miongoni mwa hutuba hiyo: “Amewaweka weko bora na akawafanya watuwame kwenye tuwamo la kheri, imewanakili migongo mitukufu na kuwafikisha mifuko ya uzazi iliyo tohara; kila wapitapo - wafapo - waliotangulia, waliobaki kati yao hutekeleza dini ya Mungu, mpaka heshima ya Mungu (s.w.t) imeishia kwa Muhammad **(s.a.w.w)**; akamtoa kutoka kwenye asili iliyo bora, na asili yenye heshima kuu, na kutoka mti ambao manabii Wake wametoka humo, na akachagua kutoka humo waaminifu Wake, Itrah yake ni miongoni mwa itrah; kizazi cha nyumba ya Mtume Mtukufu **(s.a.w.w)** zilizo bora. Na familia yake ni miongoni mwa familia zilizo bora. Na mti wake ni katika miti bora; umeinukia katika utukufu. Una matawi marefu; na matunda yasiyofikiwa[2];yeye ni imam wa wenye kufanya taq’wa, na ni mwanga wa wapendao mwongozo.
“Ni taa ambayo umemweta mwanga wake, na kimondo nuru yake imeangaza, na kipekecho cha moto ambacho mwanga wake umeangaza, sira yake ni insafu na sunna yake ni mwongozo, na maneno yake ni upambanuzi, na hukumu yake ni uadilifu; alimtuma wakati wa mwanya kati ya mitume[3] na wakati ambapo umma umepotoka na kupotoka kimatendo, na kutoelewa kati ya umma.
“Fanyeni mema - Mungu awarehemu - kwa mwanga wa wazi, njia ni ya wazi inaitia (watu) kwenye nyumba ya amani, (yaani pepo) hali mkiwa ndani ya nyumba ya kutafuta ridhaa (za Mungu), mkiwa na muda na fursa, na vitabu viko wazi (vitabu vya kuandika matendo ya waja), na kalamu ziko

1. Tabaaraka-llahu, wanasema tabaraka ina maana mbili: moja ya hizo mbili ni: kheri Yake imebarikiwa, na neema Zake na hisani Zake zimezidi. Hii ni dua, na ya pili iwe yakusudiwa: kuzidi na kutukuka dhati na sifa Yake, kwa maana ya kwamba hawezi kulinganishwa na mwingine; na huu ni utukuzo.

2. Hakusudii kuwa matunda yake hayana manufaa yeyote, kwani hiyo sio sifa njema, bali amekusudia kuwa matunda yake hayafikiwi kwa mabavu, wala hayachumwi kwa kupora.

3. Fitra: Mwanya: ni wakati uliopo kati ya manabii, yaani huyu aliopo muda wake umekwisha kabla ya kuja mwingine.

mashughulikoni (kalamu za malaika), na miili iko na siha, ndimi zikiwa huru, toba zinapokelewa, na aamali zinakubaliwa.”.

## 95 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

Anaelezea Katika Khutba Hii Hali Ya Watu Ilivyokuwa Wakati Wa Bi’tha

“Allah (s.w.t) alimtuma (Muhammad) hali watu wakiwa wapotevu katika mkanganyiko, na wakikusanya fitna[1], utashi wa nafsi umewaghilibu, na kibri kimewafanya wateleze, [2] na jaahiliya iliyoshona imewahafifisha,[3]wameduwazwa na myumbo wa mambo, na balaa la ujinga. Hivyo basi Mtume **(s.a.w.w)** alikithirisha katika kutoa nasaha nyofu, naye alipita njia ya sawa, na aliwaita kwenye hikima na mawaidha mema.”.

## 96 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

“Shukrani ni za Mungu ni wa mwanzo hapakuwa na kitu kabla yake, na ni wa mwisho hapatokuwa na kitu baada yake, na ni wa dhahiri hapana kitu juu yake, na ni wa batwini hapana kitu chini yake.”.

Na miongoni mwake katika kumsifu Mtume **(s.a.w.w)**: “Mahali pa makazi yake ni mahali bora, na asili yake ni asili iliyo bora mno kuliko asili zote, ni asili ya heshima na susu iliyo salama[4]. Nyoyo za watu wema zimeelekezwa kwake, na hatamu za macho zimegeuzwa kumuelekea yeye. Mungu (s.w.t) amezizika chuki kupitia yeye[5], na kwa yeye amezima mashambulizi ya kulipiza kisasi [6], kwa yeye ameunganisha udugu, na kuwatenganisha

---

1. Wanao kusanya fitna: Ni wanaokusanya kuni: Na Waarabu humwita anayechanganya kati ya maneno mazima na mabovu au asemaye kati ya maneno ya sawa na yaliyopotoka: Haatibul’layli: Mkusanya kuni usiku, kwa kuwa hajui kinachokusanywa na kamba yake.

2. Kiburi kimewatelezesha: Yaani kimewafanya wateleze na wawe kwenye makosa, kikawapeleka kwenye mtelezo na kuanguka kwenye madhara. Na katika riwaya nyingine, Istazahum (al-kubarau) yaani wakubwa wao na mabwana zao wamewapoteza.

3. Jahiliyah ni hali waliokuwa nayo Waarabu kabla ya nuru ya elimu ya Uislamu: ikawafanya wawe na akili hafifu.

4. Yaani anatokana na nasaba iliyo tohara mbali na aibu, kwani yeye amezaliwa mahali palipo salama mno mbali na aibu ya uzinzi.

5. Kuizika chuki: Yaani kuizuia kwa kuwa yeye ni Mtume wa utangamano na wana dini yake ni watu wa mtangamano wenye kusaidiana katika mambo ya kheri, na ambaye hayuko ndani ya tanzi la mtangamano miongoni mwao basi Yeye - Mungu swt. ndiye ajuaye - yuko nje mbali nao.

6. Uadui wa kushambuliana: Yaani uadui wa mtu kumshambulia ndugu yake, ili amdhu- ru, ikiwa hatomuuwa.

walioungana[1] na kwa yeye amewatukuza waliokuwa dhalili[2], maneno yake ni ubainifu na kunyamaza kwake ni hekima.”.

1. Amewatangamanisha kwa uislamu wakawa ndugu na amewafarikisha kwa Uislamu waliokuwa karibu, ni kwa sababu Uislamu umewatangamanisha waliokuwa mbali kwa nasaba, mfano wa Ali na Ammar, na kuwafarikisha waliokurubiana kwa nasaba, mfano wa Hamza na Abu Lahab, na kuwafarikisha waliokurubiana kwa mtangamano wa kishirikina. Amesema (s.w.t): “fa asbah’tum biniimatihi ikh’wanan” (kwa neema yake mkawa ndugu 3:103).

2. Udhalili wa wanyonge miongoni mwa watu bora waliositirika na stara ya kutotajika, na wamedhalilishwa na enzi ya ushirikina na dhulma na uadui.

# NAHJUL BALAGHA

## JUZUU YA PILI

### MTARJUMI: HARUNA PINGILI

## 97 - MIONGONI MWA MANENO YAKE (A.S)

## KUWAKEMEA SAHABA ZAKE

"Japo Mwenyezi Mungu amwachie muda dhalimu mshiko wake hautomkosa, naye yuamchunga kwenye mapito ya njia zake, na mahali pa mkwamo wa koo mapitio ya mate yake[1], naapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko mkononi mwake, hawa watu (Mu'awiya na kundi lake) watapata ushindi dhidi yenu[2],

---

1. Mahali pa mkwamo wa koo (ambapo hukwama mfupa au mwiba), mapitio ya mate: maneno hapa yametumika kimfano kwa ukaribu wa ukali wa ki-ungu dhidi ya madhalimu.

2. Kisha (a.s) aliapa kuwa hapana budi watu wa Sham - Syria - watapata ushindi dhidi ya watu wa Irak, na hiyo si kwa kuwa ndio wenye haki na kwamba watu wa Iraki (watu wa Iraki hapa ni jeshi la Amirul-Mu'minina Ali bin Abi Talib) wako katika batili; bali ni kwa kuwa wao (watu wa Sham ambao ni watu wa jeshi la Muawiyah bin Abi Sufian) ni watii mno kwa amiri-jeshi wao, yaani kamanda wao wa vita; na kigezo cha ushindi vitani ni utii wa jeshi kwa kiongozi wao na kutengenea kwa mambo yake, si katika kuwa waamini itikadi ya haki ndio lazima ushinde! Kwa kuwa vitani haitoshi kuwa jeshi lipo kwenye haki hata rai zitafautiane, na liwe halitii amri ya mnadhimu wake, kwa ajili hiyo waona mara nyingi washirikina wanashinda dhidi ya watu wenye itikadi ya tawhidi. (Kwa mantiki hiyo usemi ulio zoeleka: "Mungu mwenyewe atainusuru dini yake," hauna maana yoyote, bali ni dalili ya kutoelewa mambo yapasavyo kuwa.

watawala wake,* hali ikiwa mimi nimekuwa nahofia dhulma ya raia wangu. Niliwaita kwa ajili ya vita hamkuja, niliwaonyeni hamkunisikiliza, (*) Kisha (a.s) alikumbusha nukta nzuri kuhusiana na maana hii, akasema: "Kwa kawaida raia ndiye aogopaye dhulma ya mtawala, lakini mimi naogopa dhulma ya raia wangu." Na mwenye kuzingatia hali yake (a.s) zama za ukhalifa wake, atatambua kuwa alikuwa mfano wa mtu aliyewekewa vikwazo; alikuwa hawezi kuyafikia ayakusudiayo nafsini mwake. Hiyo ni kwa sababu wamjuao ukweli wa hali yake ni kidogo mno; na kundi kubwa la watu lilikuwa haliamini kumhusu Amirul-Mu'minina ambavyo ipasavyo kuamini, na walikuwa kwa maoni ya waliomtangulia katika makhalifa ni bora kuliko yeye, na wengi wanadhania kuwa ubora upo katika kushika ukhalifa kwa hali yoyote ile, hata kwa nguvu, kama vile mfano wa Muawiyah, kundi kubwa la waislamu wanaona kuwa yeye ni khalifa yapaswa aitwe Amirul-Mu'minina, hali yaendelea hivyo, wafuatao wanawakalidi waliotangulia; na wanasema: 'Lau waliotangulia wangejua kuwa yuko bora kuliko wao wasingewatanguliza waliotangulia.' Na hawamzingatii ila ni mfuasi wa waliomtangulia kwa ubora. Na kwamba yeye alikuwa raia wao, na wengi wao walikuwa wanapigana katika kundi lake kwa ushabi- ki tu na kwa fahari ya ushujaa wa kiarabu, sio kwa ajili ya dini na itikadi. Na yeye (a.s) alikuwa analazimika kwenda nao kwa upole na kuwakurubia; alikuwa hawezi kudhihirisha aliyonayo; angalia barua zake kwa watendaji wake kwenye mikoa! Kama usemi wake: "Hukumu ni kama mlivyokuwa mnahukumu ili ipatikane jamaa kwa watu, na nife kama walivyo kufa swahibu zangu". Maneno haya hayahitaji ufafanuzi zaidi, maana yake iko wazi, nayo ni kuwa yeye aliwaambia: "Fuateni kawaida yenu kwa hivi sasa katika haki hii ya haraka kuhusu hukumu na maamuzi ambayo mlikuwa mnahukumu mpaka watu wawe na umoja; yaani mpaka mambo haya yafikie mtangamano na kutoweka mfarakano, na kutu- lia kwa fitna. Hapo nitawatambulisha niliyonayo kuhusiana na mambo haya na hukumu ambazo mlikuwa mmeendelea nazo.

Kisha alisema: "Au nife kama walivyokufa sahibu zangu." Kuna anayesema: 'Sahibu zake hapa; alikuwa anakusudia makhalifa waliomtangulia.' Na kuna anayesema: 'Sahibu zake alikuwa anakusudia Shi'a wake mfano wa Salman, Abu Dhar, Miq'dad, Ammar na wengine

si kwa sababu wana haki zaidi kuliko mliyonayo bali ni kwa sababu ya haraka yao ya kutekeleza batili yao na ugoigoi wenu mbali na haki yangu (kuifuata). Umma huwa waogopa dhulma ya niliwaiteni kwa siri na kwa wazi hamkuitika, nilikunasihini hamkukubali.

"Mkiwa mpo kama hampo, mko watumwa kama mabwana![1] Ninakusomeeni nukta za hekima mnazikwepa, na ninakuonyeni kwa mawaidha yafikayo (masikioni) mnafarakana mbali nayo, nawahimizeni kwenda jihadi dhidi ya watu waovu, wala sijafikia mwisho wa kauli yangu nawaona mnatawanyika mfano wa mikono ya Sabaa - Ayaadiy sab'a.[2] "Munarejea kwenye makazi yenu mkiwa hamuwaidhiki. Nakunyoosheni asubuhi, mwarejea kwangu jioni mkiwa mmepindama kama upinde, mnyooshaji amehemewa na mnyoshwaji amekuwa mgumu.

"Enyi kaumu ambao miili yao ipo hadhiri hali akili zao zimeghibu, na ambao utashi wao uko tofauti. Watawala wao wamepatwa na balaa. Sahibu yenu yuamtii Mungu, na ninyi mnamuasi, na sahibu wa watu wa Sham yuamuasi Mungu na hali wao wanamtii! Ningependa, wallahi lau Muawiya hangenibadilishia ninyi ubadilishaji wa dinari na dirham, angewachukua kutoka kwangu kumi kati yenu na angenipa mimi mtu mmoja kutoka wao!

"Enyi Watu wa Kufa! nimepata uzoefu kwenu wa matatu na mawili mengine: Mko viziwi hali mkiwa na masikio, na mko mabubu hali mkiwa mwasema, vipofu mlio na macho. Sio wasaidizi wa kweli wakati wa mapambano wala sio ndugu wa kuaminika kwenye balaa! Mikono yenu iingie mchanga!( – yaani mikono yenu isiwe na kheri! - hili ni neno la kumlaani mtu). Enyi mlio

---

mfano wao.' Huzingatii kauli yake akiwa juu ya mimbari kuhusu mamawatoto: "Rai yangu na rai ya Umar ni kwamba wasiuzwe, na mimi sasa naona wauzwe".

Inaendelea uk.81.

Basi Ubaida Assalmaniy, akamwambia: 'Rai yako ukiwa pamwe na jamaa yapendeza mno kwetu kuliko rai yako peke yako.' Hakurudia kusema lolote. Je hili lajulisha nguvu na kuyadhibiti mambo; au udhaifu katika mamlaka na unyonge?! Je hekima na maslahi katika wakati ule ilikuwa sio kunyamaza na kujizuia?! Huzingatii (tukio moja) alikuwa akisoma katika sala ya asubuhi nyuma yake kukiwa na jamaa katika sahibu zake; mmoja wao akasoma hali amepaaza sauti yake, akiwa anakinza usomaji wa Amirul-Mu'minina (a.s): "inil'hukmu illa lillahi yaq'dhwii bilhaqi wahuwa khayrul'faasiliina." (Hapana huku- mu ila ni ya Mungu, anahukumu naye akiwa mfanya maamuzi bora). Hakubabaika alay his-salaam, na wala hakuvunja sala yake na wala hakugeuka nyuma, lakini yeye alisoma hali akimpinga: "fasbir inna wa'ada llahi haqun wala yastakh'lifannaka lladhiyna la yuuqinuuna." Na hii ni subira kubwa na utulivu wa ajabu na ni tawfiiq iliyo bayana. Kwa haya na mengine mfano wake sahibu zetu miongoni mwa mutakalimiina wameyatolea dalili juu ya uzuri wa siasa yake na usahihi wa uratibu wake, kwa kuwa mwenye kupatwa na ria kama hawa wenye utashi unaopingana, na jeshi kama hili linalomuasi na linalompinga, kisha kwalo akavunja maadui, na viongozi, hafiki yeyote alipofika kwa uzuri wa siasa na uzuri wa mpango. Mwisho wa Tanbihi *.

1. Watumwa kama mabwana: anawasifu kiburi na upotovu.

2. Ayaadiy Sabaa: Mikono Sabaa, mithali hupigwa kwa kiarabu kwa wenye kufarakana. Yasemekana: Kuwa Sabaa ni Abu Arab Al-Yamani, alikuwa na watoto kumi, akawaweka sita kuliani na wanne kushotoni; akiwafananisha na mikono miwili, baadae watoto hao walitawanyika vibaya sana, ndio maana waarabu huupigia mfano mfarakano wowote na mfarakano wa ayaadiy sab'a - mikono Saba.

mfano wa ngamia ambao mchungaji wake ameghibu! Kila wakusanywapo upande mmoja wanatawanyika upande mwingine.
Wallahi nawaona kwa maoni yangu, endapo vita vitakuwa vikali na hali ya mambo ikiwa inayumba mtamkimbia mwana wa Abi Talib ukimbiaji wa mwanamke akiwa uchi mbele, kwa hakika mimi nipo katika mwongozo wa wazi kutoka kwa Mola wangu Mlezi, na (niko) katika njia ya Nabii wangu, na niko katika njia ya wazi nikiokota cha kuokota[1].

"Waangalieni Ahlul-bayt wa Nabii wenu, na jiambatisheni na mwendo wao, na fuateni nyayo zao, hawatokutoweni nje ya mwongozo, na hawato kutumbukizeni kwenye maangamizi, wakikaa kaeni wakiinuka inukeni, msiwatanguliye mtapotea, wala msibaki nyuma yao mtaangamia.
Kwa kweli nimewaona sahaba za Muhammad **(s.a.w.w)** simuoni yeyote kati yenu anashabihiana nao, kwa kweli walikuwa wanaianza asubuhi wakiwa na nywele timtim na wakiwa wamejaa vumbi kichwani (na mwilini)[2].

Wamepitisha usiku katika hali sijda na qiamu, wakibadili kati ya paji zao za uso na mashavu yao ( yaani mara wakisujudu kwa paji la uso na mara nyingine kwa mashavu yao). Na walikuwa wanasimama mfano wa aliyesimama juu ya kaa la moto kwa ajili ya kukumbuka marejeo yao, kana kwamba kati ya macho yao kuna goti la mguu wa mbuzi kutokana na sijda zao ndefu. Atajwapo Mungu macho yao hutiririsha machozi mpaka yalowesha kosi (kola zao), walikuwa wana yumba kama uyumbavyo mti siku ya upepo mkali, wakiogopa adhabu, na wakiwa na matarajio ya thawabu.".

## 98 - NA MIONGONI MWA MANENO YAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Maneno Yake (a.s) - Ibn Qutaybah ameeleza katika al-Imama was-Siyasah, jalada la kwanza, uk. 151.

### KUHUSU DHULMA YA BANI UMAYYAH

"Wallahi wataendelea hivi (Ufafanuzi: Usemi hapa ukadiriwe hivi: Wangali bado ni madhalimu) mpaka wafikie kiasi cha kuwa hawatoacha alichokiharamisha Mungu ila watakihalalisha, wala ahadi ila wataitangua na hata haitobakia nyumba ya matofali wala ya manyoya ila dhulma yao itaingia, na ubaya wa matendo yao utawafanya duni.
Mpaka watakuja kusi-mama waliaji wawili walie: Mliaji analia kwa ajili ya dini yake, na mliaji alia kwa ajili ya dunia yake, mpaka iwe nusura ya mmoja wenu kwa mwingine mfano wa nusura ya mtumwa kwa bwana wake, akiwa yupo anamtii, na anapoghibu humsengenya.
Mpaka itakuwa mwenye shida kubwa mno kati yenu ni yule mwenye kuwa na dhana njema mno kwa Mungu miongoni mwenu.

---

1 . Naokota chakuokota: Anamaanisha kuwa upotovu umefikia kiasi cha kuushinda mwongozo, kwa hiyo mimi naiokota njia ya mwongozo kati ya njia za upotovu nikiokota huku na kule. Na kuokota ni namna ya uchukuaji kitu kutoka ardhini, na kuitwa kwa wafuasi wake kuihusu njia ya haki kuokota ni kwa sababu haki ni moja na batili ziko rangi tafauti, hivyo basi yeye huiokota haki kati ya aina kadhaa za batili.

2. Wanaianza asubuhi wamejaa vumbi: Ni ibara ya kuelezea maisha yao ya kujinyima na kujibidisha sana kiibada, kwa mfano, kusali sala za usiku, kufunga saumu za sunna mchana, kujiweka mbali na raha. Kwa hivyo makusudi ni kuwa wao walikuwa wanaishi maisha ya kujinyima kwa ajili ya Mungu (s.w.t).

Mungu akikutunukieni amani na salama ikubali- ni, na akikupeni mtihani vuteni subira, “..... Na kwa hakika mwisho mwema ni wa wachamungu.”(7:128).

## 99 - MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

Miongoni Mwa Khutba Zake (a.s) - an-Nuuriy ameieleza katika al-Mustadrak Jz. 1, uk. 411, na as-Saduq katika Man la Yahdhurul-Faqih, Jz. 1, uk. 270.

### KATIKA KUJIEPUSHA NA DUNIA

“Tunamhimidi kwa yaliyotokea, na tunamuomba msaada kwa ajili ya mambo yetu yatakayokuwa, tunamuomba usalama katika dini, kama tunavyomuomba usalama kuihusu miili[1].

“Nakuusieni kujiweka mbali na dunia hii ambayo ni yenye kukuacheni japo muwe hampendi kuiacha, na ni yenye kuichakaza miili yenu japo mupende kuifanya upya. Kwa kuwa mfano wake na ninyi ni kama wasafiri[2], wamesafiri waliokwenda kiasi fulani cha masafa kisha wakawa kana kwamba wao haraka wameikata safari, wameikusudia alama, na mara moja kana kwamba wameifikia. Ukaribu ulioje wa masafa kwenye lengo endapo mtu atalielekea na kulifikia! Ukaribu wa masafa ulioje wa kwenye lengo ikiwa mtu yualielekea na kulifikia!

Hatua fupi ilioje ya mtu aliye na siku moja tu ambayo hawezi kuizidisha, hali ikiwa amtakaye mwenye haraka yaani mauti amfuata, anasumbua duniani mpaka aitoke apende asipende! Hivyo basi msihusudiane kugombania utukufu wa dunia na fahari yake, na wala msifurahiye mapambo na neema zake, na wala msiyahuzunikie madhara yake na shida ya madhara yake.

“Kwa hakika utukufu wake na fahari yake vinaelekea kukatika, mapambo yake na neema zake vitatoweka, madhara yake na shida zake zinakwisha, na kila muda humo waelekea mwisho, na kila aliye hai humo aelekea mwisho.

Je ninyi kutokana na athari za waliokuwa mwanzo hamuonyeki! Na katika babu zenu wa mwanzo kuna ufunguzi wa macho na zingatio, endapo mtakuwa mnatia akilini! Je hamuoni kuwa waliopita miongoni mwenu hawarejei, na walioendelea kuishi hawatobaki milele! Si mwaona wana wadunia wanaingiwa na jioni na wanaingiwa na asubuhi wakiwa katika hali nyingi mtawanyiko: Kuna aliyekwisha kuwa mauti analiliwa, na mwingine ahaniwa, na aliyetupika chini amekumbwa na balaa, na mwenye kumtembelea mgonjwa, na mwingine anatapia nafsi yake, na ambaye aitafuta dunia na mauti yamtafuta yeye, na kuna aliyeghafilika wala haghafilikiwi, na katika athari za waliopita hupita waliobakia! Lo! Mkumbukeni mbomoa raha, na anayeyatia uchungu matamanio, na mkata matumaini, pindi yavamiwapo matendo mabaya, na muombeni msaada Allah (swt) ili kutekeleza wajibu wa haki Yake, na neema Zake na hisani Zake zisizo na idadi.”.

---

1. Amefanya vyema na kubuni (a.s) katika usemi wake huu, na hivyo ni kwa sababu dini au itikadi pia zina ugonjwa, tiba na kupona kama ambavyo miili ilivyo.

2. Yaani wasafiri: Kwamba ninyi mpo katika masafa ya umri ni kama walivyo wasafiri katika masafa ya njia, hawabakii ila watafikia mwisho kwa kuwa (dunia) ina kikomo.

## 100 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

### KUMHUSU MTUME WA MUNGU NA AHLUL-BAYT WAKE

"Mstahiki wa sifa ni Allah Mwenye kueneza fadhila Zake kwa viumbe, na Mwenye kuwanyooshea mkono wake wa ukarimu. Tunamtukuza katika mambo Yake yote, na tunamuomba msaada ili kuzichunga haki Zake.

Na tunashuhudia kuwa hakuna mungu mwingine, isipokuwa Yeye na kuwa Muhammad ni mja Wake na mjumbe Wake, amemtuma kudhihirisha amri Yake na kuitangaza, na awe mwenye kutamka utajo Wake.

Na alitekeleza kwa uaminifu, na alifariki akiwa ndani ya uongofu; na alituachia bendera ya haki[1], mwenye kuitangulia atakuwa ametoka[2], na mwenye kubaki nyuma yake atakuwa amenyauka, na mwenye kujiambatisha nayo atakuwa amejiunga na haki.

Dalili yake ni umakini wa usemaji[3], asimama taratibu, ana haraka akienda. Hivyo basi endapo ninyi mtamlainishia shingo zenu (yaani mkimtii), na mkamuishiria kwa vidole vyenu[4], 4mauti itamjia na itaenda naye, na mtabaki baada yake ma'sha'Allaahu, mpaka Mungu amtoe kwa ajili yenu mmoja ambaye atakukusanyeni, na kuuweka pamoja mparaganyiko wenu, msimtumainie asiyekuja wala msikate tamaa na aliyegeuza mgongo[5]kwa kuwa aliyegeuza mgongo huenda ukamteleza mguu wake mmoja, na ukathibiti mwingine, na ikarudi miwili mpaka ikathibiti yote.

"Juweni! Kuwa mfano wa Aali Muhammad **(s.a.w.w)**, ni mfano wa nyota za mbinguni, ikizama nyota yachomoza nyota. Kama kwamba neema za Mungu zimekukamilikieni, na amekuonesheni kile mlichokuwa mwakitarajia.[6]"

---

1. Bendera ya haki ni: Vizito viwili vilivyoachwa baada ya Mtume (s.a.w.w) navyo ni Kitabu cha Mwenyeezi Mungu na Itrah ya Nabii (Ahlul-Bayt).

2. Ametoka: Mwenye kuitangulia bendera ya haki atakuwa ametoka nje ya dini. Na aitanguliaye bendera ya haki ni yule ambaye anayeongeza juu ya sharia aliyoiweka Mungu, matendo au itikadi, akidhania kuwa anaipamba dini, na anaikamilisha, na yu anaiita ziada hiyo aliyoiongeza kwa jina la: Bid'atun hasanatun.

3. Umakini wa usemaji: Yaani anajikusudia yeye mwenyewe (a.s), yaani polepole, anachunga katika usemaji wake, haharakii bila kuzingatia, na maana inakuwa ni mwenye upole na kuzingatia, kisha alitilia mkazo kwa kauli yake: 'anasimama polepole' na akienda anaharakisha. Hivyo yeye haharakishii kutenda jambo kwa fujo ila akiona kwamba kuna njia ya ufanisi anaendelea haraka, hiyo ni kama kwamba anajisifu mwenyewe, Karamallah Wajihahu.

4. Kumuishiria kwa vidole:Yaani mkimheshimu na kumtukuza kama mfalme ambaye huoneshwa kwa kidole wala hasemeshwi kwa ulimi.

5. Yaani afapo huyu kiongozi na kuwaacha wanawe (baada yake) jambo la mmoja wao likayumba, msikate tamaa na kuingiwa na mashaka na mseme: "Huenda tumekosea kuwafuata hawa jamaa;" kwa kuwa mwenye kuyumba mambo yake katika sisi miguu yake itakujathibiti, na ikiwa mmoja kati ya miguu miwili utateleza, mwingine utathibiti na kuufanya ulioteleza uthibiti pia.

6. Mungu aliwaahidi kuwa faraja ipo karibu, na huu ni mfano wa ahadi za kiungu kuwa saa (kiyama) ikaribu. Kwa hakika vitabu vilivyoteremshwa vyote vimesema waziwazi ukaribu wake, japo kwetu kiko mbali, kwa kuwa la mbali (kwetu) katika elimu ya Mungu ni karibu:

“Innahum yaraunahu ba’ida wa narahu kariba.” (Hakika wao wanaiona iko mbali, na sisi tunaiona iko karibu 70:6 -7).

# NAHJUL BALAGHA

## JUZUU YA PILI

### MTARJUMI: HARUNA PINGILI

## 101 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

### NAYO NI KHUTBA MOJAWAPO AMBAYO NDANI YAKE KUNA MAELEZO YA MAPAMBANO YA KIVITA

“Mstahiki wa sifa ni Mungu ambaye ni wa mwanzo kabla ya chochote. Na wa mwisho baada ya kila kitu. Na kwa umwanzo Wake imelazimu iwe hakuna kilichomtangulia. Na kwa umwisho wake imelazimu iwe hakuna wa mwisho ila ni Yeye. Ninashuhudia kuwa hapana mungu ila ni Allah (tu) wazi wazi na kwa siri, kwa moyo na kwa ulimi.

“Enyi watu! Kunikhalifu kwenu na kuniasi kusiwafanye mnikadhibishe, wala msishawishike kuniasi, wala msikonyezane kwa macho mnaponisikiliza.

Ninaapa kwa ambaye ameipasua mbegu na kumuumba mwanadamu kuwa ambayo nimewaambieni ni kutoka kwa Nabii Al’ummiyyi **(s.a.w.w)**, Wallahi mfikishaji hakusema uwongo, wala msikilizaji hakuwa mjinga[1].

Kana kwamba namuona na namuangalia mpotovu mno[2] amepiga kelele Sham (Syria) na amesimika bendera zake mpakani mwa Kuufani - (ni jina la mji wa Kufa) - afunguapo kinywa chake na kushika kasi ukaidi wake na ujeuri (yaani dhulma) wake ardhini kuwa nzito, fitna itawang’ata watu kwa meno yake, na vita mawimbi yake yatachafuka, na siku zitadhihirisha kisir- ani chake, (zitakuwa ngumu) na usiku taabu zake.

Matunda yake yakipevuka, na akianza kuyachuma, na ngamia kuunguruma, na mikuki na panga kumwetuka, fitna korofi itachukuwa nafasi, na itakuwa kama usiku wa giza, na bahari yenye kupigapiga mawimbi yake.

“Hii ni mara ngapi mji wa Kufa unaharibiwa na dhoruba, na kupitiwa na kimbunga. Hivi punde karne itapambana na karne[3], mazao yaliyosimama yatavunwa na yaliyovunwa yataharibiwa![4]”.

---

1. Mfikishaji na msikilizaji ni yeye mwenyewe (a.s).

2. Mpotovu mno ni: Mwenye kukithiri upotovu, na hapa ni kinaya yamaanisha Abdul Malik bin Marwan; kwa kuwa sifa hizi zakamilika kwake kuliko kwa mwingine.

3. Karne kupambana na karne ni kinayah - yaani dola ya Bani Abbasi itakapojipatia ushindi itakapo pambana dhidi ya dola ya Bani Umayyah. Na karne mradi wake hapa ni kizazi katika watu, mapambano yalikuwa kati ya viongozi wa fitna na watu wa haki, kama wanavyopambana beberu kwa pembe zao wanapoparurana, na wema uliobaki ulivunwa, na uliokwishavunwa ulivurugwa na kuharibiwa na wala haitobakia ila ni shari ya jumla na balaa kamili endapo haki haikupata wakuinusuru.

4. Ni kinaya, yamaanisha kuuliwa kwa watawala katika Bani Umayyah vitani, kisha kuuliwa mateka katika wao, hali ni kama hivyo ilijiri kwa Abdullah bin Ali na Abil’Abbas Assafahi.

## 102 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

### KUHUSU MAUDHUI ILEILE YA SIKU YA KIYAMA

"Hiyo ni siku ambayo Mungu atawakusanya waliokuwa kwanza na wa mwisho ili kudodosa hesabu, na kulipwa aamali, wakiwa wanyenyekevu, wamesimama, jasho limewafunga hatamu[1].

Na ardhi ikawatetemesha[2], basi mwenye hali nzuri katika wao ni mwenye kuipata nafasi kwa ajili ya nyayo zake, na wasaa kwa yeye kuweza kupumua."

### NA SEHEMU YA KHUTBA HIIHII KUHUSU TAABU ZA SIKU YA KIYAMA

"Ni fitna kama giza la usiku, hakuna kikundi kitachosimama kupambana nayo wala bendera zao kurudishwa nyuma. Atakujieni (hiyo saa) mfano wa ngamia aliyetayari akiwa na hatamu yake na zana zake, muongozi wake yuamhamasisha[3], na mpandaji wake anambidiisha[4], watu wake wachocheao vita - mashambulizi yao ni makali, uporaji wao ndio kidogo[5]. Wanaopigana vita katika njia ya Mungu ni kaumu dhalili mbele ya wenye kiburi[6], wasiojulikana aridhini, na maarufu mbinguni. Ole wako ewe Basrah, pindi kipigo cha adhabu ya Mungu kitapokuangukia! Hakina vumbi wala sauti, watu wako watakabiliwa na umauti mwekundu na njaa yenye rangi ya vumbi.[7]".

## 103 - MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

### KUHUSU KUJIEPUSHA NA TAMAA ZA DUNIA

"Enyi watu! Itazameni dunia mtizamo wa watawa wanaojiepusha nayo, wenye kuigeuzia uso, kwa kweli Wallahi ni punde tu itawaondoa wakazi walioifanya maskani, na kumfadhaisha anayeishi kwa anasa na mwenye kujiamini, kilichogeuka na kiendacho kuzimu hakitorudi, na ambacho kinatarajiwa kuja hakina uhakika, furaha yake ni mchanganyiko na huzuni,

---

1. Jasho limewafunga hatamu: Yaani jasho limewatiririka mpaka kufikia eneo la hatamu kwa mnyama; nalo ni mdomo.

2. Ardhi kuwatetemesha: Ni kwamba ardhi itatikisika na kuyumba nao.ya msafara.

3.Yaani anamsukuma kumuhimiza aingiye kwenye nyumba zenu,na kwenu ndio mafikio.

4. Anambidiisha: Anampeleka mwendo zaidi kuliko uwezo wake, na makusudi ni kuwa watu wa fitna wanajitahidi kuchochea moto wake, wakiwa na askari waendao kwa miguu na wapanda farasi, kwa hiyo waenda kwa miguu amemkusudia kiongozi, na wapanda farasi, amekusudia wapandao farasi miongoni mwa askari.

5. Uporaji wao ni mdogo:Yaani kichukuliwacho na muuwaji katika nguo za aliyeuliwa na silaha yake katika vita, yaani si miongoni mwa matajiri.

6. Ni sifa ya waumini.

7. Umauti mwekundu: Ni kinaya mradi wake ni janga na njaa, na limeitwa mauti mekundu kwa sababu ya ukali wake, na njaa imeelezwa kuwa ni ya rangi ya vumbi ni istiari ya ukame, kwa sababu mwenye njaa anaoiona pambizo kana kwamba ina vumbi na giza. Na njaa ya rangi ya vumbi: Ni kinaya ya mahali na ukame.

na watu imara wenye nguvu wanaelekea kwenye ulegevu na udhoofu. Hivyo basi msighurike na mengi yanayokufurahisheni humo kwa sababu ya uchache wa yatakayofuatana na nyinyi kutokana nayo.

"Mungu amrehemu mtu ambaye ametafakari na kujifunza humo, amejinfunza na kufanikiwa mwangaza. Kana kwamba ambacho kipo katika dunia hii kwa muda mfupi kitakuwa kama hakijakuwa. Kama kwamba ambacho kipo katika akhera baada ya muda mfupi kitaonekana kama kwamba hakijakosa kuwa. Kila kihesabiwacho kitatoweka, na kila kitazamiwacho kinakuja. Na kila kinachokuja kimekurubia."

## SEHEMU YA KHUTBA HII HII KUHUSU SIFA ZA MWANACHUONI

"Mwanachuoni hasa ni yule mwenye kuitambua thamani yake, yatosha kwa mtu kuwa yu-mjinga kwa kutoijua thamani yake. Kwa hakika miongoni mwa watu awachukiao mno Mwenyeezi Mungu ni yule mja aliyemuachia mambo yake yeye mwenyewe. Anakwenda kombo mbali na njia iliyo sawa, anakwenda bila ya dalili, aitwapo kwenye shamba la dunia atafanya, na aitwapo kwenye shamba la akhera atakuwa mvivu, kana kwamba alilofanya ni wajibu juu yake, na kana kwamba alilolifanyia uvivu si wajibu juu yake."

## SEHEMU YA KHUTBA HII HII KUHUSU WAKATI WA BAADAYE

"Huo ni wakati ambao hatookoka kutoka humo isipokuwa aliye na usingizi sana[1], akiwa yupo hatambuliki, na akighibu, hakosekani, hao ndio taa za mwongozo na alama za misafara ya usiku, si wasambazaji wa masingizio wala si watoboa siri.

Hao Mungu atawafungulia milango ya rehema Zake, na atawaondolea madhara ya adhabu Zake [2] . "Enyi watu! Zitakujieni zama uislamu utapinduliwa juu chini kama ambavyo chombo kifunikwavyo pamwe na kilicho ndani yake.

Enyi watu! Kwa hakika Mungu amekulindeni kwa maana ya kuwa hatowadhulumu, wala hakuwalindeni kwamba hatowafanyieni mtihani[3], na amesema Mtukufu katika wasemaji:[4] "Hakika katika hayo yapo mazingatio. Na kwa yakini. Sisi ni wenye kuwafanyia mitihani." (23:30).

Ar–Radhiy (r.a) amesema: Ama kuhusu kauli yake (a.s): "Kullu mu'minin nuwamatin" Kila muumini mwenye kulala sana, amekusudia kwa hilo: yaani yule muumini asiye kumbukwa au asiyetajika, na si mtu wa shari.

---

1. Mwenye usingizi mwingi anamkusudia aliyembali na kujishirikisha na watu wa shari katika shari zao, wamuonapo hawamjui kuwa ni katika wao, na anapoghibu hawamkosi.

2. Na imeelezwa hivi: Kupitia wao Mungu atafungua milango ya rehema yake, na kupi- tia wao ataondoa madhara ya adhabu yake, (yaani kwa baraka zao kheri itakuwapo na shari itatoweka).

3. Ili abainike mkweli mbali na muongo, na mukh'liswi na mwenye shaka, kwa hivyo Mungu atakuwa na hoja dhidi ya viumbe Wake.

4.Yaani kwa kuwa Yeye (s.w.t) watu wanapoharibika hawalazimishi wawe wema, bali huwaacha kama walivyochagua ikiwa mtihani kwao.

Na al-Masayiihu: Ni wingi wa neno misyahun, naye ni chakubimbi aendaye kwa huyu na kwa huyu ili kufanya ufisadi (umbea). Al-Madhayyiiu: Ni wingi wa midh'yaun, naye ni ambaye asikiapo baya la mwenzake analitangaza na kulieneza.

**Ufafanuzi**

Usemi wake (a.s): "Mwanachuoni ni yule ambaye ameijua Qadiri yake," ni miongoni mwa mithali mashuhuri kutokana naye (a.s) na wamesema watu baada yake na wamekithirisha, mfano wa kauli yao: 'Ikiwa hutoijua Qadiri ya nafsi yako, kwa hiyo Qadiri ya mwingine hautoijua kabisa.'

Na mfano wa kauli yao: 'Ambaye hajui Qadiri ya nafsi yake, watu watakuwa hawana kosa endapo watakuwa hawamjui.'

Na miongoni mwa maneno yaliyoelezwa kutoka kwa Abi Abdillah as-Sadiq (a.s) katika riwaya marfu'u: "Ma halakamru'u arifa Qadrahu" yaani hatohiliki mtu aliyeijua Qadiri yake - riwaya hii ni ya Abul'Abbas kutoka kwake katika Al'Kaamil. Na katika Hadithil-Marfu'u:

## 104 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Khutba Zake (a.s) –

### MWANZO WA KHOTUBA HII UMETANGULIA KATIKA NAMBA 33.

"Sasa basi! Kwa kweli Allah (s.w.t) alimtuma Muhammad **(s.a.w.w)** wakati hapakuwa na yeyote katika waarabu aliyekuwa akisoma kitabu, wala kudai unabii wala wahyi (ufunuo).

Na alimpiga vita aliyemuasi akisaidiwa na wanaomtii, akiwaongoza kwenye uokovu wao, na anawaharakishia saa isije kuwashukia[1], anashindwa mwenye kushindwa, na anasimama aliyevunjika[2] anamsimamia mpaka amfikishe kwenye lengo lake[3].

Isipokuwa aliyeangamia asiye na kheri, mpaka alipowaonesha uokovu wao, na aliwakalisha mahali mwao, mambo yao yakaenda sawa, na yalitengenea.

Naapa Mungu, kwa kweli nilikuwa miongoni mwa waswagaji wake[4] - mpaka walirudi nyuma wote, na kujikusanya kwenye kamba yao, sikuonyesha

---

1. Anawaharakishia saa: Yaani kana kwamba alikuwa akiogopa wasije wakatanguliwa na saa ya kiyama, kwa hiyo anaharakisha kwa kuwaongoza kabla haijafika, nao wakiwa katika upotovu wao.

2. Alievunjika: Yaani mwenye kudhoofu itikadi yake, au azma yake kuwa butu, na akanyo'ngea mwendo wake katika njia ya waumini, au wasiwasi umejipenyeza na kuivunja miguu ya hima yake, kwa kuitikisa itikadi yake, kwa kweli Nabii (s.a.w.w) alikuwa anajishughulisha kumuangalia na kumtibu mpaka aepukane na maradhi yake haya, na aungane na walio wanyoofu, isipokuwa aliyepungukiwa na utayarifu mwenye asili mbaya, dawa kwa huyu haitokuwa na mafanikio, kwa hiyo anahiliki.

3. Mpaka amfikishe kwenye lengo, nalo ni itikadi ya haki, na utulivu wa nafsi kwenye Uislamu. Na hiyo ndiyo maana ya kauli yake ijayo: "wa bawa'ahum mahalatahum.

4. Mswagaji: Kutokana na neno saaiqu makusudi ni yule anaye liswaga kundi la wanyama kwa mfano mbuzi au 'ngombe na mradi wake ni: Ujahiliyah aliufanya mfano wa kundi la ng'ombe lililokutana kwa bahati na kundi la uislamu, kwa hiyo yeye akaliandama kulishambulia kwa upanga wake mpaka lilipokimbia na kutokomea.

udhaifu au kutokuwa na hima, au kuhini wala sikuonyesha unyonge, namuapa Mungu nitaitumbua batili mpaka niitoe haki kutoka kiunoni mwake!”

Sayyid Ar-Radhiy (r.a) amesema: Yaliyoteuliwa katika khutba hii yametangulia, ila tu mimi nimeikuta katika riwaya hii kukiwa na tofauti na iliyotangulia, kati ya ziada na upungufu, kwa hiyo hali imewajibisha kuithibitisha tena.

# NAHJUL BALAGHA

## JUZUU YA PILI

### MTARJUMI: HARUNA PINGILI

## 105 - MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

### KUHUSU BAADHI YA SIFA ZA NABII MTUKUFU NA KEMEO KWA BANI UMAYYAH NA MAWAIDHA KWA WATU

"Kisha Mungu alimtuma Muhammad **(s.a.w.w)** ili awe shahid[1]na mbashiri na muonyaji, ni mbora katika viumbe akiwa mdogo, na mwenye heshima mno akiwa mtu mzima, na msafi mno katika wasafi wa tabia, na ni mkarimu mno kwa wenye kumuomba[2].

Dunia haikuwa tamu katika ladha yake kwenu. Wala hamkuweza kunyonya chuchu zake ila mlipokuta hatamu zake zimelegea.

"Kisha alisema kuwa wao wameikuta dunia kwa bahati imekwisha kuwa ngumu kwa atakayeitawalia utawala wa haki kama anavyokuwa mgumu ngamia kwa mpandaji wake endapo hatamu yake itajikusanya, haudaji yake haitulii kwa mpandaji, haramu zake zapatikana kiurakhisi kwa aipendaye.

Ni mfano wa mti wa msidiri uliokatwa miba yake, kwa hiyo ukawa laini wateleza; na halali zake hazipo tena kwa kushindwa na haramu; na kwa kuwa umezagaa umechukua nafasi kulingana naye; na hii ni ishara kwenye aliyokuwa akiyasema daima kwa kujitwalia kwao binafsi suala la ukhilafa makhalifa waliomtangulia mbali naye, kuwa yeye alikuwa msitahiki.

"Kunyonya kiwele chake ila baada ya kumkuta kwa bahati hatamu yake ya puani inajiburura na ukanda wake wa ngozi umelegea. Uharamu wake umekuwa kwa kaumu ya watu kama msidiri ulionepa (kwa uzito wa matunda) hali ikiwa uhalali wake ni mbali, haupo.

Wallahi, mngeikuta kama kivuli kirefu, mpaka muda uliopangwa.

---

1. Maana ya kuwa shahidi ni: Yeye atatoa ushahidi nini umma ulichofanya kati ya utii au maasi.

2. Yaani Nabii (s.a.w.w.) ni mwenye kheri nyingi mno kati ya watu kwa wamuombao, anasema Amirul-Mu'minina (a.s) akiwasemesha watu wa zama zake miongoni mwa masahaba waliobaki na watu wengine miongoni mwa taabiina ambao hawakuwa zama za Mtume (s.a.w.w.): Kuwa Mungu (s.w.t) alimtuma Muhammad, akiwa mwenye heshima sana katika watu kwa tabia, na mwenye mkono wa ukarimu mno, na mbora kati yao akiwa mtoto na mwenye heshima akiwa mtu mzima. Hivyo anakuwa Mungu amemhifadhi siku za maisha yake ili amfungulie dunia, alimpa heshima kwa ajili hiyo, kwa hiyo nchi hazikukombolewa, wala haikupatikana mali kwa wingi,wala dunia haikuelekea upande wenu; wala dola hazikuwa chini yenu isipokuwa baada yake. Hivyo mliweza kuila na kustarehe nayo, kama awezavyo mkamaji kumkama ngamia, na ladha yake kuwa tamu kwenu na maisha yamekuwieni mema na mmeyakuta mazuri yenye kustawi.

Kwa hiyo ardhi kwenu ni tupu[1], na mikono yenu humo imekunjuka, na mikono ya viongozi imefungwa mbali nanyi. Panga zenu zimewadhibiti[2] na panga zao zimezuilika dhidi yenu[3].

Jueni kuwa kwa kila damu iliyomwagwa ina kisasi, na kila haki ina mdai, na mdai kisasi wa damu yetu ni sawa na hakimu anayetoa hukumu kuihusu haki yake binafsi[4], huyo ni Mungu ambaye hamshindwi amtakaye, wala hamkosi atakayemkimbia.

Namuapa Mungu Enyi Banii Umayyah! baada ya muda mfupi mtaiona nafasi yenu ikiwa mikononi mwa wengine, na nyumbani mwa adui yenu! Jueni kuwa macho yaonayo sana miongoni mwa macho ni yale yaliyopenya kuiona kheri! Jueni kuwa masikio sikivu ni yale yaliyoelewa mawaidha na kuyakubali![5]".

## KUHUSU SHUGHULI ZA IMAM

"Enyi watu, chukueni mwanga kutoka mwenge wa taa ya muwaidhi mwenye kuwaidhika[6],kunyweni na chukueni maji kutoka chemchemi iliyohifadhiwa na kusafishwa bila uchafu[7].

"Enyi waja wa Mungu! Msiutegemee ujahili wenu, wala msiutii utashi (mbaya) wa nafsi zenu kwa kuwa yule mwenye kuwasili kwenye nyumba hii[8] yupo kwenye ukingo wa kuzolewa na maji yazoayo kila uchafu[9] ananakili[10] maangamizi mgongoni kwake kutoka sehemu (ya mgongo) mpaka sehemu, kwa rai aizushayo baada ya rai; anataka kuambatanisha kisichoweza

---

1. Ardhi tupu: Isiyokuwa na ulinzi, isiyokuwa na mwenye kuihami baada ya kutumwaNabii (s.a.w.w) isipokuwa ninyi wenyewe.

2. Yaani: Panga zenu zimewadhibiti Ahlul-Bayt ambao ndio viongozi na maraisi.

3. Kana kwamba alikuwa anaishiria mauaji ya Imam Husain na watoto wake yatakay- otokea, na kana kwamba Imam Ali (a.s) alikuwa anayaona kwa macho wazi wazi.

4. Mwenye kudai kisasi cha damu yetu atapata kisasi chake bila shaka, yaani ni kama aliyejihukumu mwenyewe, hakuna anayehukumu juu yake hata amzuiye.

5. Yaani: Jicho lenye kutambua sana ni lile linalotambua kheri, na sikio lenye kudiriki sana ni lile lenye kuhifadhi wa'adhi na kuukubali.

6. Amejaalia kwamba mtoa wa'adhi mwenye kuwaidhika, kwa sababu asiyewaidhika binafsi ni vigumu mwingine awaidhike naye, na amekusudia kwa taa hii, ni yeye mwenyewe (a.s) binafsi.

7. Kunyweni maji kwa ajili ya kupoza kiu zenu kutoka chemchem safi, nayo ni chemchem ya elimu zake.

8. Nyumba ya kuutegemea ujahili na kuutii utashi danganyifu wa nafsi.

9. Nyumba hii: Yaani amefikia mahali pa kuporomokea kwenye maangamizi.

10. Ananakili: Yaani yeye akinakili hubeba maangamizi na anayabeba kutoka sehemu hadi sehemu ya mgongo wake, na anaubeba daima, anataabika kuunakili juu chini kati kwa rai na bid'a zake, hivyo yeye katika kila rai ananakili kutoka ujinga na kwenda upotovu kwa namna ambayo msingi wa yote ni ujinga na matamanio mabaya ya nafsi.

kuambatana, na kukisogeza karibu kisicho weza kusogea! Ala ala muogopeni Mungu msimlalamikie huzuni zenu yule asiyeweza kuzitanzua, wala hawezi kutangua kwa rai yake lililo lazima juu yenu.

Na kwamba si juu ya Imam isipokuwa alilobidiishwa miongoni mwa amri za Mola Wake Mlezi: Kufikisha mawaidha, na kujitahidi kutoa nasaha, na kuihuisha Sunnah, na kuitekeleza adhabu kwa wanaostahili, na kuzirudisha hisa kwa wenye kustahiki. Hivyo basi harakishieni elimu kabla ya mmea wake haujakauka, na kabla hamjashughulishwa na nafsi zenu mbali na wenye kuwa nazo. Katazeni maovu na wenyewe muwe mmejikataza, mlichoamriwa ni kukataza baada ya kujikataza!.

## 106 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

### HUMO ANABAINISHA UBORA WA UISLAMU, NA AMTAJA MTUKUFU MTUME (S.A.W.W) KISHA ANAWALAUMU SAHABA ZAKE:

“Shukrani zote anastahiki Allah (s.w.t), ambaye ameifanya sharia ya kiislamu na kuifanya nyepesi kwa mwenye kuiendea, na ameziimarisha nguzo zake dhidi ya mwenye kutaka kuushinda, na akaufanya kuwa ni amani kwa wenye kujiambatanisha nao, na salama kwa mwenye kuingia – (yaani hapigwi vita akishaingia uislamu), na hoja kwa mwenye kuueleza, na ni shahidi kwa mwenye kugombana kwa ajili yake, na ni nuru kwa mwenye kujiangaza nao, na ni fahamu kwa mwenye kutumia akili, na ni busara kwa mwenye kuzingatia, na ni alama kwa mwenye kuchunguza, na ni uelewa kwa mwenye kuazimia, na ni funzo kwa mwenye kuwaidhika, na ni uokovu kwa mwenye kusadiki, na ni ithibati kwa mwenye kutegemea, na ni raha kwa mwenye kuitumainia, na ni kinga kwa mwenye kusubiri.

Ni njia maarufu iliyo wazi mno na maingilio yaliyo wazi na ni mnara wa juu, na ni njia iliyo dhahiri, ni taa ziwakazo, ni mahali pa kujivunia, bendera iliyoinuka, yenye kukusanya farasi, ni pa kushindania washindani, mtukufu wa washindi wa farasi.

Wapandaji wake ni wenye kuheshimiwa, kusadiki (Mungu, Mtume…) ndio njia yake, vitendo vyema ndio minara yake, umauti ndio lengo lake[1], na dunia ni kiwanja chake cha mafunzo, na kiyama ni farasi wake, na pepo ni malipo yake ya mashindano.

### NA SEHEMU YA KHUTBA NI KUMUELEZA NABII (S.A.W.W):

1. Anakusudia umauti ni umauti wa kuwa mbali na matamanio ya kinyama, na maisha ya furaha ya daima kama ijulikanavyo kutoka na kauli yake (Rafi’ul-Ghaayati) vinginevyo, umauti ulio maarufu ni lengo la kila kilicho hai, au linakuwa maana (wal-mautu ghaayatuhu): Yaani dunia ni jela ya mu’mini, na umauti unamtoa kutoka kwenye jela hiyo, na anapata hadhi ya furaha ya kudumu.

“Mpaka aliwasha mwenge kwa autakaye[1], na aliangaza mwanga kwa mahabusi[2], hivyo basi yeye ni muaminifu wako wa kuaminika, na shahidi wako siku ya malipo, na ni muwakilishi wako akiwa neema, na ni Mtume wako wa kweli akiwa ni rehema.

“Oh Allah! Umgawiye fungu katika uadilifu Wako, na umpe jazaa ya kheri nyingi katika fadhila Zako. Oh Allah! Lirefushe jengo lake zaidi kuliko majengo ya wajengao, na umkirimu mafikio yake Kwako.

Itukuze kwako daraja yake, mtunukie wasila na heshima maalumu na ubora, na tukusanye sisi katika kundi lake, bila ya fedheha wala wenye kujuta, wala wenye kupetuka njia, wala wenye kutengua ahadi, wala wenye kupotea wala wenye kupoteza, wala walioshawishika kwa maovu!”

**Ar-Radhiy (R.A) Amesema:**

Maneno haya yamepita katika habari zilizotangulia, isipokuwa sisi tumeyakariri hapa kwa sababu ya tofauti iliyopo kati ya riwaya hizi mbili.

### MIONGONI MWAYO AKIWAHUTUBIA SAHIBA ZAKE

“Kwa ukarimu Wake Mungu (s.w.t) mmefikia daraja ambayo wanahishimiwa hata vijakazi wenu, na majirani zenu wanatendewa vyema, na anakuheshimuni ambaye hamna fadhila yeyote juu yake, wala hamna hisani juu yake. Na anawahofuni asiyekuwa na maalumati ya kuwa mmepata kumshambulia, wala kuwa na mamlaka juu yake.

Mnaziona ahadi za Mungu zinatenguliwa wala hamkasiriki, hali ninyi mwasumbuka kwa kutanguliwa mila za babu zenu. Na mambo ya Mungu yalikuwa yanakuja kwenu, na yanatokea kwenu, na kwenu yanarejea[3].

Mmewawezesha madhalimu sehemu zenu, na kuwaachia majukumu yenu, na mmeweka mambo ya Mungu mikononi mwao. Wanatenda kwa shaka, na wanakwenda katika utashi mbaya wa nafsi. Naapa Mungu hata wangekutawanyeni chini ya kila nyota, Mungu angewakusanyeni katika siku mbaya mno kwao!”.

## 107 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

At-Tabari ameieleza katika Ta’arikh yake katika matukio ya mwaka wa 37 H.A., na Ibn Muzahim katika Swifiin, uk. 256.

### BAADHI YA SIKU ZA SIFFIIN

“Kwa kweli nimeona kukimbia kwenu na kutawanyika kwenu mbali na safu zenu za vita, mkizungukwa na watu fedhuli na duni, na mabedui wa (Shaam)

---

1. Autakaye: yaani atakaye kupata mwanga wa taa, mwenye kuchukua moto kutoka moto mwingi, na mradi wake ni mwongozo katika dini, na ya kuwa Nabii aliwafaidisha watafutao haki ambayo kwa ajili yake watapata mwanga ili wafichue.

2. Yaani Mtume (s.a.w.w) aliipa mwanga alama kwa ajili ya aliyemfunga, yaani alisimamisha kwa ajili ya aliyemfunga ngamia wake kwa sababu ya kupotea - alama ili aongoke kwayo, yaani aliweka moto juu ya kilele cha mlima ili amuokoe kutoka kwenye kuchanganyikiwa kwake.

3. Yaani hukumu za kisharia zinawajieni kutoka kwangu na miongoni mwa mafunzo yangu kwenu, kisha yanatoka kwenu na kuwaendea mnaowaelimisha nayo, kisha yarejea kwenu ili wajifundishe watoto wenu na ndugu zenu kutoka kwa hao wanachuoni.

Syiria, ingawaje ninyi ni watangulizi katika waarabu na ni kilele cha utukufu na kilele cha ubora, na mna daraja ya juu mfano wa ile ya pua, na ule wa nundu kubwa ya ngamia.
Uhemaji wa moyo wangu utapoa tu niwaonapo mnawazunguka kama walivyokuwa wamewazungukeni, na mnawaondoa mahali mwao kama walivyokuondoeni, mkiwauwa kwa mishale na kuwachoma kwa mikuki, hivyo msitari wao wa mbele uangukie juu ya msitari wao wa nyuma, kama ngamia walioshikwa na kiu waliofukuzwa kutoka kwenye manyweo yao, na kuzuiliwa maendeo yao ya kunywea maji!".

# NAHJUL BALAGHA

## JUZUU YA PILI

### MTARJUMI: HARUNA PINGILI

## 108 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

Zamakhshari ameieleza katika Rabi'ul-Abrar, Jz. 1, mlango wa 'kubadilika kwa hali'.

### NAYO NI KHUTBA YA HALI YA MABADILIKO, YAANI MATUKIO MAKUBWA VITANI

"Mstahiki wa sifa njema ni Mungu Aliye dhahiri kwa viumbe Wake kupitia viumbe wake[1], na mwenye kudhihiri nyoyoni mwao kwa hoja Zake[2], ameumba viumbe bila ya kufikiri, kwa kuwa kufikiri hakumfalii isipokuwa wenye kuwa na dhamiri[3], naye si mwenye dhamiri[4], elimu yake imepenya mpaka ndani ya siri zisizojulikana, na kuzingira itikadi za ndani za siri."

### NA SEHEMU YA KHUTBA HII NI MAELEZO KUHUSU NABII (S.A.W.W)

"Mungu (s.w.t) amemchagua kutoka mti wa nasaba ya manabii[5], na kutoka mwale wa mwanga, na ni miongoni mwa nywele za utukufu wa kipaji cha uso, kutoka sehemu bora mno katikati ya bonde la Bat'ha'a[6], na taa za kuangazia gizani, na chemchemi za siri za hekima."

Miongoni mwayo: "Yeye - yaani Nabii **(s.a.w.w)** alikuwa mfano wa tabibu anayezunguka na tiba yake, aliyeimarisha marhamu yake, azungukaye na aliye tayari na dawa zake, na amekwisha koleza mawasimu zake[7]. Anazitumia mahali ambapo ipo haja, ili kuziponya nyoyo za vipofu, na masikio ya viziwi na ndimi za mabubu, kwa dawa zake hufu- atilia mahali ulipotawala mghafala na mahali penye mashaka na matata.

Hawakufaidika na mwanga wa hekima zake, na wala hawakuwasha moto kutoka jiwe la elimu litoalo cheche; Hivyo basi wao katika hilo ni kama

---

1. Maadamu dalili za kuthibitisha kuwepo kwa muumba ziko dhahiri kama jua, amemueleza (a.s) Mungu (s.w.t) kuwa amedhihiri na kujitokeza kwa viumbe Wake, na kilichowajulisha kuwepo Kwake ni viumbe Wake na kule kuwaumba Kwake wao.

2. Na mwenye kudhihiri nyoyoni mwao: Unaona hakusema machoni mwao, kwa sababu haonwi (s.w.t) kwa macho, huonwa (s.w.t) kwa nguvu za uoni wa kiroho.

3. Mradi wa wenye dhamiri hapa, ni wenye nyoyo.

4. Amemkanushia kuzingatia na kufikiri; kwa kuwa hilo huwa kwa wenye dhamiri na nyoyo wenye upinzani tofauti.

5. Mti wa nasaba ya manabii ni wana wa Ibrahim (a.s) kwa kuwa manabii (wengi) wame- toka kwenye kizazi chake Ibrahim (a.s).

6. Surrat–ul-Bat'ha'a: Ni katikati ya Bat'ha'a na ni eneo ambalo walikuwa wanaishi makabila ya makuraishi, na walikuwa wakiitwa Maqureishi wa Bat'ha'a.

7. Mawasiimu: Ni vyuma vitumikavyo kuwaweka alama wanyama kwa mfano farasi na aina nyingine za wanyama kama vile ng'ombe nk.

wanyama watafunao nyasi, na mawe magumu. Siri zimefichuka kwa wenye kufahamu[1] njia ya kweli imekuwa wazi kwa wale wasiokuwa na mwongozo na saa ikurubiayo imeondoa kifuniko usoni pake, na alama zimeonekana kwa wanaoangalia kwa makini.

Nimekuwaje mimi! Nawaoneni (mko) miili isiyokuwa na roho, na roho bila ya miili[2], wafanya ibada bila wema[3], na wafanyibiashara bila ya faida[4], wako macho hali wamelala[5],wanatazama hali ni vipofu, wanasikia hali ni viziwi na wanaongea hali ni mabubu!.

## MIONGONI MWAYO

"(Nimegundua kuwa) Kuna bendera ya upotovu imejiimarisha katikati, na imetawanyika na watu wa kabila lake, inakupimieni kwa kilo yake[6], na kuwachanganyeni na uzito wake.

Kiongozi wake yuko nje ya mila (ya kiislaamu) yupo katika upotovu, siku hiyo hatobaki miongoni mwenu ila ni kama mabaki ya chungu[7] au vumbi kama vumbi lililokung'utwa kutoka kwenye kipeto[8]. Hivyo basi itakusugueni kama isuguliwavyo ngozi, na itakukanyageni mkanyago wa mazao yaliyovunwa, na itamdonoa muumini kati yenu kama anavyodonoa ndege punje nene kati ya punje nyembamba.

Madhehebu yanawapelekeni wapi, na giza linawafanya mtangetangie wapi! Na mnapelekwa wapi na matarajio! Kutoka wapi mwaletwa, na mwadanganyiwa wapi? Kila muda una maelezo ya maandishi, na kila aliyetoweka ni lazima arudi, hivyo basi wasikilizeni viongozi wenu wa kiungu, na zihudhurisheni nyoyo zenu, na amkeni atakapowapigieni kelele. Mtangulizi inambidi aongee la ukweli kwa watu wake.

---

1. Imefichuka yaani siri imeinyenyekea nuru ya ufahamu kwa hiyo (hii nuru) inaifichua na kuimiliki, na wenye fahamu wanaitumia siri wapendavyo.

2. Miili bila ya roho: Yaani watu bila ya roho wala akili, na roho bila ya miili: Inawezekana anakusudia wepesi (wa kichwa) mfano wa roho bila ya mwili, na yawezekana anakusudia kupungua kwao (akili).

3. Ibada bila wema: Amewanasibisha na unafiki.

4. Biashara bila faida: Amewanasibisha na riya'a. Biashara bila faida: Ni ishara ya unafiki.

5. Wako macho usingizini: Yaani wao wako macho, hali wameghafilika na ukweli kama waliolala, hali ni hiyo hiyo katika ibara zinazofutia.

6. Maana inakuwa: Inakubebesheni dini na da'awa yake. Na yawezekana awe anakusudia kwa kauli yake: 'Anakupimieni kwa kilo yake;' watu wake wanakulazimisheni kuingia kwenye jambo lao, na wanakuchezeeni, wanakuinueni wanakuteremsheni kama afanyavyo mpimaji wa ngano kwayo apimapo kwa pishi yake - pishi ni kipimo kiasi cha ujazo wa kg.3 na zaidi kidogo, au ikuchukueni kwenda kuhiliki jumla kama mpimaji apelekapo ana-chokipima miongoni mwa punje.

7. Mabaki ya chakula ndani ya chungu kilichokwishapakuliwa (ukoko ukitaka) na mradi wake hapa ni watu duni wa hali ya chini.

8. Ni kinachodondoka baada ya kukung'uta, na mradi ni kinachobakia baada ya kumwa-ga.

Yampasa azikusanye azma zake na fikra zake ili aangalie, fahamu zake aziweke hadhiri, suala ameliatua uatuaji wa tundu la kizuizi cha vazi, na ameliparua uparuaji wa ulimbo [1] (kutoka kwenye kijiti cha mti na kuondolewa). Wakati huo batili itachukuwa nafasi yake, na ujahili utapanda kipando chake, utovu wa nidhamu utakuwa mkubwa, na wito utakuwa mdogo, na wakati utavamia uvamiaji wa mnyama mkali, na dume la ngamia litakoroma baada ya ukimya, na watu watakuwa ndugu katika maovu, watahamana kwa dini[2]. Watapendana katika uwongo, na watachukiana kwa sababu ya ukweli.

Hali ikiwa ni hivyo mtoto atakuwa chukizo[3] - (yaani atakuwa sababu ya kuchukiza badala ya kuwa kitulizo cha jicho kwa wazazi wake) na mvua - (sababu ya joto), uovu utajaa mno, na maadili mema yatatoweka, na watu wa zama hizo watakuwa mbwa mwitu, na masultani wao ni kama wanyama wavamizi, na watu wao wa hali ya kati watakuwa walafi, na mafakiri wao ni maiti, ukweli umedidimia, na uwongo umefurika, na upendo utakuwa wa maneno, hali watu wakiwa wanagombana kimoyo, na uzinzi ni nasaba, na usafi wa kutozini ni ajabu[4], na uislamu utavaliwa kama ngozi juu chini.[5]".

## 109 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Khutba Zake (a.s) - Az-Zamakhshariy ameieleza katika Rabi'ul-Abrar katika mlango wa Malaika, na ibn Abdi-Rabih katika al-Iqdu al-Farid, jalada la 4, uk. 76.

Katika kubainisha Qudra ya Mungu (s.w.t) na kuwa Yeye ni wa pekee katika utukufu na wa pekee katika suala la kuwarejesha hai viumbe Wake: "Kila kitu chamnyenyekea Yeye, na kila kitu huwa kwa kupitia kwake Yeye: Yeye ni toshelezo la kila fakiri, na hadhi kwa kila mnyonge, na nguvu ya kila dhaifu, na kimbilio la kila mwenye kuvunjika moyo.

Mwenye kuongea anamsikia tamko lake, na mwenye kunyamaza anajua siri yake, na kwa anayeishi riziki ni juu yake, na anayekufa Kwake ndio marejeo.

"Macho hayajakuona hata yawe na uwezo wa kueleza habari zako, na ulikuwa kabla ya waelezaji miongoni mwa viumbe Wako.

---

1. Suala ameliatua: Yaani ameliatua huyu mliganiaji wa kiungu suala kwenu kama inavyoatuliwa chaza na kujulikana kilicho ndani, na kama unavyomenywa mti na utomvu kutolewa. Na amelitaja hili husussan kwa sababu utomvu utolewapo hakuna athari inayobakia, hivi ndivyo walivyosema.

2. Watahamana kwa dini: Yaani watafanyiana uadui na kutengana, na mradi wake ni: Mtu wa dini kwao ni wa kuhamwa na kutengwa.

3. Yaani kwa sababu ya watoto kukithiri kutowatii wazazi wao mvua itakuwa haba, yasemekana hiyo ni miongoni mwa alama za saa Kiyama na sharti zake, mvua itakuwa joto, kwa sababu watu watakuwa hawapati faida yake, na kunufaika na kheri yake, hali hii inashabihiana mno na hali ya zama hizi!.

4. Yaani mzinzi atakuwa rafiki wa mzinzi kana kwamba kuna nasaba kati yao.

5. Mradi wake: Hukumu za kiislamu zitakuwa kinyume katika zama hizo.

Hukuwaumba viumbe kwa ukiwa, wala haukuwafanya wafanye kazi kwa ajili ya manu- faa, hautomtaka yeyote na akukose, wala hakuponyoki umshikae[1], wala hapunguzi mamlaka yako anayekuasi, wala hazidishi ufalme wako anayekutii, wala hawezi kuirudisha amri yako mwenye kukasirikia maamuzi yako, na wala hajitoshelezi bila wewe mwenye kugeuka mbali na amri yako. Kila siri Kwako ni dhahiri shahiri, na kila cha ghaibu Kwako kipo mbele yako.

Wewe ni wa milele hauna mwisho, Wewe ndio lengo hakuna jinsi ya kukuepuka, na Wewe ndio mahali pa ahadi ya marejeo ambapo hakuna jinsi ya kuokoka kwa kukuepuka Wewe ila Kwako Wewe. Mkononi mwako kuna shungi la nywele la kila kiumbe, na Kwako ni marejeo ya kila kiumbe.

Utukufu ni wako adhama ilioje ya mambo yako! Utukufu ni wako adhama ilioje tuyaonayo kwa viumbe wako! Na udogo ulioje kwa kila adhama pembeni mwa uwezo Wako! Kutisha kulikoje kwa tuyaonayo katika ufalme wako! Unyonge ulioje kwenye yale ambayo yameghibu kwetu miongoni mwa mamlaka Yako! Wingi ulioje wa neema yako duniani, ni ndogo ilioje kwa kuilinganisha na neema ya akhera!"

## UFAFANUZI

Amesema: Kila kitu ni chenye kuinyenyekea adhama ya Mungu (s.w.t), na kila kitu huwa kwa kumtegemea Yeye, na hii ndio sifa Yake makh'susi. Yaani: Kuwa Yu ajitosha si muhitaji kutoka kwa chochote, wala hakuna kitu miongoni mwa vitu kinachojitosha bila Yeye asilan.

Imekuja (khabari) katika athari kuwa: Mwenye kujitukuza kupitia asiyekuwa Mungu huwa dhalili. Na mwenye kujikithirisha kupitia asiyekuwa Mungu huwa mchache; Na ilikuwa inasemwa: 'Si fakiri mwenye kujitosheleza kwa Mungu.'

Na Al-Hasan amesema: 'Ajabu ilioje kwa Lutu Nabii wa Mungu! Amesema: "Laiti ningelikuwa na nguvu juu yenu, au nategemea kwenye nguzo yenye nguvu". (11:80) (kwa kujiun- ga na mtu mwenye nguvu aninusuru dhidi yenu) (au nikimbilie kwenye sehemu yenye nguvu). Je wamuona ametaka uimara zaidi na wenye nguvu zaidi kuliko wa Mungu!?

Na wanachuoni wametolea dalili kuthibiti kuwepo kwa Muumba (s.w.t) kutokana na yaliojulishwa na maana ya kauli yake (a.s): "Ni kimbilio la kila mwenye kuvunjika moyo," hiyo ni kwa sababu nyoyo katika hali yake ya dhahiri hukimbilia kurejea kwa muumba wao wakati wa shida na majanga.

Je humuoni mpanda chombo pindi mawimbi yanapochafuka ni vipi anavyomsihi Yeye (swt): "Na inapokufikieni taabu katika bahari, hao mnaowaomba wanapotea, isipokuwa Yeye tu". (17:67).

Kisha akasema (a.s): "Mweye kusema hulisikia tamko lake, na mwenye kunyamaza yuajua siri yake," yaani yeye hujua yaliyo dhahiri na yaliyojificha.

Kisha akasema: 'wa man aasha fa alayhi rizquhu, waman maata fa ilayhi munqalabuhu,' yaani Yeye ndiye mratibu wa ya duniani na ya akhera, na Ndiye Mtoa hukumu wa sehemu zote mbili.

---

1. Yaani hawezi kuponyoka ambaye Mungu (s.w.t) anamtia mkononi kama ambavyo wanaweza kuponyoka waliotiwa mkononi na wafalme wa dunia hii kwa hila.

Amesema (a.s): "Macho hayajapata kukuona hata yaweze kueleza khabari zako, kama ambavyo mtu huelezea kuhusu aliyoyaona, lakini Wewe huna mwanzo wala mwisho, Ulikuwapo kabla ya waelezaji wa kueleza habari Zako".

**SWALI**: Kuna kupingana kati ya haya mambo mawili, je haiwezekani awe yupo (s.w.t) kabla ya wasifiaji wa kueleza khabari zake, pamwe na hali hiyo awe aonwa na macho akishawaumba viumbe, kisha wawe wanamsifu au kumuelezea hali wakimuona wazi wazi kwa macho!

**JIBU**: Kuna kupingana kwa dhahiri, nako ni: Ikiwa Yeye (s.w.t) ni wa milele na sio wa kimwili, yaani Mungu dhati yake sio kitu cha kimwili na wala sio mfano wa kiwa au kiumbe miongoni mwa viumbe visivyokuwa mwili – incorporeal - (mfano wa akili wepesi na uzito) na ambacho si mwili wala-incorporeal, ni muhali kuonwa, kwa hiyo ni muhali kueleza kumhusu kwa njia ya kumuona.

## NA SEHEMU YA KHUTBA KUHUSU MALAIKA

"Ewe Allah! Umewafanya malaika wakae ndani ya mbingu Zako, na umewanyanyua juu mbali na ardhi Yako, wao ndio wakujuao mno katika viumbe Wako, na wakuogopao mno, na walio karibu mno na Wewe; Wao hawajakaa viunoni, wala kubebwa na matumbo ya uzazi, na hawakuumbwa kwa maji duni.

Na wala hawakutawanywa na shaka ya matukio ya wakati, na wao wana nafasi na daraja Kwako, na mkusanyiko wa upendo wao ni kwa ajili Yako, na kukithiri utii wao Kwako, na kutokughafilika na amri Yako. Lau wangeainisha uhalisi wa yaliyofichika kwao kutoka Kwako, wangezihakiri aamali zao, na wangejibeza wenyewe, na wangetambua kuwa hawajakuabudu ukweli wa kukuabudu, na hawajakutii ukweli wa kukutii Wewe.

Utukufu ni Wako, Muumba na mwabudiwa! Kwa uzuri wa balaa lako ulipoumba[1], umeumba nyumba (Jannah) na umejaalia humo dhifa: kinywaji na chakula, wanawake na wahudumu, makasri na mito, mashamba na matunda; hatimaye ulimtuma mlinganiaji analingania huko (Yaani Nabii).

Mlinganiaji hakuitikiwa wala uliyo wapendezesha hawakuyapenda wala hawakuwa na shauku na uliyowatia shauku. Waliuelekea mzoga (mzoga hapa yakusudia dunia), ambao walifedheheshwa kwa kuula.

Na waliungana kuupenda, mwenye kukiashki kitu hupofusha macho yake, na kuufanya moyo wake uwe mgonjwa, kwa hiyo yuangalia kwa jicho ele, na yuasikia kwa sikio lisilosikia, kupenda kumeirarua akili yake, na dunia imeufisha moyo wake, hali nafsi yake imehuzunika kwa ajili yake, kwa hiyo yeye ni mtumwa wa dunia, na mtumwa wa ambaye mkononi mwake mna kitu kutokana nayo, itelezeako naye yuatelezea, ielekeako naye yuaelekea. Haonyeki na muonyaji kwa amri yeyote kutoka kwa Mungu, na wala hawaidhiki na mtoa waadhi yeyote, naye awaona waliochukuliwa na ghururi, kuwa hawana batilisho wala rejea."

1. Balaa: Pengine huwa neema na pengine huwa adhabu. La kwanza huanika kwa kuegemeza wema kwenye balaa, yaani hawajakuabudu ila kushukuru neema zako juu yao.

## KUHUSU KIFO

“Limewafika walilokuwa wakilipuuza, nalo ni kuiacha dunia kumewajia (dunia) ambayo waliifanya iko salama kwao, na wamekifikia akhera kile ambacho walikuwa wanaahidiwa, yaliyowafika hayaelezeki, yamejikusanya kwao mawili: Uchungu wa kifo, na huzuni ya kuiacha (dunia), viungo vyao vya miili vimelegea kwa (mauti), rangi zao zimebadilika (kwa mauti), hatimae kifo kilizidi kuwaingia, mtu anazuilika mbali na uwezo wake wa kutamka, naye yupo kati ya ahali yake akiangaza kwa macho yake, na asikia kwa masikio yake, akili yake ikiwa sahihi, uelewa wake umebaki, anafikiri katika ambayo umri wake ameumaliza, na katika alivyoupeleka muda wake! Yu-akumbuka mali alizozikusanya, aliufumbia macho utafutaji wake[1].

Ameyachukuwa (mali) kwa njia ya halali na kwa njia yenye utata[2] hivyo sasa imemkabili dhambi ya jinsi alivyoikusanya, na amekaribia kuiacha, nayo (mali) yabaki kwa watakaobakia nyuma yake wananeemeka nayo na kustarehe nayo, kwa hiyo kheri na anasa (ya alichochuma) itakuwa ya wengine si yake yeye, na uzito (wa dhambi) utakuwa juu ya mgongo wake.

Mtu amekuwa rehani[3], hivyo yeye anauma vidole vyake akijuta kwa yaliyomdhihirikia wakati wa mauti miongo- ni mwa mambo yake, na atakuwa hapendi ambalo alikuwa analipenda siku za umri wake, na atakuwa anatamani kuwa ambaye alikuwa akimhusudu kwa ajili ya mali na kumuonea wivu, angeihodhi yeye badala yake yeye mwenyewe.

Mauti yangali yanamwingia kwa kasi mwilini mwake, mpaka ulimi wake uwe umechukuliwa na umauti kama masikio yake, yupo kati ya ahali zake hawezi kuongea kwa ulimi wake, wala kusikia kwa masikio yake, yuazungusha macho yake nyusoni mwao, akiona mtikisiko wa ndimi zao, lakini hasikii wanayojibishana. Kisha umauti utazidi kumkaba na kuyashika macho yake kama ulivyoshika masikio yake, na roho itatoka mwilini mwake, na kuwa mzoga mbele ya Ah’li zake, na ahali zake wameingiwa na ukiwa, wakiwa wamefadhaishwa naye, na wanajiweka mbali naye, hamfurahishi mliaji, wala kumjibu mwitaji. Kisha watambeba mpaka kwenye mwanandani ardhini, na kumkabidhi humo kwenye matendo yake, na kukata ziyara yake (kuwa hawaendi kumzuru).”.

## KIYAMA

“Mpaka Kitabu kifikie muda wake, na amri makadirio yake, na kukutan- ishwa viumbe wa mwisho na wa mwanzo, na itakuja amri ya Mungu

---

1. Yaani aliyatafuta mali akiwa amefumba macho. Yaani aliyachukulia mambo ya dini yake kiwepesi katika ukusanyaji mali, hivyo akawa hatofautishi kati ya mali ya halali na ya haramu, kwa hiyo anakuwa kama anafumbia macho, kwa kuwa hamaizi, au ni kwamba alikuwa anafanya hila kwa hila ya ndani zaidi katika utafutaji huo mpaka kuipata, kwa njia ya undani zaidi na kwa hila isiyo dhahiri.

2. Yaani ameyachukuwa kwa njia ya halali na yenye utata, na hili linatiliwa nguvu na maana ya kwanza (amefumba macho).

3. Mtu kustahili kuwa rehani na kushindwa kujinasuwa, maana inakuwa: Mali yake aliy- oikusanya imekuwa milki ya mtu mwingine, kama rehani iliyohama kutoka kwa mmiliki wake na kuwa milki ya mwingine nayo ndio rehani.

apendavyo katika kuwafanya upya viumbe Wake, ataiyumbisha mbingu na kuichana, na ataitikisa ardhi na kuitetemesha, na kuin'goa milima yake na kuivunja vunja, na kwa haiba ya utukufu Wake itagongana yenyewe kwa yenyewe, na kwa hofu ya ukali wake, na atawatoa nje walio ndani yake (ya makaburi), na atawafanya upya baada ya kwisha kwao (kuchakaa kwao).

Na kuwakusanya baada ya kutawanyika kwao, kisha atawapambanua[1]kwa ajili ya kutaka kuwauliza kuhusu amali zilizojficha, na matendo yaliyofichikana, na amewafanya makundi mawili: Hili moja alineemesha na hili la pili analiadhibu.

Ama watiifu atawalipa thawabu ya kuwa karibu Yake, na kuwafanya wa kudumu ndani ya nyumba yake, kiasi kwamba wafikao humo hawatotoka, wala hali haitowabadilisha, wala hawatofikiwa na hofu, wala hawatopatwa na magonjwa, wala hawatopatwa na hatari, wala kusumbuliwa na safari kwa kuwatowa sehemu hadi nyingine.

Ama watenda maasi atawakaribisha kwenye nyumba ya shari mno, na kuwafunga mikono shingoni, na kuzifunga nywele za utosi na nyayo za miguu, na kuwavisha kanzu za lami na vazi la moto, watakuwa katika adhabu ya moto uliokolea, na mlango uliowagubika wahusika wake, katika moto wenye ukali na sauti, na mwale umulikao, na wenye ukelele wa nguvu na wa kutisha, wakaao humo hawatoki, mateka wake hawakom- bolewi kwa fidia, pingu zake hazikatwi. Ile nyumba haina muda kiasi cha kuwa muda ukifika itakwisha, wala muda uliopangwa kwa wale watu hata ufikie mwisho."

## SEHEMU YA KHUTBA IMUELEZAYO NABII (S.A.W.W)

"Aliidharau dunia na kuiona duni na kuidogesha, aliona dunia haina thamani na akaidharau, na alijua kuwa Mungu (s.w.t) amemuepusha nayo kwa hiyari yake **(s.a.w.w)** na ameikunjua kwa wengine ili kuwadharau. Hivyo basi alijiepusha nayo kwa moyo wake, na kufisha utajo wake katika nafsi yake, na alipenda mapambo yake yatoweke mbali na macho yake, ili asichukue kutoka humo vazi la fakhari, au awe anatarajia humo nafasi, amefikisha kwa niaba ya Mola wake Mlezi akitoa udhuru[2], na alitoa nasaha kwa umma wake akionya, na alilingania pepo akibashiri, na alihofisha moto kwa kuhadharisha."

---

1. Atawapambanua: Yaani atawatenga na kuwafanya makundi mawili: 1. Wenye furaha na 2. Wenye shida.

2. Yaani mfikisha hoja itakayochukua nafasi ya udhuru katika kuwaadhibu endapo watakhalifu amri yake.

## AHLUL-BAYT

“Sisi ni mti wa unabii, na mashukio ya risala, na mapishano ya malaika[1], na chimbuko la elimu[2], na chemchemu za hukumu, mwenye kutunusuru na kutupenda atakuwa anangoja rehema, na adui yetu mwenye kutuchukia anangojea adhabu[3].

---

1. Yaani ni mahali pa kupishana kwa maana ya: Akiingia huyu miongoni mwao huyu mwingine anatoka, kwa hiyo anakuwa huyu wa pili kama ni khalifa wa yule wa kwanza, wanapokezana.

2. Kauli yake; ‘na chimbuko la elimu’: Anakusudia hekima au hukumu ya kisharia. Amesema Mtume wa Mungu (s.a.w.w):”Mimi ni jiji la elimu na Ali ni mlango wake, hivyo basi autakaye mji huo na auendee mlango.”.

3. Kwa sababu adhabu itawafika kwa yakini kabisa, wamekuwa kama wanaoingojea, na pia wao wanatazamia mauti, ambayo ni utangulizi wa adhabu, ndio maana amejaalia kuun- gojea kwake ni kungojea litakalofuata baada ya mauti (nalo ni adhabu).

# NAHJUL BALAGHA

## JUZUU YA PILI

### MTARJUMI: HARUNA PINGILI

## 110 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

Na Miongoni Mwa Khutba Zake (a.s) - Ibn Shu'ba ameieleza katika Tuhful-Uqul, uk. 104. Na al-Barqi katika al-Mahasin, uk. 233.

### HUMO ANAELEZEA FARADHI ZA UISLAMU:

"Kwa hakika jambo bora ambalo wanaweza kulifanya wasila kwa Mungu (s.w.t), wafanyao wasila ni kumwamini Yeye na Mjumbe Wake, na jihadi katika njia Yake, kwa kweli hicho ni kilele cha uislamu.

Na neno la ikhlasi kwa kuwa hiyo ni fit'ra; na kutekeleza wajibu wa sala kwa kuwa hiyo ni mila; na kutoa Zaka kwa kuwa hiyo ni faradhi ya wajibu, na kufunga mwezi wa Ramadhani hiyo ni kinga ya kutoadhibiwa; na kuhiji Nyumba na kuiendea kwa ibada ya Umra kwa kuwa mawili hayo yanaondoa ufakiri na yanaosha dhambi; na kuunga udugu kwa kuwa hilo lakithirisha mali na linarefusha umri. Na sadaka ya siri kwa kuwa hilo lasitiri kosa[1].

Na sadaka ya wazi wazi kwa kuwa hilo linazuia kifo kiovu; na matendo mema kwa kuwa yanazuia kuangukia kwenye fedheha.

Kithirisheni kumtaja Mungu kwa kuwa ni utajo mwema, na yafanyieni raghba ambayo (s.w.t) amewaahidi wachamungu kwa kuwa ahadi Yake ni ahadi ya kweli mno, na ongokeni kwa kufuata mwongozo wa Nabii wenu kwa kuwa hiyo ni sera iliyo bora[2].

Fuateni Sunna zake kwa kuwa ni mwongozo bora mno, na jielimisheni Qur'ani kwa kuwa hayo ni maongezi mema mno, na jitahidini kuifahamu kwa kuwa ni kheri ya nyoyo, na jitibuni kwa nuru yake kwa kuwa Qur'ani ni tiba ya vifua, na isomeni vyema kwa kuwa hiyo ni visa vyenye manufaa mno.

Kwa hakika mjuzi atendaye kinyume na ujuzi wake ni kama jahili aliyechanganyikiwa ambaye hang'amui kutokana na ujahili wake, bali hoja dhidi yake ni kubwa mno, na majuto yatamlazimu mno[3], na yeye kwa Mungu ni mlaumiwa mno[4].

---

1. Kusitiri hapa yamaanisha ni kuondoa adhabu iliyostahili kwa thawabu zaidi kuliko alivyostahili dhambi. Na asili ya neno ni: Kusitiri na kufunika na kutokana nalo lapatikana neno kafiri; kwa sababu kafiri huficha ukweli, na bahari huitwa kafiri kwa sababu ya kufunika kwake yaliyo chini yake, na mkulima ameitwa kafiri kwa kuwa anaificha mbegu katika ardhi iliyolimwa.

2. Sera, na katika hadithi:"Wahdu hadya Ammar" - fanyeni sera ya Ammar husemwa: "hada fulanu hadya fulani" yaani fulani amekwenda sera ya fulani.

3. Kwa kuwa mjuzi wakati wa mauti atajuta lau angetenda kulingana na ujuzi wake, hali ikiwa mjinga hajutii hilo.

4. Yaani anastahili kulaumiwa, kwa kuwa alijua kwa hiyo stahili yake ya lawama na adhabu ni kali zaidi, naye atajilaumu sana binafsi mbele ya Mungu kwa kuwa hatopata udhuru utakaokubaliwa.

## MAELEZO

Ametaja (a.s) vitu vinane vyote ni wajibu.Cha kwanza: Kumwamini Mungu na Mtume Wake. Na anakusudia neno imani hapa ni: Kusadiki kutupu moyoni, kwa kuweka kando yasiyokuwa hayo kwa mfano kutam- ka shahada, na matendo ya wajibu, na kuacha mabaya. Na madhehebu ya kundi miongoni mwa wanafalsafa wa itikadi za Kiislamu wamesema kuwa: Kiini cha imani ni: Kusadiki moyoni pekee; na hilo ijapokuwa si madhehebu ya sahibu zetu, wao wangesema: Kuwa Amirul-Mu'minina (a.s) amelileta tamko hili kwa mujibu wa asli ya uwekaji wa kilugha; kwa kuwa imani katika asili ya lugha ni kusadiki. Amesema (s.w.t):

"Wa maa anta bimuuminin Lana walaw kunnaa sadiqiina" - Na wewe hutuamini ijapokuwa tunasema kweli; (12:17), yaani hautotusadiki; tuwe waongo au wakweli. Na kuleta kwake (a.s) tamko hili kwa mujibu wa uwekaji wake kilugha hakubatilishi madhehebu yetu kuhusiana na kinachoitwa imani; kwa kuwa sisi madhehebu yetu ni kuwa sheria imepanua maana ya tamko hili kwa tamko lingine, kama ambavyo madhehebu yetu kuhusu Sala na Zaka na yasiyokuwa hayo mawili, hivyo basi hakuna kinachopingana kati ya madhehebu yetu na alilolileta Amirul- Mu'miniina (a.s).

La pili ni: Jihadi katika njia ya Mungu.

Tatu; Tamko la ikhlasi; yaani: Ash'hadu an laa ilaaha illa llahu wa ash'hadu ana Muhammadar-Rasulu'llah.

Na amesema: Hilo ni umbo; yaani ndilo ambalo watu amewaumba kwalo; na asili yake ni neno la kwanza, kwa kuwa ni tawhiid, na kwa hilo ndio watu wameumbwa kwalo.

Nne: Kudumisha Swala.

Tano: Kutoa zaka.

Sita: Kufunga saumu ya mwezi wa Ramadhani

Saba: Hija na Umra,

Nane: Kuunga udugu, nako ni wajibu, na kuutelekeza ni haramu, amese- ma: "Kwa leta mali na kuikithirisha.".

## SHARTI YA KUCHAPA

Sharti ya kuchapa au kusambaza ni kutaja rejeo hili. haki zote zimehifadhiwa na Taasisi ya Al-Hasanain Taasisi ya Imamu Husein (a.s) Site ya Al-Imaamaini Al-Hassanaini (a.s) ya usambazaji wa utamaduni wa Kiislamu na mafunzo ya Kidini.

## MWISHO WA KITABU

## YALIYOMO

**١ .....................................................NAHJUL BALAGHA**

١ .....................................................JUZUU YA PILI

١ ................................... MTARJUMI: HARUNA PINGILI

٢ ............................................................ DIBAJI

**٥ .....................................................NAHJUL BALAGHA**

٥ .....................................................JUZUU YA PILI

٥ ................................... MTARJUMI: HARUNA PINGILI

٥ ..................... 56 - NA MIONGONI MWA MANENO YAKE (A.S)
SIKU YA SIFFIIN ALIPOWAAMURU WATU KUFANYA SULUHU
٥ ..............................................................

٥ ..................... 57 - NA MIONGONI MWA MANENO YAKE (A.S)
AKIWAPA HABARI KUHUSU MTU ATAKAYEAMRISHA
٦ ............................................ ATUKANWE IMAM (A.S)

٦ .........................58 - NA MIONGONI MWA USEMI WAKE (A.S)

٧ ............................................... 59 - NA ALISEMA (A.S)

٧ ..............................................60 - NA AMESEMA (A.S)

٧ ...............................................61 - NA ALISEMA (A.S.)

٧ ...........................................KUHUSU KHAWARIJ

٧ ............................... 62 - NA KATIKA MANENO YAKE (A.S)

٨ .........................63 - NA MIONGONI MWA SEMI ZAKE (A.S)

٨ ............................... AHADHARISHA FITNA ZA DUNIA

٨ ................... 64 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

٨ ..................KUHUSU KUJIANDAA KWA AJILI YA MAUTI:

**١١ .....................................................NAHJUL BALAGHA**

١١.....................................................JUZUU YA PILI

١١................................... MTARJUMI: HARUNA PINGILI

١١.....................65 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

١١..........KATIKA KUMTAKASA MWENYEZI MUNGU (S.W.T)

١٢................ 66 - NA MIONGONI MWA MANENO YAKE (A.S)
AWAAMBIA SAHABA ZAKE KATIKA BAADHI YA SIKU ZA
١٣.............................................................. SIFFIIN
١٣.......................67 - NA MIONGONI MWA SEMI ZAKE (A.S)
١٤................ 68 - NA MIONGONI MWA MANENO YAKE (A.S)
١٤...................69 - NA MIONGONI MWA MANENO YAKE (A.S)
١٤...................................KUWALAUMU SAHABA ZAKE
**١٥ .....................................................NAHJUL BALAGHA**
١٥.......................................................JUZUU YA PILI
١٥...................................MTARJUMI: HARUNA PINGILI
١٥..............................................70 - NA AMESEMA (A.S)
١٥.......... KATIKA MKESHA WA SIKU ALIYOSHAMBULIWA
١٥....................71 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)
١٥..............................KATIKA KUWALAUMU WA-IRAQI:
١٦....................72 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)
ALIWAELIMISHA WATU NAMNA YA KUMSALIA MTUME WA
١٦............................................................ MUNGU
١٧................. 73 - NA MIONGONI MWA MANENO YAKE (A.S)
١٧... ALIMWAMBIA MARWAN BIN AL-HAKAM HUKO BASRA
١٨.................................74 - NA KATIKA USEMI WAKE (A.S)
١٨.............. WALIPOAZIMIA KUMFANYIA BAI’A UTHMAN
١٨.........................75 - NA MIONGONI MWA SEMI ZAKE (A.S)
ALIPOPATA HABARI KUWA BANI UMAYYAH
١٨......... WANAMTUHUMU KUSHIRIKI DAMU YA UTHMAN
**١٩ .....................................................NAHJUL BALAGHA**
١٩.......................................................JUZUU YA PILI
١٩...................................MTARJUMI: HARUNA PINGILI
١٩....................76 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)
١٩............................................... KUHUSU ZUHUDI

١٩.......................... 77- NA MIONGONI MWA SEMI ZAKE (A.S)
٢٠....................................KUWAHUSU BANI UMAYYAH
٢٠..........................78 - NA MIONGONI MWA SEMI ZAKE (A.S)
٢٠............................ ALIKUWA AKIOMBA KWA DUA HII:
٢٠.....................79 - NA MIONGONI MWA MANENO YAKE (A.S)
٢١.....................80 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)
٢٢.....................81- NA MIONGONI MWA MANENO YAKE (A.S)
٢٢ KUHUSU ZUHUDI (KUTOTILIA MANANI RAHA YA DUNIA)
٢٢..........................82 - NA MIONGONI MWA SEMI ZAKE (A.S)
٢٣...............................KUHUSU DUNIA NA WATU WAKE
**٢٣ ......................................................NAHJUL BALAGHA**
٢٣.........................................................JUZUU YA PILI
٢٣....................................MTARJUMI: HARUNA PINGILI
٢٣......................... 83 - MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)
NAYO NI MIONGONI MWA KHUTBA ZA AJABU, NA HUITWA
٢٣.............................................. ‘AL-GHARRAAU’:
٢٥................................KUTAHADHARISHWA NA DUNIA
٢٦.................................. KUWATANABAHISHA VIUMBE
٢٦.......................................UBORA WA KUKUMBUSHA
٢٨.......................HADHARI YA KITISHO CHA AS-SIIRAAT
MIONGONI MWAYO MAELEZO YA KUUMBWA
٢٩.................................................MWANADAMU
**٣٢ ......................................................NAHJUL BALAGHA**
٣٢.........................................................JUZUU YA PILI
٣٢....................................MTARJUMI: HARUNA PINGILI
٣٢.....................84 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)
٣٢.................. KATIKA KUMUELEZEA AMRU IBNUL-A’AS
٣٢......................... 85 - MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

KATIKA KUMWADHIMISHA MWENYEZI MUNGU NA KUMTUKUZA ........................................................ ٣٢
NA SEHEMU YAKE NYINGINE (YA KHUTBA) KUIELEZEA PEPO ........................................................ ٣٢
86 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S) ...................... ٣٣
KUHUSU WAADHI WA KUJIANDAA KWA AJILI YA ULIMWENGU MWINGINE NA KUFUATA AMRI ZA MUNGU . ٣٣
87 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S) ...................... ٣٤
KUHUSU AMPENDAYE MUNGU MTUKUFU ..................... ٣٤
SIFA ZA MTU FAASIQI ............................................. ٣٦
88 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S) ...................... ٣٧
KATIKA KUELEZEA MAKOSA WALIYONAYO WATU ........ ٣٨
**NAHJUL BALAGHA** ...................................................... **٣٩**
JUZUU YA PILI ........................................................ ٣٩
MTARJUMI: HARUNA PINGILI .................................... ٣٩
89 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S) ..................... ٣٩
AZIELEZEA HALI ZA WATU WALIVYOKUWA KABLA YA BI'ITHA: ........................................................ ٣٩
90 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S) ...................... ٤٠
KUHUSU BAADHI YA SIFA ZA VIUMBE ........................ ٤٠
91 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S) .................. ٤١
IJULIKANAYO KUWA NI KHUTBA YA AL'ASH'BAAHU, NAYO NI MIONGONI MWA KHUTBA TUKUFU MNO: ................. ٤١
KUUMBA ULIMWENGU ........................................... ٤٣
BAADHI YA SEHEMU YA KHUTBA HII HII ..................... ٤٤
MIONGONI MWAYO KUHUSU SIFA YA MALAIKA ........... ٤٥
SEHEMU YA KHUTBA KUHUSU SIFA YA ARDHI NA KUKUNJULIWA KWAKE JUU YA MAJI .......................... ٤٧
**NAHJUL BALAGHA** ...................................................... **٥١**
JUZUU YA PILI ........................................................ ٥١

٥١.................................... MTARJUMI: HARUNA PINGILI

٥١......................... 92 - MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

WATU WALIPOTAKA KUMPA BAI’A BAADA YA KUULIWA
٥١........................................................UTHMANI

٥٢......................... 93 - MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

NDANI YA KHUTBA HII AMIRUL-MU’MININ ANABAINISHA UBORA WAKE NA ELIMU YAKE. NA ANABAINISHA FITNA YA
٥٢.................................................. BANI UMAYYAH

٥٤.....................94 - NA MIONGONI MWA KHUTBA YAKE (A.S)

٥٤....................................... KUHUSU SIFA ZA MANABII

٥٥.....................95 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

٥٥.....................96 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

**٥٧ ...................................................NAHJUL BALAGHA**

٥٧.........................................................JUZUU YA PILI

٥٧.................................... MTARJUMI: HARUNA PINGILI

٥٧.........................97 - MIONGONI MWA MANENO YAKE (A.S)

٥٧.................................... KUWAKEMEA SAHABA ZAKE

٥٩.................... 98 - NA MIONGONI MWA MANENO YAKE (A.S)

٥٩....................... KUHUSU DHULMA YA BANI UMAYYAH

٦٠......................... 99 - MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

٦٠................................ KATIKA KUJIEPUSHA NA DUNIA

٦١....................100 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

٦١..KUMHUSU MTUME WA MUNGU NA AHLUL-BAYT WAKE

**٦٣ ...................................................NAHJUL BALAGHA**

٦٣.........................................................JUZUU YA PILI

٦٣.................................... MTARJUMI: HARUNA PINGILI

٦٣....................101 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

NAYO NI KHUTBA MOJAWAPO AMBAYO NDANI YAKE KUNA
٦٣...................... MAELEZO YA MAPAMBANO YA KIVITA

٦٤....................102 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

٦٤...........KUHUSU MAUDHUI ILEILE YA SIKU YA KIYAMA

NA SEHEMU YA KHUTBA HIIHII KUHUSU TAABU ZA SIKU YA
٦٤.......................................................KIYAMA

٦٤........................ 103 - MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

٦٤................ KUHUSU KUJIEPUSHA NA TAMAA ZA DUNIA

SEHEMU YA KHUTBA HII HII KUHUSU SIFA ZA
٦٥................................................... MWANACHUONI

SEHEMU YA KHUTBA HII HII KUHUSU WAKATI WA
٦٥........................................................ BAADAYE

٦٦....................104 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

MWANZO WA KHOTUBA HII UMETANGULIA KATIKA NAMBA
٦٦............................................................ 33.

**٦٨** .....................................................**NAHJUL BALAGHA**

٦٨.......................................................JUZUU YA PILI

٦٨.................................... MTARJUMI: HARUNA PINGILI

٦٨........................ 105 - MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

KUHUSU BAADHI YA SIFA ZA NABII MTUKUFU NA KEMEO
٦٨........ KWA BANI UMAYYAH NA MAWAIDHA KWA WATU

٦٩................................... KUHUSU SHUGHULI ZA IMAM

٧٠....................106 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

HUMO ANABAINISHA UBORA WA UISLAMU, NA AMTAJA MTUKUFU MTUME (S.A.W.W) KISHA ANAWALAUMU
٧٠.....................................................SAHABA ZAKE:

NA SEHEMU YA KHUTBA NI KUMUELEZA NABII (S.A.W.W):
٧٠............................................................

٧١....... MIONGONI MWAYO AKIWAHUTUBIA SAHIBA ZAKE

٧١....................107 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

٧١..................................... BAADHI YA SIKU ZA SIFFIIN

**٧٣** .....................................................**NAHJUL BALAGHA**

٧٣.......................................................JUZUU YA PILI

٧٣.................................... MTARJUMI: HARUNA PINGILI

٧٣....................108 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

NAYO NI KHUTBA YA HALI YA MABADILIKO, YAANI
٧٣...................................MATUKIO MAKUBWA VITANI

NA SEHEMU YA KHUTBA HII NI MAELEZO KUHUSU NABII
٧٣........................................................... (S.A.W.W)

٧٤............................................... MIONGONI MWAYO

٧٥....................109 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

٧٦......................................................... UFAFANUZI

٧٧................NA SEHEMU YA KHUTBA KUHUSU MALAIKA

٧٨...................................................... KUHUSU KIFO

٧٨............................................................KIYAMA

٧٩...... SEHEMU YA KHUTBA IMUELEZAYO NABII (S.A.W.W)

٨٠...................................................... AHLUL-BAYT

**٨١ ....................................................NAHJUL BALAGHA**

٨١.......................................................JUZUU YA PILI

٨١.................................... MTARJUMI: HARUNA PINGILI

٨١....................110 - NA MIONGONI MWA KHUTBA ZAKE (A.S)

٨١..................HUMO ANAELEZEA FARADHI ZA UISLAMU:

٨٢..........................................................MAELEZO

٨٢.........................................SHARTI YA KUCHAPA

٨٢............................................ MWISHO WA KITABU

٨٣......................................................... YALIYOMO